Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini na Nane - Tarehe 19 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpassa) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, itakumbukwa kuwa katika Vikao vyake vya tarehe 8 - 9 Juni, 2004, Bunge hili la Bajeti lilipitisha Miswada ya Sheria ya Serikali iitwayo, *The Written Laws Miscellaneous Amendment Bill, 2004* na *The Electoral Laws Miscellaneous Amendment Bill, 2004.* Miswada hiyo tayari imepata kibali cha Mheshimiwa Rais, Tarehe 15 Julai, 2004 na sasa ni Sheria Na.12 na Na.13 ya mwaka 2004. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 267

### Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Je, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata yataanza kazi lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.4 ya mwaka 1999, pamoja na Sheria ya Mabaraza ya Migogoro ya Ardhi ya mwaka 2002, yaani *The Land Disputes Court Act, 2002 Na.2 of 2002,* Mabaraza ya Vijiji na Kata yalianza kazi rasmi tangu tarehe 1 Oktoba, 2003, kufuatia tangazo la Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi katika Gazeti la Serikali Na.223 la Tarehe 8 Agosti, 2003. Wakati nikijibu swali Na.69 lililoulizwa na Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido tarehe 18 Juni, 2004 kuhusiana na Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa, baadhi ya Halmashauri kwa sasa zimeshaanzisha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji kama vile Rungwe, Baridi na Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumjulisha Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Wananchi wote kwa ujumla kwamba, Ofisi yangu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imekwisha sambaza kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri, Waraka wenye Kumbukumbu Na.CHB.90/215/05/25 wa tarehe 17 Juni, 2004 kuhusiana na utekelezaji wa Sheria Na.2 ya mwaka 2002. Aidha, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, nayo imekwishatoa nyaraka mbalimbali kuhusiana na utekelezaji wa kisheria wa Mabaraza hayo. Waraka huo wa TAMISEMI unahimiza uundaji na kusimamia uendeshaji wa Mabaraza ya Vijiji na Kata. Ni tumaini la Serikali kuwa, sasa migogoro ya ardhi itafikishwa katika vyombo hivi kwa utatuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Mabaraza ya Vijiji na yale ya Kata kwa maana ya shughuli za kila siku, yatasimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, lakini kwa maana ya miongozo ya kisheria na kanuni za kisheria, Waziri mwenye dhamana ataendelea kutoa miongozo hiyo ili kuwezesha majukumu haya kuweza kukamilishwa vizuri.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kabla ya kuondoka Mabaraza haya, Serikali za Vijiji na Mahakama zilikuwa zinatoa maamuzi katika migogoro ya ardhi na mashamba, lakini sasa hivi kazi hizo zimesitishwa kwa upande wa Serikali za Vijiji,

lakini zinatakiwa kufanywa na Mabaraza ya Ardhi ambayo kwa Babati bado hayajaanza hizo kazi. Je, pengo hilo linajazwaje ili kuwatendea haki Wananchi?

Pili, kuwa kuwa Mabaraza ya Ardhi katika ngazi zote kuanzia Vijiji na Kata yanapaswa kutoa maamuzi ya Kisheria. Je, kuna uwezekano wa Mabaraza ya Vijiji kuajiri Wanasheria?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba, kabla ya utaratibu huu kuanza, majukumu haya yalikuwa yanatekelezwa upande mmoja na Mahakama ya Mwanzo, lakini vilevile Serikali za Vijiji nazo zilikuwa na taratibu zake za kutatua migogoro hiyo, lakini baada ya Sheria hii kupitishwa mwaka 2002, pamoja na Sheria za Ardhi zile mbili nilizozitaja, zilizokuwa zimetoa mamlaka kwa vyombo hivyo, sasa zimetaka mamlaka hayo yasitishwe na badala yake sasa Mabaraza hayo niliyoyataja ndio yatachukua jukumu la kutekeleza majukumu hayo.

Kuhusu swali la pili juu ya Mabaraza haya ambayo yatakuwa yanatekeleza majukumu yake kwa upande mmoja kwa misingi ya kisheria na kwamba pengine ingekuwa vizuri basi tukawepo Wanasheria kuweza kufanya kazi za kuwasaidia, taratibu au sheria inakataa kabisa kuingiza Wanasheria katika Mabaraza ya Vijiji na Mabaraza ya Kata. Hii nadhani ni kuwawezesha tu Wananchi katika maeneo hayo waweze kutekeleza majukumu yao kwa viwango ambavyo vinazingatia hali halisi katika maeneo yao. Lakini naomba niongeze tu kwamba, Mabaraza ya Vijiji baada ya kuamua mambo yake, bado mwananchi anaruhusiwa kukata Rufaa kwenda kwenye Mabaraza ya Kata. Kwa upande wa Mabaraza ya Kata, hayatatekeleza amri ile inayotakiwa kutekelezwa kwa maana ya adhabu mpaka iwe imethibitishwa kwanza na Mahakama ya Wilaya inayoshughulikia masuala ya ardhi na nyumba.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina swali moja la nyongeza. Katika Mkutano huu wa Bunge, Naibu Waziri alijibu swali langu linalofanana na hili ya kwamba, chombo gani kinawajibika katika uendeshaji wa kifedha wa Mabaraza haya, jibu lilikuwa kwamba, sheria husika huwa inataja nani anayehusika katika kugharamia uendeshaji. Katika uchunguzi wangu wa sheria zinazohusika, sikuona jambo kama hilo. Lakini leo Waziri amekiri kwamba, Wizara yake inawajibika moja kwa moja katika uendeshaji wa Mabaraza haya. Sasa naomba aliambie Bunge hili kama Wizara imetenga fedha za uendeshaji wa Baraza mwaka huu wa fedha unaoanzia Julai, 2004 ikiwezekana na kiasi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nilipojibu swali linalohusiana na Mabaraza ya Vijiji nilisema kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na maana yangu hasa ilikuwa ni kwamba, Sheria ile ya Ardhi imeeleza waziwazi kwamba, Waziri mwenye dhamana, ambaye ni Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, ataendelea kuwa ndiye msimamizi wa jumla wa Mabaraza haya katika ngazi ya Vijiji pamoja na Kata, lakini nimeongeza leo hapa kwamba, TAMISEMI kwa upande wake, itashughulikia masuala ya usimamizi wa kila siku katika kuhakikisha kwamba,

Halmashauri inateua Wajumbe kulingana na sheria zinavyotaka. Sasa kuhusiana na suala la fedha, ninaloweza kumwambia tu Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, pale panapohitajika masuala ya fedha kuhusishwa katika Mabaraza haya, basi TAMISEMI, pamoja na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, tutashirikiana kuhakikisha kwamba, tunatatua tatizo hilo. *(Makofi)*

Na. 268

**Ajira za Vijana kwenye Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2001, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilitangaza nafasi za kazi kwa vijana kote nchini kupitia Wilayani; na kwa kuwa vijana wengi kutoka Mkoa wa Pwani walijitokeza kuomba nafasi hizo; na kwa kuwa katika zoezi la kuwachuja vijana wote walioomba nafasi hizo walipewa mazoezi ya kukimbia na kwa bahati mbaya sana katika zoezi hilo vijana watatu wa Mkoa wa Pwani walifariki dunia kutokana na kutochungwa afya zao kabla ya kuanza zoezi hilo:-

(a) Je, Serikali inatoa maelezo gani juu ya tukio hilo la kusikitisha?

(b) Je, Serikali ina mipango gani ya kuhakikisha kwamba tukio kama hilo halitokei tena?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa mwaka 2001, Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ilitangaza nafasi za kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana nchini kote. Vijana wengi wa Mkoa wa Pwani walijiandikisha na kuhudhuria usaili na wale walioweza kutimiza masharti walichaguliwa kulingana na nafasi zilizokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usaili kwa vijana wanaoomba kujiunga na Jeshi, kwa kawaida huanzia katika ngazi ya Wilaya, ambapo Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya husika, huwachuja baada ya kufanyiwa *Medical Examination* na Mganga wa Serikali wa Wilaya, ili kujua afya zao kabla ya kupelekwa Mkoani. Wakifika Makao Makuu ya Mkoa, hufanyiwa *physical test* na baadaye *medical test* tena ili kuhakikisha kuwa ni wale walio timamu kimwili na kiafya tu ndio wanaochaguliwa kujiunga na Jeshi. Usaili huu husimamiwa na Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa pamoja na Kamati Maalum kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika ngazi ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza usaili, upande wa utimamu wa mwili *(Physical Fitness),* vijana waliojiandikisha katika Mkoa wa Pwani walikimbia umbali wa Kilometa saba tarehe 6 Desemba, 2001. Katika zoezi hilo, bahati mbaya vijana watatu walifariki dunia katika nyakati tofauti baada ya kufikishwa katika Hospitali ya Tumbi. Vijana hao ni Athuman Ahmad Suleiman kutoka Mafia, ambaye alifariki siku hiyo hiyo mchana, Heriel Elamani Mgonja kutoka Kibaha, ambaye pia alifariki siku hiyo hiyo usiku na Andrea John Jackson kutoka Mkuranga, ambaye alifariki tarehe 11 Desemba, 2002. Uchunguzi wa Daktari ulionesha kwamba, vifo vyao vilitokana na Ugonjwa wa Malaria, Kisukari na njaa, kwani mmojawapo alikuwa amefunga siku hiyo. Serikali ilichukua jukumu la kusaidia katika mazishi ya vijana hawa na kwa kweli ilisikitishwa sana na taarifa ya vifo vya vijana ambao walikuwa wamejitolea kuitumikia nchi yetu kupitia Jeshi la Kujenga Taifa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba, tukio kama hilo halitokei tena, Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, itaendelea kuhakikisha kuwa, watahiniwa wanapimwa kikamilifu kwenye ngazi ya Wilaya na Mkoa ili kujua afya zao kabla ya kushiriki katika mazoezi ya kupima utimamu wa mwili. Aidha, kwa upande mwingine, tutaendelea kuwasisitizia vijana hawa nao kusaidia Kamati hizo kutoa maelezo ya uwazi zaidi badala pengine ya kutanguliza sana suala la kujiunga na JKT na hivyo wakati mwingine kuinyima Kamati na Madaktari fursa ya kujua hali zao za kiafya. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtu yeyote mwenye akili timamu, sio tu Daktari, unapomwambia mtu zoezi lako ni kukimbia, lazima kwanza umfanyie *medical check up,* vijana hawa nikiwa na ushahidi, hawakufanyiwa *medical check up* wakafariki. Je, Serikali iko tayari kuomba msamaha? *(Kicheko)*

Pili, vijana hawa kabla ya kukimbia hawakulishwa na kwa sababu kulikuwa hakuna mtu anayejua masuala ya mazoezi na michezo na unajua bila kufanya mazoezi ukikimbizwa utakufa. Je, Serikali siku nyingine itatafuta utaratibu mzuri kwa sababu kufa kwa mtu sio kufa kwa gari? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa kwamba, tukio hili Serikali ililichukua kwa masikitiko makubwa sana. Nasema ilikuwa ni ajali, haikuwa nia ya Serikali hata kidogo. Kwa hiyo, kuitaka Serikali iombe msamaha katika mazingira ambayo nia hasa ya kutaka vijana wajiunge na Jeshi la Kujenga Taifa ni nzuri, inakuwa ni kuitaka Serikali kuibana kupita kiasi. Mimi nafikiri Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, tukubali kwamba, hili jambo halikunuiwa na Serikali hata kidogo, ni bahati mbaya. *(Makofi)*

Lakini pili, kwamba, vijana hawa waliwekwa bila kula chakula na ndiyo maana ikasababisha vifo hivi, kama hoja kwa kweli ingekuwa ni hiyo, basi pengine asingekufa mmoja tu kwa hali ya njaa, wangekufa wengi tu kama hoja ndiyo hiyo. Taarifa tulizonazo zinasema wazi kwamba, yupo kijana mmoja ambaye wakati huo alikuwa amefunga na kwa bahati mbaya hakusema hili kwa Daktari wala kwenye Kamati. Sasa

zoezi ni zoezi na ndio maana maafa haya yalitokea. Kwa hiyo, ninachoweza kusema tu, tusaidiane. Serikali kwa upande wetu tutajitahidi kuhimiza taratibu zizingatiwe, lakini narudia kusema na kwa upande wa vijana, shauku isiwe Jeshi la Kujenga Taifa tu kwa vile ni upenyo wa ajira, lakini tuwe wawazi zaidi ili tuweze kusaidiana kutekeleza azma nzuri ya Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa vifo hivi ni sawa na ajali kazini, je, Serikali itakuwa tayari kutoa hata fidia kwa wazazi wao kama ubani? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya vijana hawa walikuwa ndio kwanza wanajaribu kutafuta namna ya kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Kama ambavyo mliwahi kumsikia Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), sio ajira hata kidogo. JKT ni chombo kilichowekwa pale kuwasaidia vijana wetu waweze kujua namna ya kujiajiri wao wenyewe. Kwa maana hiyo basi, maafa yaliyotokea hayawezi kuendana na fidia kwa mujibu wa taratibu zetu za Kisheria, kwa sababu hawakuwa wameajiriwa na Jeshi kama Jeshi linavyotakiwa. Lakini bado tunarudia kusema kwamba, Serikali inasikitika sana kwa jambo hili na tutahakikisha huko tunakokwenda, tunashirikiana zaidi ili kuhakikisha kwamba, mambo kama haya hayatokei.

Na. 269

**Elimu ya Hifadhi ya Mazingira**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa Elimu ya Juu ya Hifadhi ya Mazingira inayotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Hai imeleta mwamko mkubwa na Wananchi wameanza kuelewa umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti:-

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kulisaidia Jimbo la Siha kupata vitalu vya miche mbalimbali ili kuzuia hali ya jangwa isije kujitokeza hasa ikizingatiwa kuwa uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai ni mdogo?

(b) Je, kuna programu ambazo zinasaidiwa na Wahisani kutoka nchini na nje ya nchi na je, watakuwa tayari kusaidia programu ya upandaji miti katika Jimbo la Siha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Serikali imekuwa ikihamasisha Wananchi ili kuelewa na hivyo kushiriki kikamilifu katika masuala mbalimbali ya hifadhi na utunzaji wa mazingira likiwemo suala la ukuzaji miche ya miti, kuipanda na kuihudumia. Uhamasishaji huu pia umewezesha vikundi vya vijana kukuza miche ya miti na kuiuza ili kujipatia kipato. Utaratibu huu ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira unaozingatia umuhimu wa ushirikishwaji wa Wananchi katika Hifadhi ya Mazingira na hali halisi ya kujipatia mahitaji yao ya kila siku kutokana na rasilimali zilizo ndani ya mazingira wanamoishi.

Wilaya ya Hai lilipo Jimbo la Siha, linatekeleza kwa juhudi kubwa, kampeni ya Kitaifa ya upandaji miti na Wananchi hukuza miche katika vitalu vyao katika ngazi ya familia, Vijiji na hata ngazi ya Wilaya. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2001/2002, Wilaya ya Hai ilipanda miche 508,060 na katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wilaya ya Hai ilipanda miche 1,180,000 na pia Wilaya ina jumla ya vitalu 112 vya kukuzia miche ya miti na kati ya vitalu hivyo ni vitalu 12 tu ndio vinamilikiwa na Serikali, vilivyobakia vinamilikiwa na Asasi za Dini sita, *NGOs* kumi, Vikundi vya Jamii kumi na Wananchi mmoja mmoja 32 na vitalu 57 kati ya hivyo viko katika Jimbo la Siha.

Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba, juhudi za Halmashauri ya Wilaya ya Hai kuhusu Elimu ya Uhifadhi Mazingira na Kupanda Miti, zimeleta mwamko mkubwa kwa Wananchi katika Jimbo la Siha na Wilaya ya Hai kwa ujumla. Aidha, ukuzaji wa miche ya miti katika shamba la miti la *West Kilimanjaro,* umechangia kwa kiasi kikubwa, uelewa wa Wananchi wa Jimbo la Siha katika kuhifadhi mazingira na upandaji wa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuzingatia mchango mkubwa wa Wananchi katika Hifadhi ya Mazingira na Upandaji Miti, Serikali itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Hai katika juhudi zake za kuhamasisha Wananchi ili waendeleze juhudi zao za kujitegemea katika kuanzisha na kuendeleza vitalu vidogo vidogo vya miti na hatimaye kukidhi mahitaji yao ya miche ya miti. Aidha, kwa kuzingatia mafanikio hayo ya upandaji miti na Hifadhi ya Mazingira, ni matarajio yangu kwamba, Wananchi wa Jimbo la Siha wataendelea kushirikiana na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Hai kuendeleza juhudi hizi.

(b) Kwa kuwa miongoni mwa matatizo yanayoikabili Tanzania ni pamoja na upotevu wa bioanuwai, kutoweka kwa misitu na uharibifu wa ardhi, Serikali inaendelea kubuni na kuratibu programu mbalimbali za upandaji miti. Katika kuandaa na kuratibu programu hizo, kipaumbele huelekezwa kwa maeneo ambayo yanakabiliwa na uharibifu mkubwa wa ardhi na ukataji miti ovyo. Kwa mfano, kutokana na uharibifu wa mazingira uliokuwa unaikabili Wilaya ya Hai, hasa eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, mwaka 1986 hadi 1998, Serikali ya Japan kupitia Shirika la *FAO,* ilisaidia kufanikisha programu ya upandaji miti kandokando ya barabara itokayo Moshi kwenda

Arusha na katika maeneo ya Uwanja wa Ndege. Pia Shamba la Miti la Taifa la *West Kilimanjaro* lililopo katika Jimbo la Siha, limekuwa likitoa miche ya miti bure kwa Wananchi. Serikali ya Sweden, ilitoa misaada kwa miaka mingi kuendeshea shughuli za shamba hilo.

Aidha, Serikali inaendeleza juhudi zake za kuhamasisha Wananchi wajitegemee katika kutekeleza kampeni mbalimbali za hifadhi ya mazingira ikiwemo ile ya upandaji miti na pale Wahisani wa ndani na nje wanapopatikana, Serikali itawashauri wasaidie maeneo yenye matatizo ya mazingira ikiwa ni pamoja na maeneo ya Jimbo la Siha. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Ninaomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa.

Kwa kuwa amekubali kwamba tutashirikiana kuona ni namna gani tutaweza kulisaidia Jimbo la Siha katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na utaratibu na programu za kupanda miti; na kwa kuwa Jimbo la Siha ndicho chanzo cha maji na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo anajua jambo hili; je, anakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kutoa msaada mahususi kwa ajili ya Jimbo la Siha na je, atakuwa tayari tutakapomaliza kikao hiki tuongozane ili aweze kuniambia *specifically* ni nani hao anaotarajia kwamba wanaweza wakashirikiana na Jimbo la Siha katika upandaji wa miti? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwishasema kwamba, ni azma ya Serikali kusaidiana na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote katika jitihada zetu za kuhifadhi mazingira. Pale anaposema mahususi katika suala linalohusu chanzo cha maji, hapa ndio tunapaswa kusisitiza zaidi juu ya uhifadhi wa mazingira. Sasa kuhusu msaada mahususi, ningependa niseme kwamba, tutafanya hivyo pindi tutakapokuwa tunapata uwezo. Naomba tu nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba, tumeipitisha Bajeti ya Serikali, lakini wote tunafahamu ni asilimia 41 ya Bajeti hiyo ambayo ni tegemezi. Kwa hiyo, tukiweza kuziba hili pengo la asilimia 41, haya tunayoyatarajia tunaweza tukayafanya bila matatizo makubwa kama ilivyo hivi sasa.

Na.270

**Ujenzi wa Sekondari kwa Nguvu za Wananchi**

**MHE. OMAR M. MWENDA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi wanatambua umuhimu wa elimu na kwamba ni kichocheo cha maendeleo, kwa hiyo, wanahamasika kujenga Shule za Sekondari za kutwa lakini wameshindwa kukamilisha baadhi ya majengo kwa mfano Maabara, nyumba za Walimu na Hospitali; na kwa kuwa Halmashauri za Wilaya zimeshindwa kusaidia; na kwa kuwa

tunakwenda na Sayansi na Teknolojia na Sekondari kukosa Maabara hakutasaidia sana maendeleo yaliyokusudiwa:-

Je, Serikali itakubaliana nami kuwa sasa wakati umefika wa Serikali kubeba mzigo wa kujenga majengo yaliyobaki kwa kila Sekondari?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA - k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Mwenda, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wananchi wengi wanatambua umuhimu wa elimu katika ukuaji wa uchumi na kuondoa umaskini. Kutokana na ukweli huo, Wananchi wa sehemu mbalimbali nchini, sasa wamehamasika kujenga Shule za Sekondari za kutwa na ni kweli pia kuwa kasi ya mahitaji ya elimu bora ni kubwa kuliko uwezo wa Wananchi wa kujenga majengo yote muhimu ya Shule za Sekondari kama vile madarasa, maabara na nyumba za walimu.

Serikali inatambua ukweli huo na ndio maana katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari kwa kipindi cha mwaka 2004 - 2009, Serikali itatoa ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya Shule za Sekondari za Serikali zinazojengwa na Wananchi ya Shilingi milioni saba kwa ajili ya ujenzi wa darasa na Shilingi milioni tisa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa maabara na maktaba utakuwa kwa zabuni ya Serikali ngazi ya Wilaya. Pia Serikali itasaidia ujenzi wa hosteli pale inapohitajika kwa kulipia vifaa vya ujenzi vinavyotengenezwa viwandaji. Kwa hiyo, pamoja na Wananchi kuchangia nguvu zao, Serikali pia imebeba mzigo mkubwa wa kujenga majengo ya Shule hususan majengo ya maabara na maktaba ili kutoa elimu bora katika ngazi hii ya Sekondari itakayosaidia sana kuleta maendeleo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

**MHE. OMAR M. MWENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pamoja na hayo, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Shule ya Matanda iliyopo Kata ya Lihimalyao haina maabara wala haina hosteli wala haina nyumba za walimu. Je, yuko tayari kutoa fungu la pesa kupeleka huko kwa shughuli hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza mpango wa Serikali kuchangia nguvu za Wananchi kama alivyouliza, lakini nimesema tunaanza utaratibu huo katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2004 hadi 2009. Kwa hiyo, ningemwomba basi tuvute subira kwa sababu tumejiwekea utaratibu wa kulishughulikia hilo kama alivyouliza.

Nina hakika wapiga kura wa jimbo lake, watakuwa wamesikia azma ya Serikali na si kwa maneno, tunafanya kwa vitendo.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sasa hivi lalamiko kubwa kutoka kwa kila Mbunge katika Bunge lako Tukufu ni kuhusu majengo ya zamani ambayo yako katika hali mbaya; na kwa kuwa tunapoanza mpango wa MMES inawezekana kuingiliana kwa kazi hizi mbili, kurekebisha majengo yaliyopo ambayo yameshindikana kwa muda mrefu na mpango mpya wa kujenga majengo mapya kunaweza kukaleta mtafaruku ambao pengine utatupa shida katika kukamilisha malengo tuliyonayo; je, Serikali iko tayari kuunda Kamati au Tume ya kuzungukia nchi nzima kuweza kutathmini hali ya majengo ya zamani ili kazi itakayofanyika iwe inajulikana vyema kuliko tunavyofikiria sasa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, tunayo majengo ya zamani na yana hali mbaya na anachopendekeza kwamba Serikali iko tayari kuunda Kamati kuzungukia nchi nzima ili kuona hali hiyo, ningependa niseme kwamba, kwanza ni kweli baadhi ya majengo wala si ya skuli zetu au shule zetu tu yaliyo katika hali mbaya. Majengo mengi ambamo zinatolewa huduma za jamii, mengi ya majengo haya mengine yana hali mbaya. Lakini niseme hali hii tunaifahamu na kinachofanya hali iendelee kuwa kama tunavyoiona ni kile nilichokisema, nakisi katika Bajeti yetu kihali halisi lakini jawabu lake si kuunda Kamati ya kuzunguka nchi nzima, maana nina hakika Kamati hiyo nayo itakuwa na gharama zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali inao utaratibu wa kujua mambo haya tunayoyazungumza katika mtandao kwa mfano wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, majengo haya yanafahamika kupitia maafisa wetu wa Wizara ya Elimu ngazi ya Wilaya. Kwa hiyo, tunapokuwa tunalifanya hili na kwa sababu tunafahamu, tutayachukua yote kwa pamoja na tutajitahidi kupunguza gharama kuliko kuunda Kamati nyingine ambayo itakuwa kwa kweli ni chanzo cha kupunguza hata kile kiasi tunachokielekeza huko. *(Makofi)*

Na. 271

**Wanafunzi katika Shule za Msingi**

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa wanafunzi wanaosoma katika shule za msingi za Serikali na zile za binafsi hufanya mtihani ule ule wa Taifa wa Darasa la Saba na baadhi ya wanafunzi wanaofaulu kutoka kwenye shule hizo huchaguliwa kuingia katika Sekondari za Serikali:-

(a) Je, ni wanafunzi wangapi wa shule za msingi za Serikali na za binafsi katika Mkoa wa Dar es Salaam walifanya mitihani ya darasa la saba katika mwaka 2003,

ni wangapi walifaulu mtihani huo na wangapi walichaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule za sekondari za Serikali?

(b) Kwa kuwa idadi kubwa ya wanafunzi wasomao katika shule za msingi binafsi ni wale ambao wazazi wao wana uwezo na wengi wao hufaulu vizuri zaidi kutokana na mazingira mazuri ya kusomea yatokanayo na uwezo wa wazazi wao na si kwa sababu ya kuwa na akili zaidi, je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuleta usawa na uwiano kati ya watoto wasio na uwezo (wanaosoma shule za msingi za Serikali) na watoto wenye uwezo, kwa kuamua kuwa wale watoto wanaosoma kwenye shule binafsi waendelee na masomo yao kwenye sekondari binafsi wasiingie katika sekondari za Serikali ili waachie nafasi kwa watoto ambao wanafaulu katika shule za msingi za Serikali wapate nafasi ya kutosha katika sekondari za Serikali, kwa sababu wazazi wao hawawezi kuwalipia katika sekondari binafsi na kwamba uamuzi huo uwe wa miaka kumi au kumi na tano hadi Sekondari za Serikali zitakapokuwa nyingi nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA - k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2003 katika Mkoa wa Dar es Salaam waliofanya mtihani wa darasa la saba na waliofaulu ni kama ifuatavyo:-

| Aina ya shule | Waliofanya | Waliofaulu | Waliochaguliwa | Asilimia waliochaguliwa |
|---|---|---|---|---|
| Za Serikali | 34,981 | 14,709 | 4,276 | 29.1 |
| Za Binafsi | 1,250 | 1,110 | 512 | 46.1 |
| Jumla | 36,231 | 15,819 | 4,788 | 30.2 |

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na takwimu hizo shule za msingi za serikali zilitoa wanafunzi 4276 sawa na asilimia 89 kati ya 4788 waliochaguliwa kujaza nafasi za kidato cha kwanza. Kwa hiyo sioni sababu yoyote ya msingi ya kuchukua hatua anazopendekeza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho siyo kuwanyima nafasi za sekondari wanaofaulu kutoka shule za msingi za binafsi zinazodhaniwa kuwa ni bora, bali ni kuboresha elimu ya msingi na sekondari katika shule zote ili watoto wote wapate elimu iliyo bora. Aidha, matokeo ya MMEM yanaonyesha kuwa elimu katika shule zetu za msingi inaendelea kuboreka kwa matokeo ya mwaka 2003 kufaulu kwa asilimia 40.1 kutoka asilimia 27 ya mwaka 2002. Aidha, ili kukabili ongezeko la watoto wanaofaulu darasa la saba, Serikali imebuni Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari wa miaka mitano kuanzia 2004 - 2009, wenye lengo la kuongeza na kuboresha elimu ya sekondari, ili ifikapo 2010, asilimia 50 ya wanaomaliza elimu ya msingi, wapate nafasi ya elimu ya

sekondari, bila kubagua kati ya wale wanaotoka shule zisizo za Serikali na wanaotoka shule za Serikali kwa sababu watoto wote hao ni wetu na ni sehemu ya nguvukazi ya kesho, itakayokuza uchumi wetu kuweza hata kuhimili kulipa madeni tunayokopa sasa kuwaelimishia.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali wengi sana wanaofaulu huachwa, kwa mfano, kwa tarakimu zake zaidi ya 10,000 walifaulu lakini hawakwenda shule za sekondari; na kwa kuwa shule hizi za *private* wamekuwa kwa kiasi fulani wanaziba zile nafasi; je, Serikali itajaribu kuchukua hatua gani ili wazazi wanaosomesha katika shule za *private* waweze vile vile kusaidia ama kujenga shule za sekondari nyingi za binafsi ili kuwepo na uwiano mzuri kidogo kwa sababu wao wana uwezo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, analoliuliza Mheshimiwa Mbunge, liko katika msingi wa kushirikisha sekta binafsi na hasa katika eneo hili la elimu na kama tunavyosema kwamba, elimu ni ufunguo wa maisha, mimi nina hakika kwamba, kama nilivyosema katika jibu la msingi la Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wananchi wamekwisha ng'amua na wanathamini umuhimu wa elimu. Kwa kuwa tunao mpango wa kuboresha elimu ya msingi na kuboresha elimu ya sekondari na nina hakika nimetaja hapa kwamba, hata mchango wa Serikali katika ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, maabara na maktaba, mimi nina hakika kwa sababu tunatambua mchango wa sekta binafsi, hawa wazazi wanaosomesha watoto wao hivi sasa katika shule za binafsi pia sidhani kama watakubali kubaki nyuma katika kuchangia juhudi za Serikali katika suala hili.

Na. 272

**Itifaki**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED)** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Itifaki ilivyoelezewa kwenye Katiba ya Nchi na kutokana na majibu ya Serikali kwa swali Na. 2062 tarehe 13 Novemba, 2002 na kutokana na mahusiano ya nchi na nchi, je, viongozi wetu wanaokwenda nje ya nchi (rasmi) hupokelewa kwa utaratibu gani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mheshimiwa, hakuna Mkataba wa Kimataifa, kuhusu utaratibu wa Itifaki ya mapokezi ya Viongozi wa Kitaifa wanapotembelea nchi nyingine. Hata hivyo, kutokana na mazoea yaliyojengeka miaka mingi katika dunia ya diplomasia, upo utaratibu uliokubalika takriban na Mataifa yote duniani kuhusu mapokezi ya Viongozi wa Kitaifa wanapotembelea nchi nyingine. Kwa mujibu wa utaratibu huo, ziara za viongozi

zipo za aina kuu tatu. Nazo ni ziara rasmi ya Kitaifa *(State Visit)*, ziara rasmi *(Official Visit)* na ziara ya kikazi *(Working Visit).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara ya kikazi *(Working Visit)* ni ile waifanyayo viongozi kwenda nchi nyingine kwa ajili ya kuhudhuria mkutano au shughuli maalum kama vile Rais wetu alivyokwenda Ethiopia hivi karibuni kuhudhuria Mkutano wa Wakuu wa nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika. Ziara rasmi *(Official Visit)* ni ile ambayo kiongozi wa nchi moja huenda nchi nyingine kwa ajili ya mazungumzo au mashauriano kuhusu jambo au mambo fulani yanayowahusu. Ziara rasmi ya Kitaifa ni ile ambayo kiongozi wa nchi moja huenda nchi nyingine kwa ajili ya mazungumzo au mashauriano kuhusu jambo au mambo fulani yanayowahusu wao viongozi, ama zinazozihusu hizo nchi ambayo ni *bilateral.*

Ziara rasmi ya Kitaifa ni ile ambayo kiongozi wa nchi hutembelea nchi nyingine kwa siku kadhaa yenye kuhusisha matembezi na kuona shughuli kadhaa katika nchi hiyo. Ni ziara ambayo hata mapokezi yake huwa rasmi na ya Kitaifa. Kwa kawaida huwepo gwaride rasmi na mizinga hupigwa kulingana na hadhi ya kiongozi huyo, kwa Rais mizinga 21 na kwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu mizinga 19. Katika ziara rasmi ya Kitaifa pia huwepo msafara wa heshima *(Ceremonial Drive)* inayojumuisha miongoni mwa mambo mengine, gari la wazi, pikipiki zisizopungua 12 na mbwembwe nyingi. Vile vile huwepo Dhifa ya Taifa *(State banquent)* na nchi mwenyeji kwa kawaida hugharimia idadi maalum ya Wajumbe wanaofuatana na kiongozi huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kutegemea shughuli aendayo kuifanya kiongozi mhusika atapata mapokezi stahiki. Kwa ziara rasmi ya Kitaifa, kiongozi huyo hupokelewa na mwenyeji wake hasa pale panapofanyika gwaride rasmi. Baadhi ya nchi hufanya gwaride rasmi kiwanjani mara anapofika lakini nchi nyingine hufanyia mahali pengine. Aidha, kutegemea mahali linapofanyika gwaride na mazingira ya nchi husika na mazoea yao katika baadhi ya nchi hakuna msafara wa heshima *(Ceremonial Drive).*

Kwa ziara ya kikazi, kiongozi atapokelewa kwa mujibu wa makubaliano baina ya waandaaji wa mkutano au shughuli husika na Serikali mwenyeji. Mara nyingi nchi mwenyeji hupanga Mawaziri kupokea au kusindikiza viongozi na wakati mwingine hata Maofisa Waandamizi huhusishwa. Kwa ziara rasmi, kiongozi anaweza kupokelewa na mwenyeji wake kiwanjani au anaweza kupokelewa na Waziri au hata Afisa Mwandamizi. *(Makofi)*

Na. 273

**Umeme - Vijiji vya Jimbo la Songwe**

**MHE. PAUL E. NTWINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alipotembelea Wilaya ya Chunya hapo mwaka 2003 aliahidi kuwa umeme toka Makongolosi kwenda Lupa, Mkwajuni na Mkwajuni kwenda Kanga hadi Galula ungekuwa tayari mwaka huu wa 2004; na kwa kuwa kupeleka

umeme sehemu hizo kutaongeza tija katika ukuaji wa uchumi wa Wananchi wa Wilaya ya Chunya hasa ikizingatiwa kuwepo kwa madini mbalimbali kwa wingi kama vile dhahabu, chuma, almasi, makaa ya mawe na kadhalika; na kwa kuwa nguzo zipo tayari kwenye maeneo hayo:-

(a) Je, ni kitu gani kinachochelewesha kazi isifanyike hata ile ya kusimika nguzo ambazo tayari zipo?

(b) Je, ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Hadi kufikia Julai 15, 2004 nguzo zipatazo 15 zilikuwa zimeshafikishwa kwenye eneo la mradi na tayari nguzo 31 zimekwisha kusimamishwa. *(Makofi)*

Mashimo 140 yamechimbwa kwa ajili ya kusimamisha nguzo, kazi hiyo ni sawa na kilomita 14 na kazi bado inaendelea. Kazi ya kukata miti katika njia ya umeme imefanyika kwa kilomita 11. Kama nilivyosema awali, kazi inaendelea, *transformer* nne zinatarajiwa kuwekwa katika vijiji vya Upendo, Mamba A na B, Macha C na D na Lupatingatinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya mradi wa umeme, ujenzi wa laini ya msongo wa kilovoti 33 kutoka Mkwajuni hadi Galula yenye urefu wa kilomita 29 ni kama ifuatavyo:-

Mashimo 42 kwa ajili ya kujengewa nguzo tayari yamechimbwa, nguzo 42 zimesimamishwa, tarehe 16 Julai, 2004 katika kutekeleza ahadi niliyoitoa Bungeni wakati nachangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, nilikutana na Waheshimiwa Wabunge wapatao 12 na kupitia masuala ya umeme katika maeneo yao, wakiwemo Mheshimiwa Paul Ntwina na Mheshimiwa Njelu Kasaka.

Kama tulivyokubaliana katika Mkutano ule, ahadi ya kufikisha umeme Lupa, Kanga, Galula na vijiji vya Jirani, imekwishaanza kutekelezwa na utekelezaji wake hata hivyo utakwenda kwa awamu kama ilivyoelezwa katika Mkutano ule ambao pia ulijumuisha viongozi wa juu wa Shirika la Ugavi wa Umeme nchini *(TANESCO)*.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na kazi kule kuwa inaendelea, mimi nina swali la nyongeza kama ifuatavyo: Kwa kuwa Kijiji cha Mwambani Wananchi wenyewe wamejitolea kutoa umeme Mkwajuni na kuchimbia nguzo karibu kilomita nne. Je, Serikali iko tayari kutambua nguvu zao na kufanya iwe ni mfano wa kuigwa katika sehemu nyingine ambazo huwa wanachimbiwa na Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wananchi wa vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge amewataja kwa juhudi zao za kujitolea kuchimba mashimo haya na kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, ni mfano wa kuigwa katika maeneo mengi ya nchi yetu, kwenye kazi ya kupeleka umeme vijijini na sehemu nyingine, ni kazi yenye gharama kubwa na pale inapobidi huwa tunawaomba Wananchi wajitolee na tunashukuru kwamba, katika eneo hili wamefanya hivyo.

Napenda nichukue nafasi ya pekee kumpongeza sana Mheshimiwa Paul Ntwina, kwa juhudi zake za kuwahamasisha Wananchi na kufuatilia kwa karibu, utekelezaji wa mradi wa umeme wa eneo lake ambalo amelitaja. *(Makofi)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali dogo la nyongeza. Pamoja na kuipongeza Serikali jinsi ilivyosaidiana na Mheshimiwa Ntwina huko Songwe, napenda na mimi kutetea wanawake au wasichana wanaosoma katika shule za sekondari Mkoa wa Mtwara kwa mfano, shule za Kata, Jimbo la Nanyumbu, Sekondari ya Mnyambe, Sekondari ya Kitangari, lini umeme utafika huko? *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali hili naona ni jipya kidogo. Mheshimiwa Waziri kama ana majibu anaweza kusaidia, lakini naona kama hana majibu. Naona hana. Liletwe kwa njia ya kawaida, lakini ni swali zuri Mheshimiwa Lydia Boma, ulilete kwa njia ya kawaida. *(Kicheko)*

Na. 274

**Utabiri wa Hali ya Hewa**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** alijibu:-

Kwa kuwa wataalam wa hali ya hewa wamekuwa wakitoa utabiri ambao haufanani na ukweli kwa sababu ya kutumia vifaa vilivyopitwa na wakati. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wataalam hao vifaa vya kisasa na vya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Utabiri wa uhakika wa hali ya hewa unachangiwa na utumiaji wa vifaa vya kisasa na vya kutosha pamoja na utaalam unaofaa. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, licha ya upungufu mdogo wa vifaa walivyonavyo Mamlaka ya Hali ya Hewa, vingi ni vya kisasa na vinaboreshwa na kuongezwa kila uwezo wa kifedha unapopatikana na pia kuomba kwa wafadhili mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuendelea kuelimisha wafanyakazi wake kwa kutumia bajeti yake na pia kwa msaada wa wafadhili mbalimbali. Lengo kuu ni kuona utaalam wa utabiri unaendana na wakati na teknolojia ya leo. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, licha ya upungufu wa vifaa katika maeneo kadhaa, utabiri unaotolewa ni wa uhakika na wanaotumia taarifa hizo wanafaidika nao. Tutaendelea kuboresha huduma zetu kila mara na kila uwezo utakapopatikana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna kifaa kinachoitwa Rada kinasaidia katika kutoa utabiri wenye uhakika zaidi kuliko vifaa hivi vingine. Je, Serikali itakuwa na mikakati hii lini kuhakikisha kwamba inanunua rada katika kuwawezesha wataalam wetu kutoa utabiri wenye uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimwambie Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba, tunao mradi ambao tumetengeneza na tumepanga kuupeleka kuomba msaada *Europen Union* wa kununua rada saba kwa ajili ya shughuli hizi. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, rada moja inauzwa kwa dola milioni moja. Kwa hiyo, tutahitaji kama milioni nane pamoja na ufungaji wake. Juhudi hizo zinafanywa na zikipatikana tutakujulisha Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuniona. Kwa kuwa Kituo cha Hali ya Hewa kilifunguliwa Singida Mjini mwaka 2003 na kwa kufunguliwa kwake ni kwamba, kilikuwa bado hakijamalizika vizuri pamoja na watumishi waliopo pale na vifaa havitoshi. Ni lini Wizara itakamilisha ujenzi wa kituo hicho pamoja na kukamilisha kuweka watumishi na vifaa vya kutosha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kituo cha Hali ya Hewa kilifunguliwa mwaka 2003 na ninamhakikishia kile kituo ni kituo kamili ambacho kimekamilika na kina vifaa na kinakidhi mahitaji kutokana na hali halisi ya kituo. Tukihisi kama kunahitajika wataalam wa ziada, hatutasita kuwapeleka. *(Makofi)*

Na. 275

**Kuondokana na Matumizi ya Jembe la Mkono**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Dira ya Taifa 2025 ya kuondoa umaskini imeelekeza hatua za mambo muhimu ya kipaumbele ikiwemo elimu, maji, miundombinu (barabara na umeme) na kadhalika, kurahisisha katika mapambano hayo na kwa kuwa kilimo kinaajiri zaidi ya asilimia themani ya Watanzania na kwa kuwa katika dira hiyo haionyeshwi dhahiri namna ya kuondokana na kilimo duni cha kutumia jembe la mkono. Je, ni hatua

gani za makusudi zinalenga kuondokana na matumizi ya jembe la mkono na vishamba vidogo visivyo na tija?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua kwamba, jembe la mkono linapotumiwa kuvunja ardhi katika kilimo, ni moja kati ya vikwazo vinavyofanya kilimo kisikue kwa kasi inayotakiwa. Aidha, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000, inaahidi kuongeza juhudi za kukienzi na kukiendeleza kilimo kwa kuhakikisha kuwa, kanuni za kilimo bora zinafuatwa, zikiwemo zile za matumizi ya zana za kisasa na pembejeo. Ibara ya 15 (iii) na (iv) inasema: "Ili kuweza kufikia malengo haya, CCM katika kipindi kijacho, itahimiza Serikali kufufua na kueneza kilimo cha maksai pamoja na matumizi ya mikokoteni inayovutwa na ng'ombe na punda badala ya mizigo kubebwa na binadamu, hususan wanawake na watoto na suala la kueneza kilimo cha matrekta litawekewa mkakati".

Katika juhudi za kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka wa 2000 na Sera na Mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuanzia mwaka wa 2002/2003, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kukarabati vituo vya kufundishia maksai na kuwafundisha wakulima matumizi ya wanyamakazi. Katika mwaka wa 2003/2004, vituo 25 vilikarabatiwa na kupatiwa vitendea kazi. Kwa maeneo yenye mifugo, juhudi zitawekwa katika kupanua kilimo cha wanyamakazi na baadhi ya mikoa imepiga hatua kubwa katika eneo hili. Mikoa inayoongoza ni pamoja na Singida, Rukwa na Shinyanga.

(b) Katika mwaka wa 2003/2004, Serikali ilianza kutenga fedha kupitia kwenye Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, kwa ajili ya kuwakopesha wakulima ili kuwawezesha kununua matrekta mapya na kukarabati matrekta mabovu. Inakisiwa kwamba, kuna matrekta mabovu zaidi ya 6,000 ambayo yanatengenezeka. Aidha, Mfuko unatoa mikopo ya kununulia zana za kilimo zinazotumiwa na wanyamakazi.

Katika mwaka wa 2003/2004, Mfuko wa Pembejeo ulitoa mikopo saba yenye thamani ya shilingi 186,450,000/=, kwa ajili ya kununulia matrekta mapya kumi na matano. Aidha, Mfuko ulitoa mikopo kwa ajili ya kuanzisha vituo viwili vya matrekta. Tunaamini kwamba, uanzishaji wa vituo vya kilimo vitakavyowapa wakulima huduma mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukodishia matrekta, ndiyo njia bora zaidi ya kuendeleza kilimo cha matrekta kuliko ile ya kukopesha trekta moja moja. Katika mwaka uliopita, mfuko ulitoa mikopo 103 yenye thamani ya shilingi milioni 452,203,146/= kwa ajili ya kukarabati matrekta 103. *(Kicheko)*

Serikali imekuwa ikiwahimiza Wananchi na wafanyabiashara kuagiza matrekta na mashine nyingine za kilimo kwa wingi yakiwamo matrekta mapya, yaliyotumika na yaliyokarabatiwa. Aidha, Wizara imekuwa ikitafuta habari juu ya upatikanaji wa matrekta, bei za matrekta na kadhalika na kuzitumia kuwashauri watu wanaotaka kuagiza matrekta. Nakipongeza Chama cha Wafanyabiashara wa Pamba Tanzania *(Tanzania Cotton Association),* kwa uamuzi wake wa kila *ginnery* kununua matrekta ya kuwalimia wakulima wanaozunguka *ginnery* hizo.

Matrekta 30 kati ya 100 yanatarajiwa kuwasili nchini wakati wowote kuanzia sasa. Kufuatia hatua mbalimbali ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Serikali, idadi ya matrekta na zana za kilimo zinazoingizwa nchini imekuwa ikiongezeka.

Kwa mfano, kati ya mwaka 2000 na 2003, matrekta 1,080 yaliingizwa nchini ikilinganishwa na wastani wa matrekta 50 tu yaliyokuwa yanaingizwa nchini kwa mwaka katika miaka mitatu iliyotangulia.

Baadhi ya Mabenki yameanza kuonyesha nia ya kutoa mikopo kwa sekta ya kilimo kama alivyoeleza Waziri wa Fedha katika hotuba yake ya mwaka 2004/2005. Serikali inakusudia kuanzisha Benki ya Kilimo ambayo itakuwa na uwezo mkubwa wa kutoa mikopo ikilinganishwa na asasi zilizopo sasa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Pia nasikitika kwa majibu ya Waziri, mimi sijamwuliza hivyo, nimeuliza juu ya Dira ya Taifa ya Kuondoa Umaskini, sijammuliza Ilani wala majibu yake aliyojibu wala hajajibu chochote. *(Makofi/Kicheko)*

Mimi nauliza hivi lengo la hiyo Dira kuna *timeframe* ya kuondokana na hili jembe la mkono kama vile ambavyo tuna *timeframe* ya kuondokana na madarasa, ujinga na kadhalika, je, kwenye hiyo Dira iko *timeframe* ya kuondokana na jembe la mkono? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa huwezi kurukia kwenye matrekta na una wafugaji wengi wenye mifugo, kuna mkakati gani wa kuwapa majembe ya kukokotwa na ng'ombe watu wa sehemu zenye mifugo? Ndio swali langu hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa majibu kwa ufupi kama ifuatavyo: Dira ipo, ni ya 2025, ndio Dira tuliyonayo, huo ni ufupi wake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matrekta na majembe aliyouliza yapo na hapo ninayo baadhi ya orodha naweza kuitaja.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA:** Kwa ufupi, kwa mfano, kwa Tabora...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hiyo orodha naomba mtatuwekea tu kwenye Meza baadaye.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA:** Ahsante. *(Kicheko)*

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa Wilaya kuu ya Nzega ikiwa ni pamoja na Igunga tulianza kutumia wanyamakazi kwa kufundishwa katika Kituo cha Mwanala tangu mwaka 1939. Tokea hapo wakulima wameachwa bila kuendelezwa, yaani wanatumia hawa ng'ombe wa kulima kwa kulima tu hawajawezeshwa kuwatumia kupalilia au kupanda. Sasa katika mpango wao badala ya kuwahamisha pale anasema wanaanza tena kufundisha, wataanza lini kuwaondoa pale kwenye kulima watumie ng'ombe hawa kwa kupalilia na kupanda? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli hizi zinaenda sambamba na mkakati wote wa *mechanization* nchini. Kwa taarifa, Nzega sio tu tuna matrekta lakini tuna plau za maksai 20,583, hii inaendelea. Kwa taarifa zaidi mikakati na msisitizo unategemea sana *District Council* wanapokaa kujadili kwa undani utekelezaji wa miradi hiyo na ndipo hapo tunaweza kutoa. Ni vigumu kutoka Dar es Salaam kuagiza matrekta milioni kadhaa yafanye hapa na pale wakati wako mbali. Tunaomba Halmashauri ya Wilaya hiyo ya Nzega tushirikiane katika kutekeleza azma hii. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona maswali yamekwisha. Nitangaze tu kikao cha leo cha Kamati ya Maliasili na Mazingira, Wajumbe wakutane Chumba Na.428, ghorofa ya nne, saa tano asubuhi.

Baada ya hapo, nafikiri Mheshimiwa Spika yupo tayari kunipokea, karibu. *(Kicheko/Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005
### Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, inayohusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako

Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, aidha, niruhusu niungane na Waheshimiwa Wabunge, ndugu na marafiki katika kuwafariji na kuwapa salamu za rambirambi, familia, ndugu na wapiga kura wa Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini. Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *Amina.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wote, waliopatwa na misiba, misukosuko au mikasa ya aina yoyote ile katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kuwapongeza Wabunge wapya, Mheshimiwa Danhi Makanga Mbunge wa Bariadi Mashariki, kwa kuchaguliwa kwake na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kwake kujiunga na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Maswa, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliopata nafasi ya kuchaguliwa kutuwakilisha katika nyadhifa mbalimbali Kimataifa. Tunawapongeza Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, kwa kuchaguliwa kwao na Bunge lako Tukufu kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika. Tumejawa na furaha na faraja maridhawa kwa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kuchaguliwa kwa kauli moja kuwa Rais wa kwanza wa Bunge hilo la Afrika. Imani hii ya Wabunge wa Bunge la Afrika kwa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella ni ishara tosha ya imani ya Bara la Afrika katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, anayeshughulikia Mazingira, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuteuliwa kwake na Bunge lako Tukufu, kutuwakilisha katika Baraza la Wabunge wa Nchi za *SADC. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wale wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yetu kwa kipindi kilichopita na ambao wametuwezesha kupanga mipango ya mwaka 2004/2005 na kuboresha hoja zetu ambazo tunaziwasilisha katika hotuba hii. Aidha, natoa shukrani kwa Wananchi wote wa Tanzania. Pia natoa shukrani zangu kwa Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Katibu Mkuu wangu, Bibi Ruth H. Mollel, Watumishi wa Wizara yangu, pamoja na taasisi na mashirika mbalimbali ya ndani na nje, kwa misaada na ushauri wao,

bila kumsahau Mheshimiwa Benedicto Mutarchoka Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara yangu, kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuiboresha hoja hii. Aidha, shukrani zangu ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Huduma za Jamii, chini ya Mwenyekiti wao Mheshimiwa Omar Kwaang'w, Mbunge wa Babati Mashariki, kwa uchambuzi na ushauri wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu ulifanyika kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kuondoa Umaskini, Sera ya Elimu ya Juu, Sera ya Ufundi na Mafunzo na Sera ya Sayansi na Teknolojia. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hatua za utekelezaji wa mambo yaliyoainishwa katika Mpango Kabambe wa Wizara zimeshaanza. Baadhi ya malengo yaliyoanza kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- Wizara imeanzisha Mamlaka ya Elimu Tanzania *(Tanzania Education Authority),* kwa lengo la kusimamia mfuko wa elimu utakaowezesha kuinua ubora wa elimu, kuongeza udahili wa wanafunzi na upatikanaji wa elimu hiyo kwa usawa. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Mamlaka imetoa jumla ya Sh. 6,716,429,884/= kwa ajili ya maendeleo ya Vyuo na shule.

- Wizara iliwasilisha Muswada wa Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu na ufundi, ambao ulipitishwa katika Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2004. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Muswada huu umesainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- Wizara imekamilisha Mpango/Mkakati wenye lengo la kuboresha utendaji wa majukumu ya Wizara pamoja na upimaji wa utendaji wa watumishi wa Wizara kwa mfumo wa uwazi *(Open Performance Review Appraisal System - OPRAS).*

- Idadi ya wanafunzi katika Vyuo Vikuu vya Umma imeongezeka kutoka wanafunzi 21,407 mwaka 2002/2003 hadi kufikia wanafunzi 28,910 kwa mwaka 2003/2004. Aidha, kwa Vyuo Vikuu Binafsi, idadi imeongezeka kutoka wanafunzi 2,040 kwa mwaka 2002/2003 hadi kufikia wanafunzi 2,764 kwa mwaka 2003/2004.

- Idadi ya wanafunzi wa kike katika Vyuo Vikuu vya Umma imeongezeka kutoka 7,536 kwa mwaka 2002/2003 hadi kufikia 8,344 kwa mwaka 2003/2004, likiwa ni ongezeko la wanafunzi 808, ambalo ni ongezeko la asilimia 11.

- Kwa upande wa Vyuo vya Ufundi, idadi ya wanafunzi ni 2,103 kwa mwaka 2003/2004, ambapo idadi ya Wanafunzi wa kike imeongezeka kutoka 202 kwa mwaka 2002/2003 hadi kufikia 245 kwa mwaka 2003/2004, ambalo ni ongezeko la asilimia 21.

- Aidha, kwa lengo la kupanua uwezo wa kutoa huduma za afya, Wizara imetoa udhamini kwa wanafunzi madaktari 128 wa mwaka wa kwanza wanaosoma kwenye Vyuo Vikuu Binafsi na Vyuo Vikuu vya Umma wenye udhamini binafsi. Uamuzi huo

wa Serikali una madhumuni ya kupiga hatua kuelekea lengo la uwiano wa Daktari mmoja kwa Wananchi 10,000, uliowekwa na Shirika la Afya Duniani kutoka uwiano wa 1:25,000 uliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara yangu imekamilisha zoezi la kuainisha gharama halisi za kumwelimisha mwanafunzi wa Elimu ya Juu na ufundi. Mpango huu unalenga kupunguza gharama za uendeshaji katika taasisi zetu, kupanua udahili na kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara yangu imekamilisha ripoti ya utafiti wa sekta ya elimu baada ya ngazi ya elimu ya msingi *(Post Primary Education),* ikiwa ni maandalizi ya mradi wa uhuishaji Vyuo vya Elimu ya Juu na Ufundi. Ripoti hiyo ya utafiti imeweka bayana mikakati ya matumizi ya Vyuo vya Umma vilivyo chini ya Wizara mbalimbali na mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:-

- Kuboresha mitaala kwa kuandaa na kuanzisha kozi zinazolenga katika ushindani wa soko la ajira, pamoja na mbinu za kufundishia kwa kutumia teknolojia ya *video conference system.* Kozi mpya ni *B.Sc. Wildlife Science and Conservation, B.Sc. Molecular Biology and Biotechnology, B.Sc. in Aquaculture, B.Sc. Biotechnology and Laboratory Sciences, B.Sc. Nursing Midwifery* na *B.Sc. Nursing Management.*

- Kuwasilisha na kupitishwa kwa Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu na ufundi nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitekeleza yafuatayo: Kukarabati majengo ili yaweze kuendana na ongezeko la idadi ya wanafunzi, kuboresha miundombinu ili iweze kwenda sambamba na ongezeko la mahitaji, kutumia teknolojia ya *Video Conference System* katika ufundishaji ili kurahisisha na kuleta ufanisi katika ufundishaji, kudahili wanafunzi 10,866, kati yao wanawake wakiwa ni 3,501 ambao ni asilimia 32.2 ya jumla ya wanafunzi wote, kukamilisha taarifa ya awali ya kuanzisha Chuo cha Madini Nzega na kukamilisha na kusaini Mkataba wa Uanzishwaji wa *Mlimani City.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo kimetekeleza yafuatayo: Kuboresha mitaala sita kwa kubuni kozi mpya za Shahada ya kwanza, kuongeza udahili wa wanafunzi wa masomo ya Shahada ya Uzamili kutoka wanafunzi 10 mwaka 2002/2003 hadi kufikia wanafunzi 29 mwaka 2003/2004. Aidha, Chuo kimedahili wanafunzi wawili wa Shahada ya Falsafa, kuanza kutumika kwa mitaala ya Stashahada ya Uzamili *(Postgraduate Diploma)* katika nyanja za Ardhi na Uhandisi Mazingira, Chuo kimesomesha walimu 34 ambao wamefuzu Shahada ya Falsafa na wengine 32 wako katika hatua tofauti katika Shahada hiyo na kukamilisha mchanganuo kwa ajili ya uimarishaji wa maabara ya Idara ya Uhandisi Mazingira na ukarabati wa Jengo la Utawala kwa ajili ya kutoa huduma za maktaba.

Chuo kimepata fedha kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania jumla ya Shilingi 563,033,600/= kwa ajili ya shughuli hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mzigo mkubwa unaobebwa na Serikali katika kugharamia elimu ya juu nchini, Chuo kimetekeleza azma ya kuzalisha asilimia 15 ya fedha za ziada za matumizi mengine kwa njia ya kutoa ushauri wa kitaalam. Njia hii imekisaidia Chuo kujenga ofisi za walimu 34 na madarasa 10 na Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Chuo Kikuu kishiriki cha Sayansi za Afya-Muhimbili kimetekeleza yafuatayo: Kuimarisha mfumo wa mawasiliano wa mtandao katika majengo yote ya chuo *(Local Area Network),* kimeongeza idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Shahada ya kwanza kutoka 337 kufikia 359, kuanzishwa kwa Shahada mpya mbili ambazo ni *BSc. Nursing Mid-wifery* na *BSc. Nursing Management.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimetekeleza yafuatayo: Kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 13,357 mwaka 2003 hadi kufikia wanafunzi 16,316 mwaka 2004. Asilimia 25 ya wanafunzi hao ni wanawake, kuimarisha utoaji huduma kwa kufunga kompyuta katika vituo 14 na kompyuta 17 zimefungwa Makao Makuu. Huu ni msaada kutoka Shirika la *UNESCO,* kutoa mafunzo ya teknolojia na mawasiliano kwa watumishi wa chuo ili kuongeza ufanisi katika kazi na kimezindua kituo cha Chuo Kikuu Huria Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimetekeleza yafuatayo:-

- Kuendeleza miradi inayojumuisha utafiti na mafunzo ya mbinu bora za kilimo. Miradi inaendeshwa katika Mikoa na Wilaya zifuatazo: -

- Kilimo cha Bustani na uzalishaji wa mboga na matunda - Mkoa wa Morogoro. Zaidi ya wakulima 2550 wamefaidika na maradi huo.

- Kilimo cha mseto kinachohusu upandaji miti bora kwa matumizi ya malisho, kuni na kurutubisha ardhi - Gairo, Wilaya ya Kilosa. Zaidi ya wakulima 200 wamefaidika.

- Mradi wa Uhakika wa Chakula - Mikoa minane katika Kanda ya Mashariki na Kanda ya Nyanda za juu Kusini. Zaidi ya wakulima na wafugaji 2000 wamefaidika.

- Mradi wa mbuzi wa kienyeji kwa ajili ya nyama na maziwa - Gairo, Mgeta, Iringa na Mbeya. Zaidi ya wakulima 300 wamefaidika.

- Mradi wa kufichua mabomu kwa kutumia panya buku. Mafanikio yameanza kuonekana baada ya kufanyiwa majaribio nchini Msumbiji na sasa hivi Chuo kimepata maombi kutoka Angola.

- Mradi wa Vanilla, zao linaloendelea kupata umuhimu Mkoa wa Kagera.

- Kuandaa na kuendesha kozi fupi, warsha, mikutano, semina na kutoa huduma za ushauri wa kilimo, utunzaji na usimamizi wa mali ya asili, misitu na ufugaji. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004 washiriki wapatao 1,000 wamefaidika.

- Kukarabati majengo tisa na kuweka mitambo miwili ya simu pamoja na kuimarisha mtandao wa mawasiliano *(Local Area Network - LAN).*

- Kukamilika kwa uanzishwaji wa Shahada mpya tatu za kwanza ambazo ni Shahada ya *BSc. Acquaculture,* Shahada ya *BSc. Biotechnology and Laboratory Sciences,* Shahada hizi zitaanza mwaka wa masomo 2004/2005 na Shahada ya *Rural Development,* itaanza mwaka wa masomo wa 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Chuo Kikuu Mzumbe kimetekeleza yafuatayo:-

- Kimeanza kufundisha masomo ya Shahada ya Uzamili katika uongozi *(MBA)* na Shahada za kwanza kwa mtindo wa mafunzo ya jioni *(Parallel Programs)* katika Jengo la Chuo lililoko Dar es Salaam.

- Kimekamilisha matayarisho ya uanzishwaji wa programu za Shahada ya Udaktari wa Falsafa. Aidha, Chuo kimeshaanzisha programu mpya tatu ambazo ni *Bsc. Information Technology, Bsc. Applied Statistics* na *Certificate in Information Technology.*

- Kimeendeleza ushirikiano na Vyuo Vikuu vingine vya ndani na nje ya nchi.

- Kimekamilisha ukarabati wa jengo lililokuwa likitumika kama Chekechea ambalo kwa sasa ni Bweni la wanachuo 140.

- Kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004, chuo kimedahili Wanafunzi 550, kati ya hao 250 ni kwa udhamini wa Serikali na 300 kwa udhamini binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu limetekeleza yafuatayo: Kushauri, kuratibu na kuhakikisha ubora wa Vyuo vya elimu ya juu vinavyoanzishwa, limetoa ushauri kwa serikali na kutoa mwongozo kwa vyombo vinavyomiliki Vyuo kuhusu uendelezaji, upanuzi, uboreshaji na uwekezaji katika elimu ya juu, limetoa machapisho na kuelimisha umma kuhusu majukumu ya Baraza na taratibu za Elimu ya juu kwa ujumla, limeendesha semina mbili kwa wafanyakazi wa Baraza kuhusu kinga dhidi ya Ukimwi na katika vita dhidi ya rushwa na pia limefanya tathmini na kutoa ulinganisho wa vyeti vilivyotolewa kwa Watanzania na Vyuo mbalimbali nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Mamlaka ya Elimu Tanzania ilitekeleza yafuatayo:-

- Iliwekeana Mkataba wa maelewano *(MoU)* na Mfuko wa Elimu ya Juu Zanzibar, kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa Mfuko wa elimu kwa upande wa Zanzibar.

- Iliandaa ripoti ya awali ya uchambuzi yakinifu wa hali ya Elimu nchini na kuainisha kipaumbele katika sekta ya elimu.

- Ilikamilisha taratibu za ajira ya watumishi watakaohudumia Mamlaka. Watumishi 18 wamekwishaajiriwa.

- Ilikamilisha taratibu, miongozo na vigezo vya ugawaji fedha kutoka katika Mfuko wa Elimu kwa ajili ya ngazi zote za elimu.

- Imefanya ziara za uhamasishaji na kutoa elimu kwa wadau na wananchi juu ya Mamlaka na Mfuko wa Elimu katika mikoa 18 ya Tanzania Bara.

- Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania imewasilisha Wizara ya Fedha, Mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato kwa kutambua msamaha wa kodi kwa wachangiaji kulingana na Sheria ya Mfuko wa Elimu.

- Imeanzisha mashirikiano na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Elimu na Utamaduni na Mifuko mbalimbali ya Elimu katika ngazi za Mikoa na Wilaya.

- Imewezesha Serikali kuanza utekelezaji wa udhamini wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Shahada ya kwanza ya Udaktari katika Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ufundi, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara imefanya yafuatayo:-

- Imekarabati majengo, mitambo na vifaa mbalimbali katika Vyuo vya Ufundi Arusha na Mbeya kwa gharama ya shillingi millioni 73. Aidha, imenunua vifaa vya kufundishia Vyuoni vyenye thamani ya shilingi millioni 47.

- Imegharimia mafunzo ya Uzamili kwa walimu 20 kwa ngazi za Udaktari wa Falsafa *(Ph.D.)* watatu, Shahada ya Uzamili *(MSc.)* saba na *Diploma* ya Uzamili *(PGD)* saba na Stashahada ya Juu ya Uhandisi *(ADE)* waatu.

- Imehamasisha wasichana kujiunga na mafunzo ya elimu ya ufundi kwa kutoa kozi maalumu za wiki kumi zilizolenga kuinua uwezo wao kitaaluma na ambazo ziliendeshwa katika Vyuo vya ufundi Mbeya na Arusha. Kupitia kozi hii Wasichana 19 walichaguliwa kujiunga na mafunzo ya ufundi sanifu katika Vyuo vya ufundi ikiwa ni asilimia 47 zaidi ya idadi ya mwaka 2002/2003, ambayo ilikuwa ni wasichana 10.

- Imenunua mashine na mitambo yenye thamani ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya Chuo cha Ufundi Mbeya ili kuimarisha ufundishaji wa Stashahada ya juu ya Uhandisi. *(Makofi)*

- Imenunua vitabu vya kiada na rejea vyenye thamani ya shilingi milioni 85 katika fani za mitambo, umeme, magari, usanifu, majengo, ujenzi na masomo ya jumla kwa Vyuo vya ufundi Arusha na Mbeya.

- Imeandaa mpango wa utekelezaji *(Action Plan)* wa kupanua Chuo cha Ufundi Mbeya ili kiwe Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, ifikapo mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imetekeleza yafuatayo:-

- Imetayarisha mitaala mipya katika ngazi ya Shahada ya Uhandisi *(B.Eng)* katika fani za Uhandisi Mitambo, Uhandisi Umeme, Uhandisi Mawasiliano, Anga na Kompyuta.

- Imenunua kompyuta 100 kwa msaada kutoka Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo *(SIDA)* chini ya mradi wa *IT Fundis.*

- Imeanzisha kozi mpya ya kompyuta ya *IT Pre-Technician course* chini ya mradi wa *IT Fundis,* kozi hii itakuwa inachukuwa wanafunzi 60 kila mwaka.

- Imegharamia mafunzo ya uzamili kwa walimu 35 ndani na nje ya nchi katika ngazi mbalimbali: Udaktari wa Falsafa 17, Shahada ya Uzamili 12 na Diploma ya Uzamili sita. Aidha, walimu watano wanapata mafunzo ya Shahada ya kwanza na mmoja *Diploma.*

- Imejenga na kuunganisha mtandao wa mawasiliano ya habari *(Internet)* katika maabara za kompyuta, ofisi na mabweni ya wanafunzi.

- Imeendesha warsha tatu kwa wanafunzi, uongozi na wafanyakazi kuhusu uzuiaji wa kuenea kwa UKIMWI.

- Imedahili Wanafunzi 119 wa kiwango cha Stashahada ya juu *(ADE).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi limetekeleza yafuatayo:-

- Limesajili Vyuo 34 na kati ya hivyo, 21 vimepewa hati ya usajili kamili *(Full Registration)* na 11 vimepewa usajili wa muda *(Provisional Registration).* Aidha, Vyuo viwili vimepewa hati ya usajili wa awali *(Preparatory Registration).*

- Limekagua na kutoa Ithibati ya muda *(Provisional Accreditation)* kwa Vyuo ishirini. Aidha, Baraza linaendelea kutoa ushauri kwa Vyuo hivyo ili viweze kupata Ithibati kamili *(Full Accreditation).*

- Limeendelea kuratibu mitihani ya kitaifa ya *Full Technician Course (FTC)* na *Advanced Diploma in Engineering (ADE)* kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani la Taifa *(NECTA)*.

- Limeanza kutayarisha mitaala ya programu 11 za mafunzo katika fani za uhandisi na sayansi nyinginezo *(engineering and other sciences)*. Aidha, Baraza limefanya utafiti wa soko la ajira *(Labour Market Demand Survey),* ambao umeliwezesha kufahamu mahitaji halisi ya ujuzi unaotakiwa na soko la ajira kwa wanafunzi wanaohitimu katika Vyuo vya Ufundi nchini. Baraza linatarajia kukamilisha mitaala hiyo mwishoni mwa mwaka 2004.

- Limeidhinisha mitaala ya mafunzo ya kompyuta yatolewayo na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam katika ngazi ya cheti *(IT Pre-Technician Certificate)*.

- Limeweka mfumo wa uwekaji kumbukumbu *(Database)* za Vyuo vya Ufundi nchini.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Sayansi na Teknolojia, katika kipindi cha mwaka wa Fedha cha 2003/2004, Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:-

- Iliandaa mkataba unaolenga kukuza na kusimamia matumizi salama na ya amani ya Nishati ya Nyuklia kwa maendeleo ya Taifa. Mkataba huo unahusu:-

- Azma ya Kutokomeza au Kutoendeleza Utengenezaji na Matumizi ya Silaha za Nyuklia *(Non- Proliferation of Nuclear Weapons Treaty - NPT)*.

- Kutumia Nishati ya Nyuklia kwa shughuli za amani tu na siyo katika utengenezaji wa Silaha za Nyuklia *(Safeguards Agreements)*.

- Itifaki ya Kimataifa *(Additional Protocol to Safeguards Agreement)*.

- Misaada ya Kushughulikia Ajali ya Nyuklia au Dharura ya Ki- Radiolojia *(Convention on Assistance in the Case of a Nuclear Accident or Radiological Emergency)*.

- Azma ya Kutoa Taarifa ya ajali ya Nyuklia Mapema *(Early Notification of Nuclear Accidents)*.

- Aidha, Bunge liliridhia mikataba inayohusu Tanzania kuruhusu ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha kupima na kufuatilia Viwango vya Mionzi Ayonisha katika Mazingira chini ya Tume ya Kimatifa ya Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia na Tanzania na Kuzuia Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test - Ban Treaty)*.

- Ilikamilisha Taarifa ya Maelewano *(Memorandum of Understanding - MoU)* ya ushirikiano kati ya Tanzania na Uswiss katika uendelezaji wa ujuzi na mafunzo katika

maeneo ya utafiti wa kisayansi na kiteknolojia pamoja na uboreshwaji wa miundo mbinu ya asasi taasisi za utafiti na maendeleo.

- Iliwasilisha kwa Sekratariat ya Baraza la Mawaziri rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu Utungaji wa Sera ya Taifa ya Biotekinolojia.

- Iliandaa na kurusha hewani vipindi 52 kupitia Redio Tanzania Dar es Salaam juu ya umuhimu wa utumiaji wa sayansi na teknolojia katika maisha ya wananchi ya kila siku.

- Ilizitembelea Halmashauri za Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Mtwara, Arusha, Mbeya na Mwanza kupata maoni na kuzihamasisha kuhusu umuhimu wa kuunda Kamati za Sayansi na Teknolojia nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kutoa Tuzo ya Wizara kwa wasichana kumi na tisa (kidato cha sita wasichana wanane na wasichana kumi na moja wa kidato cha nne), waliofanya vizuri na kuongoza kwa upande wa wasichana katika masomo ya sayansi ya msingi (hisabati, kemia fizikia na baolojia) katika mwaka wa 2003.

- Wizara yangu Iliwezesha mkutano wa wadau uliojadili kuanzishwa kwa *The Tanzania Association of Academy of Sciences (TAAS).*

- Wizara yangu iliwasilisha Tume ya Taifa ya *UNESCO,* mradi wa *Popularization of Science and Technology in Tanzania,* kwa lengo la kusambaza matokeo ya utafiti kwa mwananchi ili kuongeza ufahamu juu ya mabadiliko yanayotokana na maendeleo ya sayansi na tekinolojia ulimwenguni kote.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ilitekeleza yafuatayo:-

- Iliweza kubuni jiko sanifu kwa ajili ya kupunguza upoteaji wa joto katika matumizi ya *Briquettes,* hasa kwa matumizi ya mkaa wa kawaida kwa kushirikiana na wadau wengine.

- Imeshiriki katika ukarabati wa mtambo wa mashine ya upepo ya mradi wa upepo wa maji katika kijiji cha Mgunga, Wilaya ya Dodoma.

- Imefadhili miradi 10 ya utafiti (katika maeneo ya afya ya jamii na tiba, kilimo na mifugo, maliasili, viwanda na nishati pamoja na sayansi ya awali) kwa jumla ya shillingi 49,350,000.00. Pia Wanasayansi na watafiti 16 kwa jumla ya shillingi 22,848,000.00 kutoka taasisi na asasi za utafiti na maendeleo katika mikutano mbali mbali nje na ndani ya nchi kwa lengo la kusambaza matokeo ya tafiti walizofanya.

- Imetayarisha kumbukumbu *(database)* ya teknolojia kutoka asasi mbali mbali nchini na kuzisambaza kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya zote nchini.

- Iliandaa na kuendesha kongamano la wadau juu ya uanzishwaji wa Masjala ya Taifa ya Utafiti *(National Research Registry).*

- Iliandaa Kongamano la Kimataifa la 13 la mazao ya jamii ya mizizi *(13$^{th}$ Symposium of International Society for Tropical Roots Crops - ISTRC),* lililofanyika Arusha mwezi Novemba, 2003. Dhana kuu ilikuwa namna ya kupunguza umasikini na kuhakikisha maisha endelevu kwa kutumia mazao hayo.

- Imeratibu uanzishwaji wa kituo dada *(Sister Institution)* cha *International Centre for Genetic Engineering and Biotechnology (ICGEB)* na kuziwezesha taasisi sita zinazojihusisha na masuala ya baotekinolojia hapa nchini kujiunga na kituo hicho.

- Walielimishwa juu ya taratibu na kanuni za uingizaji na usafirishaji wa vyakula vitokanavyo na mabadiliko ya Jeni *(Genetically Modified Foods - GMO),* kwa waingizaji na wasafirishaji wa vyakula *(importers and Transporters).*

- Iliweza kuwasiliana na Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya zote kwa lengo la kupata majina ya watu mbalimbali wanaojishughulisha na ugunduzi na uvumbuzi nchini ili kufanyia tathmini kazi zao na itakapobidi ziweze kuendelezwa kwa manufaa ya Taifa.

- Imeongeza thamani ya Tuzo kiwango cha juu kutoka shillingi 1,000,000.00 hadi shillingi 5,000,000.00 kwa lengo la kuwahamasisha wagunduzi, wavumbuzi watafiti na wanasayansi nchini.

- Kwa kushirikiana na asasi na taasisi mbali mbali Tume imehawilisha teknolojia katika sehemu mbali mbali nchini. Teknolojia hizo ni pamoja na kukiwezeshha kikundi cha *Jiboreshe Youth Group* cha Arumeru, mkoani Arusha na wanakijiji wa Mkuranga kufundishwa namna ya kulima uyoga. Teknolojia ya ujenzi wa nyumba ya mfano kwa kutumia mianzi, nyumba inayohimili matetemeko ya ardhi, Wilayani Rungwe na kuboresha teknolojia za mawasiliano na habari kwa kuendelea na upanuzi wa mtandao wa mawasiliano kwa njia ya kompyuta kati ya taasisi, asasi na mtandao wa watafiti kwa kuongeza *internet bandwith* kutoka 256 *kbps* hadi 512 *kbps,* kusaidia utayarishaji na ukarabati wa tovuti za Manispaa ya Kinondoni, Zanzibar na Chuo cha Ustawi wa Jamii, Kituo cha Habari na Mawasiliano Sengerema na Kijiji cha Lunga Lugoba, kutengeneza mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu za kanda katika maktaba ya Televisheni ya Taifa (TVT), kutoa mafunzo ya kompyuta kwa watu 30 wakiwemo wafanyakazi 17 wa Manispaa ya Kinondoni na mwanakijiji mmoja wa kijiji cha Lugoba, Wilaya ya Bagamoyo na kuanzisha kituo cha Redio Sengerema yenye usikivu wa nusu kipenyo kati ya kilomita 35 na 50.

- Imeshiriki katika kupanga mikakati ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Teknohama).

- Ilisambaza na kutoa mafunzo ya programu ya *Computerized Documentation System/Integrated Set of Information Systems (CDS/ISIS), (Bibliographical database)* kwa taasisi sita.

- Iliendesha semina nane za uhamasishaji juu ya haki miliki *(Intellectual Property Rights)* kwa wanasayansi, wana-teknolojia na wahandisi 160 kutoka taasisi na asasi nane.

- Imeanza kutoa habari za kisayansi na kiteknolojia kupitia tovuti ya Kimataifa ijulikanayo kama *www.wsciDev.Net.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004, Tume ya Taifa ya Mionzi ilitekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha mabadiliko ya Sheria ya Kinga ya Mionzi *(The Protection from Radiation Act, 1983)* kwa kutungwa Sheria mpya *(The Atomic Energy Act, 2003).*

- Kukamilisha ujenzi wa hifadhi ya Mabaki ya Vyanzo vya Mionzi *(CRWMF)* huko Arusha.

- Kupima mionzi katika vyakula viingiavyo nchini ambapo sampuli 2,700 zilipimwa na wafanyakazi 1000 Katika vituo vya mionzi walipewa huduma ya upimaji mionzi *(Personal Radiation Monitoring).*

- Kukagua na kusimamia ubora na usalama wa vituo 125 vya mionzi vitoavyo huduma za *X-ray.* Matokeo ya ukaguzi huo ni pamoja na vituo 95 vilionekana kukidhi viwango vinavyokubalika Kimataifa, vituo 27 vilikuwa na matatizo ya ubora wa mashine au vyumba vya kutolea huduma hiyo, vituo vitatu vilifungiwa kutoa huduma kutokana na hali mbaya ya usalama hadi vikamilishe marekebisho.

- Kukagua Migodi minne ya Geita, Kahama, Nzega na Kiwira, kati ya migodi sita kwa lengo la kubaini kuwepo kwa hewa aina ya *radon,* iletayo madhara na kujua kiwango kilichopo ili kulinda usalama wa watumiaji wa migodi hiyo.

- Ilikagua minara 62 ya simu za mikononi za kampuni za simu za *Vodacom, Mobitel* na *Celtel* na *radio transmission station* moja iliyoko kilomita 40 kutoka Dar es Salaam karibu na Shule ya Msingi ya Salasala. Matokeo ya ukaguzi huo ni kwamba minara ilikuwa na wastani wa *Power Density 0.005mW/cm2* mara mia moja ya vile vilivyoko katika nchi ya Marekani lakini ni chini ya kiwango kilichowekwa na Shirika la Kimataifa lijulikanalo kama *International Commission for Non-Ionizing Radiation Protection (ICNIP 1998)*. Aidha, kituo cha redio kilikuwa na viwango kati ya *Field Electrical Strength 106.4 - 156.0 V/m* zaidi ya kile kichowekwa na Shirika la Kimatifa la *ICNIP.*

- Kukarabati mashine 30 za *X-ray* katika hospitali mbalimbali nchini na vifaa vingine 35 katika tekinolojia ya nyuklia.

- Kuratibu misaada ya zaidi ya *USD* 800,000 kwa Taasisi nane za kitaifa kupitia miradi ya Kitaifa na Kikanda (Afrika) inayogharimiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(IAEA).*

Mheshimiwa Spika katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Tume ya Taifa ya *UNESCO* imetekeleza yafuatayo:-

- Ilishirikisha Taifa katika maandalizi ya Programu na Bajeti ya *UNESCO* kwa kipindi cha 2004/2005.

- Ilishirikisha Taifa katika kikao cha 32 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* kilichofanyika tarehe 29, Septemba hadi tarehe 17 Oktoba, 2003 na hatimaye kutekeleza maamuzi ya mkutano huo Wizara yangu iliongoza Ujumbe wa Taifa. Maamuzi hayo ni pamoja na kuteua Wajumbe kwenye Kamati za *UNESCO* ambazo Tanzania ni Mjumbe. Kamati hizo ni Kamati ya Utawala *(Administrative Committee),* Kamati ya *Management of Social Transformation - MoST,* Kamati ya *Man and Biosphere Programme (MAB)* na Kamati ya *International Programme for the Development of Communication (IPDC).*

- Iliratibu utekelezaji wa Miradi iliyofadhiliwa na *UNESCO* katika kipindi cha 2002/2003: Miradi hiyo ni Mradi wa vifaa kwa ajili ya Vituo vya Kanda vya Chuo Kikuu Huria Tanzania, Vifaa kwa ajili ya Kituo cha Redio Zanzibar kilichoko Pemba, Mradi wa kuandaa Sera ya Vijana, Zanzibar, Mradi wa kuendeleza wahunzi wadogo wadogo, Mradi wa vifaa Kwa Kituo cha Walimu Same, Mradi wa ununuzi wa vifaa na vitabu wa Shule ya Sekondari Soni, Mradi wa kuendeleza Hifadhi ya Utamaduni wa Dunia ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara, mafunzo ya muda mrefu na mfupi yaliyofadhiliwa na *UNESCO* kwa kushirikiana na nchi Wanachama za Uholanzi, Poland, Jamhuri ya watu wa China na Jamhuri ya Korea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Utawala na Utumishi, Wizara yangu imetekeleza yafuatayo: Kudhamini watumishi 32 kwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi, kuwapandisha vyeo watumishi 62 wa kada mbalimbali ambao wametimiza masharti ya ajira zao, sawa na asilimia 93 ya lengo lililokusudiwa. kuendesha semina tatu kwa watumishi 447 kuhusu athari za ugonjwa hatari wa UKIMWI, kutoa elimu kuhusu masuala ya jinsia na kudhibiti rushwa katika sehemu ya kazi na kuwaelimisha watumishi 447 wa Wizara, Makao Makuu na Vyuo vya Ufundi vya Mbeya na Arusha kuhusu mpango wa maboresho ya Utumishi wa Umma *(PSRP).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, kwa Elimu ya Juu, Wizara yangu inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuunda Bodi ya kuratibu mikopo ya wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu na ufundi nchini na nje ya nchi.

- Kupata ofisi kwa ajili ya watumishi wa Bodi ya mikopo ya wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu na ufundi.

- Kutoa mwongozo kuhusu mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo vya elimu ya juu na ufundi nchini na nje ya nchi kupitia Bodi ya mikopo ya wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu na ufundi.

- Kuboresha mitaala na mbinu za kufundishia kwa lengo la kuboresha elimu ya juu.

- Kushirikisha wadau katika kutathmini utekelezaji wa mpango wa ugharimiaji endelevu wa elimu ya juu.

- Kuwasiliana na wadau ili kuelimisha juu ya upatikanaji na ugharimiaji wa elimu ya juu ndani na nje ya nchi.

- Kuwashirikisha wadau katika zoezi la kutathmini sera ya Elimu ya Juu na kutoa mapendekezo ya kuboresha/kurekebisha.

- Kuendeleza ushirikiano wa kielimu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Madola, Ushirika wa Maendeleo kusini mwa Afrika, na nchi mbalimbali ambazo zina ushirikiano wa kielimu na Tanzania.

- Kuendelea kudhamini wanafunzi wa Shahada ya kwanza ya Udaktari katika Vyuo Vikuu binafsi. Kwa mwaka huu wa masomo 2004/2005, Wizara itadhamini Wanafunzi 256 (128 wa mwaka wa kwanza na 128 wa mwaka wa pili) katika Vyuo Vikuu vya binafsi pamoja na Wanafunzi walio katika udhamini binafsi katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya cha Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatarajia kutekeleza yafuatayo: Kuendesha mifuko ya kugharimia utafiti na kudhamini wanafunzi, kuiendeleza sehemu iliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya Taasisi ya Sayansi za Bahari na kuifanyia marekebisho maktaba ya Chuo ili iweze kutumiwa na wanafunzi kwa saa 24.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2004/2005, Chuo Kikuu cha Ardhi na Usanifu Majengo kinatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuratibu utekelezaji wa sera na programu za chuo katika kuboresha ufanisi.

- Kuunda mitaala ya masomo ya Shahada nyingine za kwanza na kusimamia kazi ya kurekebisha mitaala ili zile kozi za msingi zinazofanana, zifundishwe kwa pamoja katika idara mbalimbali.

- Kuendelea kutathmini mitaala na ufundishaji ili kufanya mabadiliko pale panapostahili.

- Kuimarisha, kutangaza na kusimamia masuala ya kukuza uhusiano kati ya chuo na taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa.

- Kuendelea kuhamasisha na kuwaendeleza wanataaluma kufikia Shahada ya udaktari wa falsafa ili kuongeza ubora wa viwango vya kitaaluma.

- Kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi za walimu na madarasa na kukarabati barabara za ndani na maegesho ya magari.

- Kkurabati jengo la utawala ili liwe Maktaba.

- Kuhamisha barabara inayopita karibu na tenki la maji.

- Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa tanki la maji kwa lengo la kuzuia mmomonyoko wa udongo kuzunguka tanki, na kununua mashine za kusukuma maji.

- Chuo kitadahili jumla ya Wanafunzi 350. Kati ya hao, 250 kwa udhamini wa Serikali na 100 kwa udhamini binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuimarisha mafunzo ya Shahada za kwanza na za juu kwa kuzingatia sera na mbinu mbalimbali ambazo chuo kimejiwekea.

- Kutoa kipaumbele kwa miradi inayojumuisha utafiti na mafunzo ya mbinu bora za kilimo kwa wakulima.

- Kuendesha warsha/Kongamano za Kisayansi kwa kuwashirikisha wadau kutoka nje ya nchi ili kubadilishana utaalamu.

- Kutoa huduma za ushauri wa kilimo, utunzaji na usimamizi wa mali ya asili, misitu na ufugaji kwa wakulima na wafanyakazi. Kukarabati majengo na mtandao wa mabomba ya maji chuoni.

- Kujenga maabara ya Zoolojia na kituo cha Ujasiriamali na Biashara *(Business Service Centre).*

- Kupanua jengo la maktaba ya Kampasi ya Solomon Mahlangu na kukamilisha tathmini ya ujenzi wa chanzo mbadala cha maji kwa ajili ya kampasi hiyo.

- Kuendeleza ujenzi wa maabara ya patholojia ya mbegu kwa ufadhili wa *DANIDA*.

- Kuendeleza ujenzi wa maabara ya Zoolojia, kituo cha Ujasiriamali na Biashara na Upanuzi wa maktaba iliyoko Kampasi ya Solomon Mahlangu, kwa ufadhili wa Serikali ya Norway chini ya mradi wa *FOCAL.*

- Kukamilisha taratibu za kukifanya Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Sokoine cha Kilimo. *(Makofi)*

- Chuo kitadahili jumla ya Wanafunzi 850 katika mwaka 2004/2005 kati ya hao, 700 kwa udhamini wa Serikali na 150 kwa udhamini binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005,Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kinatarajia kutekeleza yafuatayo: Kupanua matumizi ya kompyuta katika Chuo na kuimarisha mawasiliano, kujenga karakana ya kompyuta itakayotumika kwa mafunzo na matengenezo, kuongeza idadi ya wanafunzi kufikia 19,000, kuboresha uwiano kati ya wanafunzi wanawake na wanaume kufikia asilimia 24, kuhamasisha uandishi wa vitabu vya masomo kwa kutumia wataalam wa hapa nchini na kuongeza idadi ya wanafunzi wasioona na kurekodi kanda za kutosha za masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Chuo Kikuu Mzumbe kinatarajia kutekeleza yafuatayo: Kuendeleza ujenzi wa maktaba ya chuo kwa msaada wa fedha kutoka Mfuko wa Elimu, kuendelea na ukarabati wa majengo ya chuo kwa ajili ya malazi ya Wanafunzi, kukarabati jengo la chuo lililoko Dar es Salaam kwa mkopo kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania, kuajiri Walimu saba wa *Ph.D.* na kuwasomesha Walimu saba katika ngazi ya Uzamili na Chuo kinatarajia kudahili jumla ya Wanafunzi 800 kati ya hao, 250 kwa udhamini wa Serikali na Wanafunzi 550 kwa udhamini binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili kinatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuandaa mikakati ya ujenzi wa vyumba vya mihadhara ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi.

- Kukarabati na kuongeza uwezo wa maktaba kutoka wanafunzi 197 kwa sasa hadi 1300. *(Makofi)*

- Kufanya mapitio ya ikama ya wafanyakazi mara baada ya kukamilika kwa mgawanyo wa wafanyakazi baina ya Chuo na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

- Kuendelea na ukarabati wa hosteli zilizoko Barabara ya Chole, *Oysterbay,* zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 595.

- Kudahili Wanafunzi wa Shahada mpya za *BSc. Nursing Mid-Wifery* na *BSc. Nursing Management. (Makofi)*

- Chuo kinatarajia kudahili jumla ya Wanafunzi 410 kati ya hao, 250 kwa udhamini wa Serikali na 160 kwa udhamini binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu linatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kuratibu na kusimamia taratibu za uanzishwaji, usajili na ithibati ya Vyuo vya elimu ya juu.

- Kukagua, kutathmini na kutoa stahili za barua za mamlaka za uanzishwaji wa Vyuo vipya vitano na hati za usajili kwa Vyuo Vikuu vishiriki kumi.

- Kukagua na kuhuisha ithibati *(re-accreditation)* ya Vyuo Vikuu viwili vya umma na kimoja cha binafsi.

- Kukamilisha mfumo wa tuzo za Kitaifa za Elimu *(National Qualifications Framework).*

- Kuendelea kutoa machapisho na kuelimisha umma kuhusu majukumu na taratibu za ithibati ya elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Mamlaka ya Elimu Tanzania inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea kuutangaza Mfuko wa Elimu.

- Kuelimisha na kuhamasisha umma kuchangia gharama za elimu kwenye Mfuko wa Elimu Tanzania na kuwekeza kwenye miradi ya elimu.

- Kudhibiti na kuboresha taratibu, miongozo na vigezo vya matumizi ya fedha za Mfuko wa Elimu.

- Kutoa ruzuku na mikopo ya riba nafuu kwa taasisi na shule ili kuongeza ubora wa elimu ikiwa ni pamoja na miundombinu.

- Kuanzisha na kuendeleza mashirikiano na makubaliano na wadau mbalimbali kama, wakala wa kukusanya kodi, wasimamiaji wa Miradi ya Elimu, Mifuko ya Elimu ya Wilaya na Wizara zinazosimamia Elimu.

- Kushirikiana na TAMISEMI katika kuanzisha na kuimarisha Mifuko ya Elimu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Elimu ya Ufundi, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2004/2005, inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kugharamia mafunzo ya watumishi 15 wa Vyuo vya Ufundi Arusha, Mbeya na Makao Makuu katika ngazi ya Udaktari wa Falsafa, Shahada ya Uzamili, *Diploma* ya Uzamili na Stashahada ya Juu ya Uhandisi.

- Kukarabati majengo, mitambo na vifaa mbalimbali kwa Vyuo vya Ufundi Arusha na Mbeya.

- Kutoa mafunzo maalumu kwa wasichana katika mpango maalum wa kujiunga na elimu ya ufundi katika Vyuo vya Ufundi Arusha na Mbeya.

- Kugharamia mafunzo maalumu ya Ualimu kwa walimu wahandisi watakaoajiriwa katika Vyuo vya Ufundi Arusha na Mbeya.

- Kununua na kufunga mashine na mitambo katika chuo cha Ufundi Mbeya kwa Lengo la kuboresha mafunzo yatolewayo.

- Kuhuisha Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996 ili iendane na mabadiliko ya sasa ya ushindani kiteknolojia na utandawazi.

- Kununua vitabu vya kiada na rejea kwa Vyuo vya Ufundi Arusha na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kukarabati maabara nne pamoja na mabweni manne ya Taasisi.

- Kuanza kutumia mitaala mipya ya masomo katika ngazi ya ufundi sanifu kwa kutumia mfumo mpya wa *National Technical Awards.*

- Kuanza kutoa kozi mpya ya uzamili inayohusu masuala ya ukarabati.

- Kununua kompyuta 300 zaidi na vifaa vya Teknolojia ya mawasiliano na habari ili viweze kufungwa katika maabara saba za kompyuta zitakazoanzishwa katika Taasisi hii.

- Kutayarisha mitaala mipya saba ya masomo katika ngazi ya ufundi sanifu kwa kutumia mfumo wa *NTA.*

- Kudahili Wanafunzi 120 wa kiwango cha Shahada.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi linakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kusajili Vyuo 25 na kutoa ithibati kwa Vyuo 20 vyenye uwezo wa kutoa mafunzo ya elimu ya ufundi.

- Kuratibu mitihani ya ufundi kwa ngazi ya ufundi Sanifu *(FTC)* na Stashahada ya juu ya uhandisi *(ADE)*.

- Kuratibu mafunzo ya utayarishaji wa mitaala inayozingatia umahiri na mahitaji ya soko la ajira.

- Kuandaa, kukuza na kuidhinisha mitaala ya programu za mafunzo 12 yenye kuzingatia umahiri *(Competence-based).*

- Kusimamia na kuhakiki ubora wa mafunzo yatolewayo katika Vyuo vya ufundi *(Quality Control and Quality Assurance)*.

- Kuimarisha ushirikiano na baadhi ya Taasisi za ndani na nje zilizo na majukumu yanayofanana na Baraza hili.

Mheshimiwa Spika, Sayansi na Teknolojia, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara yangu inatarajia kutekeleza yafuatayo, kama ilivyopendekezwa katika kifungu cha 14 cha *declaration on science and the use of scientific knowledge* katika mkutano ujulikanao kama *UNESCO - World Conference on Science, Science for the Twenty - First Century A New Commitment (WCS/3/Draft Rev),* uliofanyika mwezi Julai, 1999 Budapest, Hungary.

- Kuandaa Nyaraka mbalimbali kwa maamuzi ya Serikali kuhusu Tanzania kuanzisha vituo vya sayansi *(Science Parks),* kwa lengo la kuwaunganisha watafiti, wataaluma, viwanda na wadau mbali mbali katika masuala ya sayansi na tekinolojia na Tanzania kuanzisha kituo cha *Millennium Science Initiative (MSI)*, kituo kitakacho jishughulisha katika kujenga uwezo wa watafiti, wanasayansi na wanatekinolojia kwa kuridhia mikataba saba inayosimamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(IAEA),* kuandaa utaratibu wa uundaji upya wa Kamati za Sayansi na Teknolojia katika ngazi za Wilaya na Vijiji, kukamilisha utungaji wa Sera ya Utafiti wa Sayansi nchini, kukamilisha utungaji wa Sera ya Bioteknolojia kuhuisha Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 iliyounda Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, kukamilisha mwongozo wa kuwahamasisha wanafunzi wa kike kujiunga na masomo ya sayansi na tekinolojia katika ngazi mbali mbali za elimu, kukamilisha mwongozo wa kuwaenzi wabunifu, wagunduzi na wenye vipaji maalum na wale wanaoendeleza Teknolojia asilia kwa maendeleo ya Taifa la kisasa la Tanzania *(Indigenous Technologies),* pamoja na kuratibu uanzishaji wa chombo kipya cha Tume ya Taifa ya Nguvu za Atomiki *(The Tanzania Atomc Energy Commission - TAE),* kitakachochukua nafasi ya Tume ya Taifa ya Mionzi.

Mheshimiwa Spika katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia itatekeleza yafuatayo:-

- Kukamilisha uanzishaji Masjala ya Taifa ya Utafiti *(The National Research Registry).*

- Kuhawilisha teknolojia mbali mbali zikiwemo tekinolojia za ujenzi wa nyumba za gharama nafuu, ukulima wa uyoga, ujenzi wa nyumba kwa kutumia mianzi katika sehemu zenye mianzi hapa nchini na utengenezaji wa *briquettes* na majiko sanifu, ukaushaji wa mazao ili kusaidia utunzaji wa chakula kwa matumizi ya baadae na kupunguza upoteaji wa chakula na utumiaji wa *biolatrine* kwa asasi za Magereza.

- Kuboresha teknolojia za mawasiliano na habari nchini kwa kupanua mtandao wa mawasiliano kwa njia ya kompyuta kati ya taasisi, asasi na mtandao wa watafiti wa ndani na nje.

- Kutoa mafunzo kwa wadau mbali mbali na kuunganisha Wilaya za Kilosa na Lindi kwenye mtandao wa *Internet.*

- Kuendelea na utafiti na utekelezaji wa miradi ya matumizi ya nishati mbadala (makaa ya mawe, mionzi ya jua, upepo na gesi ya samadi) majumbani na kufadhili miradi ya utafiti kulingana na vipaumbele vya utafiti.

- Kuandaa kongamamo la wanasayansi na watafiti pamoja na maonyesho ya sayansi ya vijana.

- Kusimamia uanzishaji upya wa chama cha wagunduzi Tanzania na kuendelea na ufuatiliaji wa wabunifu na wenye vipaji maalum katika mikoa.

- Kutoa mafunzo mbali mbali kwa watafiti ili kuwawezesha kutayarisha miradi ya utafiti inayokubalika kitaaluma.

- Kuendelea na ukarabati wa jengo la Tume.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Tume ya Taifa ya Mionzi itatekeleza yafuatayo:-

- Kupima uchafuzi wa mionzi katika vyakula na bidhaa zingine na kutoka nchini ambapo sampuli 2,500 zinatarajiwa kupimwa.
- Kutoa huduma za upimaji mionzi kwa wafanyakazi 1,000 katika vituo 250 vya mionzi.

- Kukagua na kutoa leseni kwa vituo 250 vinavyotumia mionzi.

- Kuanza kutumia maabara mpya ya hifadhi ya mabaki ya vyanzo vya mionzi, kwa kukusanya, kushughulikia na kuhifadhi mabaki ya mionzi yote yaliyo katika Taasisi 10 hapa nchini.

- Kutoa elimu ya kinga ya mionzi kwa umma na wafanyakazi 1,200 wa mionzi kwa kupitia vyombo vya habari, vipeperushi, semina na mafunzo maalum.

- Kuratibu na kusimamia uingizaji na uimarishaji wa teknolojia ya nyuklia, kwa kupitia miradi ya kitaifa na kikanda inayofadhiliwa na *IAEA.*

- Kuendeleza mpango wa ukaguzi wa migodi sita na minara ya simu za mikononi ipatayo 900 ili kubaini hali ya usalama na kupendekeza hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Tume ya Taifa ya *UNESCO* inatarajia kufanya yafuatayo: Kuendelea kuratibu utekelezaji wa maamuzi ya Kikao cha 32 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya Serikali, kuratibu utekelezaji wa Miradi inayoendelea na ile itakayoidhinishwa katika kipindi cha mwaka 2004/2005 na kushirikisha Taifa katika maandalizi ya Programu na Bajeti ya *UNESCO* kwa kipindi cha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Idara ya Utawala na Utumishi inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuwadhamini watumishi 35 mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi.

- Kutekeleza Mkataba wa huduma kwa Mteja kwa lengo la kuboresha huduma inayotolewa na Wizara kwa Umma na kuendesha mafunzo kwa watumishi 453 kuhusu uhusiano na wateja *(Client Service Charter).*

- Kuwapandisha vyeo watumishi 60 wa kada mbalimbali ambao wametimiza masharti ya ajira zao.

- Katika hatua za awali za kutekeleza Mpango wa Maboresho ya Utumishi wa Umma *(PSRP),* Wizara itaanza rasmi kushirikisha Sekta Binafsi kuanzia mwezi Julai, 2004, katika kutoa huduma zisizo rasmi *(non core functions),* hususan huduma za ulinzi, usafi na mapokezi.

- Kutekeleza mfumo wa uwazi wa upimaji utendaji kazi wa mtumishi Serikalini *(Open Performance Review Appraisal System).*

- Kuhamasisha watumishi kuhusu mambo yafuatayo kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa Wananchi: Elimu ya Jinsia katika sehemu za kazi, athari za ugonjwa hatari wa Ukimwi na mbinu za kupambana na rushwa sehemu za kazi

Mheshimiwa Spika, Dira ya Wizara ya Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu kufikia mwaka 2025, ni kujenga jamii iliyoelimika, yenye uwiano wa kijinsia na inayoweza kujiletea maendeleo kwa kutumia Sayansi na Teknolojia. Ili kufanikisha azma yake, Wizara katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuanzisha Bodi ya mikopo ya wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu na ufundi. Mpango huu unatarajiwa kupanua udahili wa wanafunzi katika Vyuo Vikuu vya umma na vya binafsi kwa kudahili wanafunzi ambao hapo nyuma walikuwa wanakosa nafasi kwa kukosa ama udhamini au mikopo. Takwimu zinaonyesha kwamba wastani wa asilimia 65 wamekuwa hawapati udhamini wa Serikali na hivyo kulazimika kujiunga na Vyuo vingine vya umma au Vyuo Vikuu binafsi kwa kujigharimia wenyewe. Tazama kiambatanisho namba nane.

- Kuongeza Udahili wa Wanafunzi ndani na nje. Udahili wa ndani unategemewa kuongezeka kutoka Wanafunzi 5,150 kwa mwaka 2003/2004 hadi kufikia Wanafunzi 5,870 kwa mwaka 2004/2005 ikiwa ni ongezeko la asilimia 13.9. Udahili wa nje ya nchi unategemewa kuongezeka kutoka Wanafunzi 58 kwa mwaka 2003/2004 hadi kufikia Wanafunzi 96 kwa mwaka 2004/2005 ikiwa ni ongezeko la asilimia 65.5.

- Kuendelea kuhamasisha wananchi kuhusu dhana ya kuchangia gharama za elimu kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania.

- Kufanya uchunguzi wa kina *(Mapping),* juu ya mahitaji halisi ya idadi ya Vyuo vya elimu ya juu na ufundi nchini kwa kuzingatia ongezeko la idadi ya wahitimu kutoka Sekondari na Vyuo vya Ufundi Stadi.

- Katika hatua za awali za kutekeleza mpango wa kuboresha Utumishi wa Umma *(PSRP),* Wizara itaanza rasmi kushirikisha Sekta Binafsi katika kutoa huduma za ulinzi, usafi na mapokezi.

- Kuwasilisha Bungeni sheria ya Elimu ya Juu (Vyuo Vikuu).

- Kuanzisha mfumo wa utoaji wa huduma kwa wateja kwa kukamilisha Mkataba wa Hiari wa Utoaji Huduma *(Client Service Charter).* Mkataba unatilia mkazo misingi ya utumishi bora wa umma, unaolenga katika kuboresha huduma, uwajibikaji, uadilifu, utii kwa Serikali, ukarimu kwa wateja na kuheshimu sheria na maadili ya taaluma.

- Kuendelea kuboresha mitaala na mbinu za kufundishia kwa lengo la kuboresha elimu ya juu na ufundi ili kukidhi haja ya soko la ajira.

- Kuendelea kuweka uwiano mzuri wa kinjinsia katika Vyuo vya elimu ya juu na ufundi.

- Kuratibu kusimamia na kuhakikisha kwamba Vyuo vya elimu ya juu na ufundi vinavyoanzishwa vinakidhi vigezo vilivyowekwa na Taasisi za kusimamia zoezi hilo.

- Kuratibu ushirikishwaji wa Taifa katika mkutano mkuu wa kimataifa wa Elimu unaofadhiliwa na *UNESCO* utakaofanyika Geneva, Septemba, 2004 *(UNESCO International Conference on Education, Geneva, September, 2004).*

- Kuendelea na uhamasishaji watumishi, wasomi na Wanataaluma wawe washiriki katika vita dhidi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI, ili kuitunza nguvu ambayo ni hazina ya pekee kwa maendeleo ya Taifa.

- Kuendeleza juhudi za kupambana na rushwa katika Wizara na Taasisi zake.

- Kutoa mafunzo ya muda mrefu ya uzamili na muda mfupi, ndani na nje ya nchi kwa Walimu wa Vyuo vya Arusha na Mbeya pamoja na kuwadhamini watumishi katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

- Kununua Mitambo na Mashine kwa ajili ya Chuo Cha Ufundi Mbeya na kukiimarisha, ili kiweze kutoa mafunzo katika ngazi ya juu ya Elimu ya Ufundi. Hii ni hatua mojawapo ya kukigeuza chuo hiki kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia.

- Kuratibu utekelezaji wa miradi iliyosajiliwa na *UNESCO* na ile itakayoidhinishwa katika kipindi cha mwaka 2004/2005.

- Kuendelea kuhamasisha Wanafunzi na wafanyakazi madhara ya ugonjwa hatari wa UKIMWI.

- Kuridhia mikataba mbali mbali ya Kimataifa inayosimamia matumizi salama ya Nyuklia.

- Kutathmini Sera ya elimu ya juu na kutathmini mpango wa ugharimiaji wa elimu ya juu na kutoa mapendekezo ya kuboresha/kurekebisha.

- Kuendelea kuhamasisha matumizi ya sayansi na teknolojia.

- Kuhamasisha wananchi kuhusu uundaji wa Kamati za Sayansi na Teknolojia na uanzishaji wa vituo vya sayansi.

- Kuhamasisha wanafunzi mashuleni kuchukua masomo ya sayansi za msingi katika ngazi zote za elimu.

- Kutoa mwongozo kwa wabunifu na wagunduzi.

- Uhuishaji wa Sera ya Sayansi na Teknolojia.

- Utungaji wa Sera ya Utafiti wa Kisayansi na Kiteknolojia.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wahisani na wadau mbalimbali kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika Wizara yangu. Ni dhahiri kuwa msaada walioutoa na wanaoendelea kutoa hususan katika kuboresha Sayansi na Teknolojia, Elimu ya Juu na Ufundi, katika Vyuo na taasisi umesaidia kwa kiasi kikubwa kuchangia pale ambapo Serikali imekuwa ikishindwa kutokana na ufinyu wa bajeti. Nchi hizo ni pamoja na Sweden, Uholanzi, Japan, Ubelgiji, Jamhuri ya Korea, Jamhuri ya watu wa China, na Umoja wa Nchi za Ulaya. Aidha, Mashirika ni pamoja na Benki ya Dunia, *Commonwealth Science Council, International Atomic Energy Agency, Third World Academy of Sciences, Interantional Foundation for Sciences, UNESCO* na Shirika la Kimaendeleo la Sweden *(SIDA/SAREC), Carnegie Foundation, NORAD* na *DANIDA*. Naomba waendelee na moyo huo, nasi tunaahidi kuendeleza ushirikiano huu kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha hotuba yangu naomba ruhusa kumnukuu James D. Welfolson, Rais wa Benki ya Dunia alipokuwa akizindua Kamati ya Kazi ya Benki ya Dunia kuhusu umuhimu wa elimu ya juu katika maendeleo ya Taifa naomba

ruhusa sasa kunukuu: *"It is impossible to have a complete education system without an appropriate and strong higher education system, I am not for a moment suggesting that primary education and secondary education are not at the very essence of development and that this is not enough. You have to have centers of excellence and learning and training if you are going to address the issues of property and development in the developing countries. The key is the higher education not just on the technological side but to create people with enough wisdom to be able to use it". (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia usemi huu pamoja na azma yetu ya kutekeleza dira ya maendeleo Wizara yetu katika mwaka wa fedha inaomba sasa ili kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza mipango iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2004/2005, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 84,315,118,600.00. Kati ya fedha hizo, Sh. 70,284,667,800.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh 14,030,450,800.00 ni kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Wachangiaji wanne wa mwanzo watakuwa ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali na Mheshimiwa Margareth Mkanga.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, atoe maoni ya Kamati yake. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutimiza masharti yaliyomo kwenye Kanuni ya 81(1), Toleo la 2004 ya kutoa maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii uliyoipa jukumu la kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo yaliyowekwa katika Bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa mwaka 2003/2004 na kupitia Malengo ya Makadirio ya Wizara hiyo kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii ilichambua na kujadili yafuatayo: Dira na majukumu ya Wizara ya Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu, utekelezaji wa maagizo ya mapendekezo ya Kamati wakati ikichambua Bajeti ya Wizara

ya Mwaka 2003/2004, utekelezaji wa Malengo yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 na malengo yaliyowekwa na maombi ya Fedha kwa Mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kujadili na kuchambua vipengele vilivyotajwa hapo juu; Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na Naibu wake wakisaidiwa na timu ya Wataalam ikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara, walijibu hoja na maswali mbalimbali yaliyotolewa na wanakamati na hivyo kukubali hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojioa na Elimu ya Juu iletwe kwenye Bunge lako Tukufu ili ijadiliwe na aidhinishiwe Bajeti ya Wizara yake kwa mwaka 2004/2005. Hivyo, Kamati yangu inaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali kupitia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii inaunga mkono Dira ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, inayoipa jukumu la kugeuza nchi yetu kuwa yenye misingi imara, yenye kuipa uwezo wa kuwa mshindani katika nyanja za Sayansi na Teknolojia miongoni mwa Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na dhima ya Wizara ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Juu, Ufundi, Sayansi na Teknolojia ili kuwezesha upatikanaji wa nguvu kazi yenye uwezo wa kutumia rasilimali zilizopo kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati inaunga mkono lengo la kuwezesha utoaji wa elimu iliyo bora na yenye uwiano bora wa kijinsia katika nyanja za ufundi na elimu ya juu, kuratibu na kuendeleza Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Wadau, kuajiri wataalam wenye sifa, kuweka na kudumisha kiwango cha juu cha ubora katika utekelezaji na kuwa na Wataalam wanaohitajika katika Taasisi kulingana na mahitaji ya jamii ya Tanzania na ulimwengu wa utandawazi.

Aidha, Kamati inashauri kuwa ni vizuri kujenga mazingira bora kwa ajili ya sekta binafsi kushiriki katika utoaji wa Huduma za Elimu ya Juu, Ufundi, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, Kamati ya Huduma za Jamii ina maoni kuwa pamoja na kukubaliana na maelezo hayo hapo juu, kwa muda wa miaka mitatu mfululizo imekuwa ikiishauri Serikali kujenga misingi itakayowezesha Taifa kutumia Sayansi na Teknolojia katika sekta zote za uzalishaji kwa kutenga asilimia moja ya pato la Taifa kila mwaka kwa ajili ya mfuko wa kuendeleza utafiti katika nyanja za Sayansi na Teknolojia na hivyo kuwezesha Serikali kufikia dhima yake ya kuleta mafanikio katika matumizi ya Sayansi na Teknolojia ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, Kamati inataka Serikali ituambie ni asilimia ngapi ya pato la Taifa inatengwa kila mwaka kwa ajili ya Mfuko wa Sayansi na Teknolojia na kuendeleza utafiti kama ilivyoelekezwa katika Sera ya Serikali ya Sayansi na Teknolojia ya kutenga asilimia moja ya Pato la Taifa kila mwaka kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia.

Kamati inaweka msisitizo huo ikifahamu kuwa nchi zote zilizofanikiwa kutumia Sayansi na teknolojia na kuboresha uzalishaji zimekuwa zikitumia matokeo ya utafiti, kwa kutenga fedha nyingi kila mwaka kwa ajili ya kuendeleza utafiti *(Research Development).* Mipango hiyo huwa ni pamoja na kuhamisha au kununua na kuendeleza teknolojia inayohitajika kwa maendeleo ya nchi hiyo *(transfer, adopt and develop appropriate technology). (Makofi)*

Hivyo, ili kufikia lengo hilo, Kamati inashauri kuwa mafanikio yaliyokwishapatikana na yanayopatikana katika utafiti wa Sayansi na Teknolojia, yaendelezwe na yasambazwe *(out reach activities)* kwa wananchi ili kuwarahisishia uzalishaji, maisha yao na hatimaye kuinua Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kufanikisha kuleta maendeleo ya matumizi ya Sayansi na Teknolojia Kamati yangu inashauri kuwa Wizara ya Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu ifanye juhudi za makusudi za kuanzisha mahusiano ya karibu na Shirika la Nyumbu - Kibaha, *Tanzania Automotive Centre,* lililopo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Tunashauri kuwa Kitivo cha Uhandisi cha Chuo Kikuu Dar es Salaam kipewe nafasi na uwezo wa kutumia kikamilifu miundo mbinu iliyopo, vifaa na wataalam kuendeleza utafiti na mafanikio ya utafiti yaliyokwishapatikana katika mradi huo.

Aidha, Kamati inashauri kuwa teknolojia ya kuzalisha magari ambayo yaliwahi kuonyeshwa kwenye maonyesho ya Sabasaba miaka ya 90 iendelezwe na kuzalishwa kibiashara ikiwezekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya juu, Kamati yangu ilijadili maendeleo ya Vyuo vya Elimu ya Juu na kutoa maoni yafuatayo kwa baadhi ya vyuo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kukubali ushauri wa kuboresha miundo mbinu ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na mitaala, uwezo wa wahadhiri na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili elimu ya ufundi inayotolewa iweze kukidhi mahitaji na mabadiliko katika sayansi na teknolojia.

Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na Baraza la Elimu ya Ufundi *(NACTE),* iwezeshwe kutunga mitihani na kutoa tuzo kwa kuzingatia taaluma zinazofundishwa kama ilivyo kwa Vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye juhudi za makusudi kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia ili Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam iweze kufikia hadhi iliyokusudiwa ya ubora wa hali

ya juu *(Centre of Excellency)* ikiwa ni pamoja na kuwa na uwezo wa kutoa wahitimu wazuri waliobobea katika taaluma za teknolojia mpya kwa kuzingatia mahitaji ya soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ushauri huo, Kamati inataka Serikali ione umuhimu wa kutumia teknolojia na vifaa mbalimbali vinavyobuniwa na Vyuo au Taasisi za Ufundi ili kuvijengea uwezo, mfano taa za kuongoza magari barabarani *Traffic Lights* zilizobuniwa na Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam *(DIT),* Majiko Sanifu yaliyobuniwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM)* na kadhaliika. Pia taarifa za mafanikio katika kubuni vifaa ziwe zinaletwa hapa Bungeni kwa nia ya kuelimisha wananchi kupitia wawakilishi wao na kuona kama kweli tunapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kamati inashauri kuwa Vyuo hivyo vipewe uwezo kuzalisha na kuuza teknolojia hizo badala ya Serikali kuendelea kuziagiza kutoka nje ya nchi. Hivyo, Taasisi za Serikali zionyeshe uzalendo katika kununua bidhaa zinazotengenezwa kwa ubora unaofaa kutoka ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa azma yake ya kuboresha miundombinu ya Chuo cha Ufundi Mbeya na kuwa na mipango ya kuinua hadhi yake hatua kwa hatua na kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia *(MIST)* na hatimaye ifikie hadhi ya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia *(MUST).*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali na uongozi wa Chuo kwa kukarabati majengo ya Chuo yaliyoachwa na Warusi waliokuwa wanajenga Chuo hicho. Vile vile Kamati inapongeza Chuo kwa kutunza vizuri mazingira, kutengeneza samani za Chuo na kutenga maeneo maalum kama hatua muhimu sana ya usalama katika mabweni ya wanachuo kwa ajili ya huduma mbalimbali kama vile kupiga pasi, kuchemsha maji, kuchemsha chai au kahawa, kupumzikia, kusikiliza redio na kuangalia *Television* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri ufuatao kuhusu chuo hiki:-

- Serikali ifanye maandalizi ya kutosha kutekeleza azma yake kwa Chuo kupata wataalam wenye sifa, vifaa vya kufundishia, kuzingatia mahitaji ya Wataalam katika soko la ajira yanayobadilika kufuatana na mabadiliko yanayoendelea katika nyanja za Sayansi na Teknolojia.

- Barabara inayoelekea Chuoni kutoka Barabara kuu iendayo Zambia itengenezwe kwa kiwango cha lami.

- Serikali itenge fedha za kujenga uzio kwenye ardhi inayomilikiwa na Chuo kwani kuna watu wanaovamia na pia Serikali itoe hati kwa Chuo kumiliki eneo hilo kisheria ili itumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

- Chuo kibuni mipango kabambe ya kuendeleza na kutumia kikamilifu ardhi ya Chuo kama ambavyo Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam na *SUA* walivyo na mipango kabambe ya kutumia ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Mzumbe kinaunganishwa na barabara ya vumbi toka barabara kuu iendayo Iringa. Kamati yangu ikiwa na Naibu Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, ilifanya ziara Chuoni hapo mwezi Februari, 2004 na kujionea adha wanayopata Wanamzumbe na hasa wageni wa Kimataifa wanapotembelea Chuo kutokana na barabara hiyo ya vumbi. Wageni kila wanapotembelea Chuo hiki wamekuwa wakisikika wakisema *that road again* walipokuwa wakiaagana na wenyeji wao.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na aibu hii *(that road again),* tunashauri Serikali kuijenga barabara hii hadi kiwango cha lami kupitia Mpango wa Barabara za Mkoa *TANROADS* katika mwaka huu wa fedha. Tunamshukuru Mkuu wa Mkoa Morogoro, ambaye alikubali kufuatilia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ingependa kupata taarifa ya utekelezaji wa suala hili kwani tulipokubali kuanzisha Chuo Kikuu, ni lazima vile vile tukubali na gharama zake kama tunavyokubali gharama ya kuendesha demokrasia ya Vyama Vingi. *(Makofi)*

Kamati inakipongeza Chuo Kikuu cha Mzumbe, kwa jitihada zake za kutafuta ufumbuzi kwa matatizo yanayokikabili katika kutoa Elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipongeza juhudi zinazofanywa na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Morogoro *(SUA),* za kuongeza idadi ya wanafunzi katika Chuo hicho kwa lengo la kutumia vizuri miundombinu iliyopo. Kamati inashauri Serikali kuwa, ili kupunguza gharama za kukodisha mabweni ya wanafunzi ikamilishe ununuzi wa maghorofa ya Kihonda yaliyokuwa mali ya Kiwanda cha Morogoro *Ceramics,* badala ya Chuo kuendelea kuyakodisha kwa gharama kubwa kutoka kwa mmiliki wa sasa. *(Makofi)*

Aidha, Kamati inashauri kuwa zoezi hili liendane na Serikali kutenga fedha za kutekeleza mpango wa kujenga mabweni ya wanafunzi katika ardhi ya Chuo kwa kuzingatia mpango kabambe wa kutumia ipasavyo rasilimali ya Chuo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampasi ya Mazimbu, Kamati ilishauri Serikali kuandaa mikakati ya kuendeleza na kutumia kikamilifu muindombinu iliyoachwa na wapigania uhuru wa *ANC* hasa Kiwanda cha Samani, Shamba la Mifugo, Mashine ya kutengeneza vyakula vya mifugo na mabohari. Ni vema tukubali ukweli kuwa baadaye itakuwa vigumu sana kujenga au kufufua mitambo ambayo kwa sasa haifanyi kazi kwa kukosa mtaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, kama kweli Serikali ina nia ya kuimarisha utekelezaji katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na kuimarisha matumizi ya miundombinu hiyo, basi itoe mtaji wa kuendeshea miundombinu hiyo

kutokana na fedha za Serikali au fedha zinazopatikana baada ya kuuza Mashirika ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri huu unatokana na imani na ukweli kuwa, *SUA* kuna wataalam wa kutosha kuweza kufufua miundombinu hiyo na hatimaye kuwa kitovu cha maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa ili *SUA* iweze kujiongezea mapato yake kutokana na tafiti mbalimbali zilizokwishafanikiwa, ni vema Chuo kijitangaze katika nyanja walizofanikiwa vizuri, mfano mzuri ni utafiti wa mbegu bora, miche ya mazao mbalimbali, uwezo wa Panya Buku wa kugundua mabomu yaliyotegwa ardhini na kadhalika

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inakipongeza Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwa mafanikio yaliyopatikana katika nyanja za utafiti, kufundisha na kutoa ushauri wa kitaalam *(Research, Training and Consultancy),* kama ilivyoonekana katika maonyesho ya *Dar es Salaam International Trade Fair* ya mwaka huu na kuweza kuwa mshindi wa kwanza katika nyanja hizo. Ni matumaini ya Kamati yangu kuwa, Chuo kitaendeleza jitihada zake na kuendelea kufanikiwa katika kuelimisha jamii kupitia maonyesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga fedha za kuendeleza Taasisi ya Sayansi za Bahari *(Institute of Marine Sciences),* iliyopo Zanzibar ikiwa ni pamoja na fedha zilizotumika kulipa fidia za mali na mazao ya Wananchi wa eneo la Buyu. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kutoa ardhi ya kutosheleza mahitaji ya Taasisi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali ianze ujenzi wa Taasisi hiyo mapema iwezekanavyo. Aidha, Kamati inapongeza hatua za awali za kuweka jiwe la msingi na kukamilika kwa michoro na ramani za majengo ya Taasisi. Kamati inatazamia kutembelea eneo hilo kabla ya Mkutano wa Bunge lijalo kulingana na ratiba ya kazi zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Elimu Tanzania, Kamati inampongeza Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa juhudi zake za kutembelea karibu Mikoa yote na kuelimisha na kuhamasisha wadau kuchangia Mfuko huu maalum wa kuimarisha miundombinu ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa ili Mamlaka ya Elimu Tanzania iweze kuimarisha uwezo wake na kutekeleza kazi zake kwa ufanisi, Serikali ilete Bungeni marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Elimu Tanzania *(Tanzania Education Fund)* na kuwezesha Bunge kuweka kiwango cha chini cha Serikali kuchangia kila mwaka kutoka Hazina kwa ajili ya Mfuko wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri hivyo baada ya kugundua kuwa, kiwango cha fedha kinachotolewa na Serikali kwa ajili ya Mfuko huu kimeendelea kupungua kila mwaka tangu Mfuko huo uanzishwe kwa maelezo kuwa ndicho kiwango kilichopatikana.

Hoja hii ya Serikali tunaona ni dhaifu tukizingatia ukweli kuwa mapato ya Serikali yanaongezeka na uchumi wa nchi unaonyesha kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwaka 2001/2002, katika bajeti Mamlaka ilipewa asilimia 0.5, Mwaka 2002/2003, ilipewa asilimia 0.4; Mwaka 2003/2004 ilipewa asilimia 0.39 na matarajio yanaonyesha ambayo pengine tutajua kwenye hotuba ya Waziri au bajeti yake kwa 2004/2005 inaonekana kwamba matarajio ni 0.3 tu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa endapo Serikali itaendelea na mtindo huu wa kushusha kiwango cha fedha za Mfuko huu kila mwaka na endapo haitaonyesha nia ya kuimarisha Mfuko huu wakati mapato yake yanaongezeka, mfuko huu ambao ni muhimu kwa maendeleo ya Watanzania, basi Bunge litafute namna ya kuishinikiza Serikali au Wabunge tulete Muswada binafsi wa kuweza kurekebisha hali hii ili Sheria itaje kiwango cha chini cha Serikali kuchangia, badala ya Sheria ya sasa kutaja tu kuwa kiwango cha juu kisizidi asilimia mbili ya Pato la Taifa baada ya kuondoa gharama za madeni ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali ipunguze matumizi yasiyo ya lazima kama vile takrima ili kuimarisha Mfuko huu muhimu wa elimu ya Watanzania. *(Makofi)*

Aidha, Kamati inashauri kuwa uchangiaji wa watu binafsi katika Mfuko huu uangaliwe kwa makini hasa kwa Mashirika na makampuni makubwa ikiwekwa maanani kuwepo nafasi ya wachangiaji kupata nafuu ya kodi, ili usije ukatumika kama mwanya wa kukwepa kodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Kamati imeona tatizo la udahili mdogo katika Vyuo vya Elimu ya Juu mwaka huu na mfano hai ni kutoka Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam ambacho kati ya wanafunzi 7,079 wenye sifa za kuanza mwaka wa kwanza katika taaluma mbalimbali mwaka huu kama ilivyonukuliwa kwenye kitabu kilichotayarishwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni wanafunzi 2,500 tu wamechaguliwa. Hii ni kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali na kuwaacha wanafunzi wenye sifa karibu 4,579. Vile vile tunaamini kuwa takwimu kwa Vyuo vya *SUA* na Mzumbe hali ni hiyo hiyo. Hivyo, tatizo ni kubwa sana na linahitaji kuangaliwa upya na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali itoe udhamini kwa idadi kubwa zaidi mwaka huu wakati inaendelea na kuweka utaratibu wa kuanza kutumika Sheria inayounda Bodi ya Mikopo ya Wanafuzi katika Vyuo vya Elimu ya Juu.

Aidha, Kamati inashauri kuwa Serikali ichukue tahadhari ya kutosha wakati inaandaa kanuni za Mfuko huo ili azma na madhumuni yaliyokusudiwa wakati wa kuanzisha Mfuko yazingatiwe na hasa eneo la masharti ya dhamana kama ilivyochangiwa na wadau mbalimbali baada ya Muswada wa Sheria kupitishwa na Bunge lako.

Pia Kamati inashauri kuwa, Serikali itoe elimu kwa umma kuhusu madhumuni ya kuanzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili Wananchi waelewe malengo mazuri ya Serikali kwani kumekuwepo na upotoshaji kuhusu lengo la kuanzisha Bodi hii.

Mheshimiwa Spika, Vile vile Kamati inatoa ushauri ufuatao kwa maeneo mbalimbali:-

Serikali kupitia Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu *(HEAC),* liwezeshwe na liendelee kusimamia Vyuo vyote vya Elimu ya Juu vilivyoko Tanzania Bara na Zanzibar ili kuona kuwa viwango vya elimu inayotolewa inakidhi hadhi ya Vyuo vya Elimu ya Juu, kwa kuwepo kwa Wahadhiri wenye sifa na mazingira mazuri ya kujifunzia na kufundishia kwa kuzingatia taaluma zinazotolewa.

Aidha, Serikali itafute fedha ili kuwezesha Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu kujenga Ofisi yake katika kiwanja kipya kilichopo eneo la Victoria Dar es Salaam. Ushauri huu ni kutokana na adha na usumbufu unaolipata Baraza kutokana na tatizo la kukatika katika kwa umeme mara kwa mara katika ofisi waliyokodi katika jengo Shirika la Posta na hivyo kukosa kutumia ipasavyo teknolojia ya mawasiliano na Vyuo vya Elimu ya Juu ulimwenguni kote.

Aidha, Vyuo vyote vianzishe mpango wa kuendeleza wahadhiri waliopo kufikia ngazi ya shahada za juu ikizingatiwa kuwa wapo wahadhiri wenye umri mkubwa na karibu watalazimika kustaafu. Hivyo, kuanzishwe mpango maalum wa kujaza nafasi zitakazokuwa wazi kufuatia muda wa wahadhiri wenye umri mkubwa kustaafu utakapowadia.

Serikali ihamasishe Mashirika yenye uwezo wa kuanzisha Vyuo vya Elimu ya Juu kutokana na umuhimu wa kuwa na Vyuo vya Elimu ya Juu katika fani za Sayansi ili kukidhi mahitaji maalum na kuwezesha Taifa kuongeza kiwango katika matumizi na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia katika maisha ya jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii kumpongeza Waziri wa Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu na Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, ambao kwa mujibu wa Kanuni ya 87(1) ni Wajumbe wa Kamati yangu wakati wanawasilisha hoja yao na nawashukuru kwa ushirikiano tuliopata wakati tunachambua Bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa mwaka 2004/2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini na ushirikiano wao wakati wa kuchambua na kupitia vifungu mbalimbali vya bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba niwatambue wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii waliochambua Bajeti ya Wizara Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa kuwataja majina:-

Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi H. Mpeme, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Oscar T. Mloka, Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, Mheshimiwa Hamisi J. Nguli, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Halimenshi K. Mayonga, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Khamis Ali Salehe na mimi Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', ambaye ni Mwenyekiti. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru wataalam mbalimbali kutoka Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bi. Ruth Mollel, kwa michango na ushirikiano wao wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani kwa Katibu wa Bunge na Ofisi yake, kwa huduma walizotoa wakati wa vikao vya kuchambua Bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Mwisho, nampongeza Katibu wa Kamati hii Ndugu Theonest Ruhilabake, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa mwaka 2004/2005, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5) (b) (c) na 81(1), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii, niwapongeze Mheshimiwa Pius Ngwandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara, Viongozi wote wa Wizara, pamoja na Wakuu wa Vyuo vya Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu, kwa kazi zao nzuri wanazozifanya katika mazingira magumu kifedha.

Mheshimiwa Spika, leo katika kuzungumzia matatizo na mafanikio ya Wizara hii hasa kwa upande wa Vyuo Vikuu, sitapoteza muda kurudia maoni na ushauri ambayo nilikwishautoa kwa Wizara hii katika hotuba tatu za bajeti za miaka mitatu iliyopita lakini nikumbushie kuwa katika hotuba yangu ya mwaka 2003/2004, niliishauri Wizara kuandaa programu na mipango kamambe *(Master Plan)* ya kuongeza idadi ya Vyuo Vikuu na wanafunzi wake kwa awamu ya miaka mitano mitano. Nilishukuru wakati Mheshimiwa Waziri, alipokuwa akihitimisha hotuba yake mnamo tarehe 16 Julai, 2003, alisema kuwa, Wizara ilikuwa tayari imeshaandaa mpango kabambe kama nilivyoshauri.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya, mimi binafsi, pamoja, pengine na Waheshimiwa Wabunge wengi hawajaona kitabu kinachoelezea mpango huo ambao Mheshimiwa Waziri ameshautayarisha.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kama Wizara ilikwishatayarisha mpango huo, sasa ifikirie kuutazama upya kwa kutumia matarajio na matokeo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), kwani kwa kutumia takwimu za idadi ya wanafunzi wanaoingia shule za msingi na wale wanaotarajia kuingia shule za sekondari za kati na za juu, basi itakuwa rahisi kukadiria kwa uhakika zaidi kazi na rasilimali zinazotakiwa katika kuendeleza elimu ya juu na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, mwaka huu wa masomo 2003/2004, Tanzania inao wanafunzi 40,184 katika Vyuo Vikuu vya Umma, Vyuo Vikuu vya Binafsi, Taasisi za Elimu ya Juu zilizoko chini ya Wizara zingine, pamoja na Vyuo vya Ufundi. Katika Vyuo vya Umma kuna wanafunzi 28,910, katika Vyuo vya Ufundi kuna wanafunzi 2,103; Vyuo vilivyoko chini ya Wizara nyingine kuna wanafunzi 6,407 na Vyuo vya Binafsi kuna wanafunzi 2,764, ambao ni jumla ya wanafunzi 40,184.

Mheshimiwa Spika, ni makadirio ya Wizara ya Elimu na Utamaduni kuwa kutakuwa na wanafunzi 2,000,000 katika shule za sekondari ifikapo mwaka 2,010 na wahitimu wa sekondari wasiopungua 500,000 kila mwaka, bila shaka katika shule za sekondari za juu kutakuwa na wahitimu 250,00 kila mwaka. Hivyo, kutokana na takwimu za Wizara ya Elimu na Utamaduni katika kitabu chao cha *Basic Statistics in Education 1995 - 2004,* kwa matokeo ya mtihani wa Kidato cha sita VI mwaka 2003 asilimia za ushindi kwa *division one* 16.5% na II 30.8%. Hivyo, kama hali ikiendelea hivyo ni dhahiri kuwa kati ya wanafunzi 250,000, nusu yake kwa maana ya 125,000 watakuwa wanapaswa kuingia Vyuo Vikuu kila ifikapo mwaka 2010.

Idadi hiyo itakuwa kubwa, na hivyo kuthibitisha uhalali na ukweli wa kuwa na Chuo Kikuu kila Mkoa wa Tanzania Bara. Kwani ikiwa kufikia mwaka 2014, kutakuwa na wanafunzi wa Vyuo Vikuu 500,000 nchini Tanzania tukiwa na Vyuo Vikuu 21 na kila Chuo kikiwa na wastani wa wanafunzi 20,000, litakuwa jambo kubwa sana. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaiomba Wizara na Serikali kuipa msaada kifedha Baraza la Ithibati la Vyuo vya Elimu ya Juu *(The Higher Education Accreditation Council),* ili waweze kuwa na Ofisi zao pamoja na vitendea kazi kwani kwa sasa wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa siyo kazi ya wanasiasa kutunga mitaala ya masomo katika shule na vyuo vyetu. Lakini panapokuwa pana umuhimu wa kutoa ushauri, tunafarijika kufanya hivyo. Hivyo napenda kutoa ushauri kwa Wizara hii kuvikumbusha Vyuo vyetu Vikuu juu ya kuangalia uwezekano wa kuingiza somo la sheria component husika katika masomo yatolewayo katika Vitivo vya Kilimo, Uhandisi kuhusu sheria zinazoendana na mambo ya uhandisi au sheria za ndani na nje zinazoendana na mambo ya kilimo katika Kitivo cha Chuo husika. Hii itawasaidia wahitimu wa shahada hizo kuwa na *component* ya sheria husika katika eneo ambalo amesomea.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Aprili, 2004, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya *The Higher Education Student's Loan Board,* kwa ajili ya kutoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu. Mara tu baada ya Bunge kupitisha Muswada huo, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waliandamana kwa amani kupinga Muswada huo na Serikali kwa kasi kama ya mwanga, ilikifunga chuo hicho na baadaye wanafunzi wa Vyuo vingine kwa kushirikiana na wale wa Chuo Kikuu waliandamana tena na mara hii Serikali iliwasikiliza. Hivyo, kutokana na yale yaliyotokea, tunaomba kuishauri Serikali kujenga tabia ya majadiliano na wadau muhimu inapokuwa inatunga sheria fulani hasa zinazohusu jamii za Wananchi wa eneo hilo ili waweze kuelewa haki zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kugoma na kufukuzwa ndipo Serikali ilipoanza kufafanua na kutembelea Wananchi kuwaelimisha kuhusu sheria hiyo. Lakini ukizingatia kuwa Chuo kilipofungwa wanafunzi walipoteza muda na pesa kurudi makwao na Chuo chenyewe kilipoteza fedha nyingi kugharimia mambo mbalimbali ili kurejesha ratiba ya masomo katika hali yake na Serikali yenyewe ilipoteza fedha kwa kuunda Tume kuchunguza matatizo yanayosababisha migomo Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, sipendelei na siungi mkono migomo hasa pale palipo na uwezekano wa kujenga hoja na kupata haki husika, lakini inatia mashaka pale ambapo Serikali inatoa ufafanuzi mara baada ya mgomo kufanyika.

Tunaomba Serikali ijenge utamaduni wa kujadiliana na wanafunzi wanapokuwa na matatizo. Katika hili Wizara ingeweza kutoa muda na pesa, kutoa semina na ufafanuzi kwa jamii ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu kabla ya kuleta Muswada Bungeni. Hapa sizungumzii *Public Hearing* inayohusisha tu viongozi wa wanavyuo na walimu wachache kutoka kwenye Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, ninampongeza Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, jinsi ambavyo anakuwa mwepesi wa kusikiliza hoja bila hasira na kuzitafutia ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitazungumzia suala la Sayansi na Teknolojia. Huu ni mwaka wa nne, Kambi ya Upinzani ikiendelea kuishauri Serikali kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Sayansi na Teknolojia hasa katika kutoa pesa za kutosha katika utafiti na maendeleo au *Research and Development.* Lakini ushauri wote huu umekuwa ukiangukia kwenye masikio kiziwi.

Mheshimiwa Spika, imeelezwa kwenye Dira ya Taifa kuwa kufikia mwaka 2025, Tanzania itakuwa imejenga jamii iliyoelimika na ya kisasa katika matumizi ya Sayansi na Teknolojia, ili kuleta maendeleo ya haraka ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, nimewahi kujinukuu mara mbili,wakati nikitoa mawazo ya Kambi ya Upinzani hapa Bungeni katika bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na

Elimu ya Juu, nilisema hivi: " Lakini Kambi ya Upinzani ina wasiwasi na udhati, dhamira na uwezo wa Serikali yetu wa kuweka matendoni yale yote yaliyoainishwa katika Dira hii na hii inatokana na ufinyu wa fedha zinazotolewa kwa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu hasa fedha za utafiti na maendeleo, tafsiri finyu ya Wizara hii, kwa dhana ya kuiangalia katika muktadha wa Elimu ya Juu tu na leo naongeza jambo lingine ambalo ni ukosefu wa utashi wa kisiasa wa kutoa rasilimali na fedha za kutosha kwa ajili ya utafiti, sayansi na teknolojia".

Mheshimiwa Spika, tangu kuwepo kwa maarifa katika sayansi iwe sayansi ya jamii au asilia, kumekuwepo na kanuni za kufanyia kazi ili kutimiza malengo yaliyotarajiwa:-

(i) Katika nchi zilizoendelea, katika kupanga vipaumbele vya shughuli zao za kijamii na kiuchumi wanakuwa na kanuni ya kutumia ili kupanga bajeti zao. Huko Marekani, Ulaya, Japan, Uchina, India, wanazo kanuni za kujua kuwa katika Pato la Taifa ni asilimia ngapi itumike katika masuala ya utafiti na maendeleo. Mfano, hivi sasa inaeleweka wazi kuwa nchi zinazoendelea zinatoa 20% ya fedha zote zinazohusika katika utafiti na maendeleo na huku nchi zilizoendelea zikichangia 30% katika utafiti na maendeleo Duniani.

(ii) Kanda ya Amerika Kaskazini 37.7%, Kanda ya Ulaya 27.2%, Kanda ya Asia 30.5%, Kanda ya *Latin America/Carribean* 2.9% na Kanda ya Afrika 0.6%

(iii) Kwa kuzingatia idadi ya watafiti duniani, katika jumla ya watafiti duniani, nchi zinazoendelea zilichangia 28% na nchi zilizoendelea zilichangia 72% na hii ni kwa takwimu za mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, kanuni inayotumiwa na nchi nyingi ya kupanga fedha za utafiti na maendeleo, yaani *Gross Expenditure on Research and Development of the GDP,* yaani uwiano wa matumizi katika Utafiti na Maendeleo kutokana na Pato la Taifa, inatofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine. Lakini ushahidi uko wazi kuwa, kadri nchi inavyotoa pesa nyingi katika eneo la Utafiti na Maendeleo, ndivyo inavyopata mafanikio makubwa ya kisayansi, kiteknolojia, kiuchumi na kijamii.

Mfano, mwaka 1997, Pato la Taifa la China lilikuwa *$* 3.543 bilioni na ilikuwa imewekeza katika Utafiti na Maendeleo kiasi cha *$* 21 billioni, lakini ilipoongeza *$* 50 bilion, Pato la Taifa la China liliongezeka na kufikia *$* 5,029 bilion kwa mwaka 2000. Pamoja na mambo mengine yalichangia katika hilo. Hii inajionyesha pia katika nchi kama Japan, Marekani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa kwa sasa kiashiria kinachotumika sana sana katika kulinganisha Kimataifa na kuelezea Sera ya Sayansi na Teknolojia ni uwiano kati ya matumizi ya fedha za Utafiti na Maendeleo na Pato la Taifa. Hivi sasa nchi za Ulaya zimeamua kutumia mpaka asilimia tatu ya Pato la Taifa kwa ajili ya Utafiti na

Maendeleo. Israel inatumia asilimia nne nukta nne, Sweden inatumia asilimia tatu nukta nane, India imepanga kutumia asilimia mbili ifikapo mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Tanzania, ilipitisha katika Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia mwaka 1996 kutumia asilimia moja ya Pato la Taifa. Kitu cha ajabu ni kuwa, Serikali imetenga shilingi milioni 300 kwa ajili ya Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH)!*

Mheshimiwa Spika, Tanzania inazo Taasisi na vyombo mbalimbali vya kufanya utafiti wa kisayansi na kiteknolojia kama vile *Tanzania Industrial Research and Development Organization (TIRDO), Tanzania Engineering and Mechanical Design company(TEMDO), Tanzania Automotive Technology Centre (TACT), Technology Development and Transfer Centre (TDTC), Commission for Science and Technology (COSTECH)* na *Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology (CAMARTEC).*

Mheshimiwa Spika, nimekwishaeleza kuwa, Serikali imetoa shilingi milioni 300, kwa ajili ya Tume ya Sayansi na Teknolojia. Ushahidi uliotolewa tarehe 18 Julai, 2003 wakati wa semina ya Wabunge iliyotolewa na Taasisi *CAMARTEC*, pengine utathibitisha kilio cha Kambi ya Upinzani kuhusu kutotekelezwa kwa masuala ya Utafiti na Maendeleo katika Tanzania., kwani Wabunge tulielezwa kuwa trekta linalotumika pale *CAMARTEC* lina miaka 21 na gari linalotumika pale lina miaka 14 na ufinyu wa bajeti kwa Taasisi ya *CAMARTEC* na nyingine nyingi, nimeyasema haya kuhusu *CAMARTEC* ili kuvutia hisia za Waheshimiwa Wabunge, ili waone kuwa hii ndio picha halisi ya Taasisi zetu nyingi zinazojihusisha na masuala ya utafiti, sayansi na teknolojia,ili kuishauri na kuielekeza na kuiagiza Serikali hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, wakati, mfano wa *CAMARTEC* wanalalamika kwa kukosa magari ya kufanyia kazi za utafiti, Kamati moja ya Kudumu ya Bunge imelalamikia kitendo cha Idara moja ya Serikali kutenga shilingi milioni 80 kununua gari moja la Afisa mmoja wa Serikali katika Idara hiyo na Baraza la Mawaziri liliidhinisha hivyo, wakati huo huo Wananchi wakielezwa kuwa Serikali haina fedha za kuzipatia Taasisi za Utafiti, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linaloendana na hilo la fedha kwa ajili ya Taasisi za Sayansi,Teknolojia na Utafiti ni idadi na maslahi ya wanasayansi watafiti.

Tukitumia kigezo cha idadi ya watafiti kwa kila watu 1,000,000 kwa takwimu za mwaka 2000 katika nchi nyingine hali ni kama ifuatavyo:-

| **Nchi** | **Kila watu milioni moja** | **Idadi ya watafiti** |
|---|---|---|
| Japan | 1,000,000 | 5,206 |
| Marekani | 1,000,000 | 4,006 |
| Ulaya | 1,000,000 | 2,458 |
| China | 1,000,000 | 554 |
| Afrika ya Kusini | 1,000,000 | 309 |

| | | |
|---|---|---|
| Afrika | 1,000,000 | 78 |
| Afrika Chini ya Jangwa la Sahara | 1,000,000 | 51 |
| Tanzania | 1,000,000 | Haijulikani. |

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutokuwa na takwimu za wanasayansi watafiti kwa Tanzania, ni jambo la busara Serikali ikaanza kuweka sensa na takwimu ya wanasayansi wake watafiti, kwani kwa kufanya hivyo, kutasaidia kujua yafuatayo: Wako wanasayansi watafiti wangapi, mahitaji yao na idadi inayohitajika kwa ajili ya kuongeza.

Mheshimiwa Spika, katika hili wataalam au watafiti kumekuwepo na uhamiaji wa wataalam hawa kwenda nchi za nje, kama ambavyo hapa Tanzania, Serikali haina idadi ya wanasayansi wake, waliopo na waliohama, hata mimi sina idadi hiyo. Ila hoja hapa ni kuwa, wanahama kwenda kutafuta *Green Pasture.* Mfano, imekadiriwa kuwa kati ya asiimia 40 mpaka 60 ya wanasayansi watafiti wa nchi za Argentina, Chile, Colombia na Peru, walikuwa wamehamia na kufanya kazi katika nchi zenye viwanda. Lakini kinachosababisha hali hiyo ya kuhama kwa wataalam hao ni mishahara midogo kwa wataalam, mishahara midogo kwa wasaidizi wao, ukosefu wa vifaa na zana za kufanyia kazi pamoja na mazingira magumu ya kufanyia kazi zao.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na matatizo katika kuunganisha Taasisi au Vyuo vya Utafiti na wenye viwanda hapa Tanzania, uhaba wa fedha za kuzalisha kwa wingi zana zinazotokana na utafiti wa wagunduzi na wavumbuzi na Wananchi watumiaji kutopata taarifa za zana zilizozalishwa, zinazoweza kuwasaidia katika kurahisiha kazi zao na kuwaongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri kuwa kuhusu kuhuisha upya shughuli za Taasisi za Sayansi na Teknolojia, Serikali iunde Tume kufanya upembuzi yakinifu juu ya umuhimu na namna bora ya kupata vyanzo vya fedha kwa ajili ya kuzifufua Taasisi hizo, iangalie uwezekano wa kuziunganisha chini ya chombo kimoja taasisi zote za utafiti wa sayansi na teknolojia kuliko ilivyo sasa ambavyo ziko kwenye Wizara tofauti tofauti, Serikali itoe Waraka ni kwa kiasi gani kinachopaswa kutengwa kila bajeti kwa shughuli za utafiti na maendeleo na namna ya kuboresha maslahi na vifaa kwa watafiti.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haiwezi kuitenga Wizara ya Sayansi na Teknolojia ikabaki kuwa moja kama ambavyo tungeitenga kukawa na Wizara ya Elimu ya Juu, basi Serikali ifanye kama inavyofanya kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambavyo Jeshi la Magereza lina Kasma yake, hivyo, Idara ya Sayansi na Teknolojia iwe na Kasma yake na nusu ya Bajeti ya Wizara hii iende kwa Idara hiyo ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kufuatia Sera yake ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 ya kutenga asilimia moja ya Pato la Taifa kwa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, basi ilete Muswada wa sheria ili kufanikisha utekelezwaji wa Sera hiyo. Kwa mfano, mwaka huu kama sheria hiyo ya kutenga asilimia moja ya Pato la Taifa ingekuwa inatumika, Idara ya Sayansi na Teknolojia ingeweza kupata shilingi bilioni 90

bila ya kuweka fedha zinazokwenda kwenye Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu. Hivi sasa Mheshimiwa Waziri, kwa ujumla wa Wizara yake yote anaomba shilingi bilioni 84, kiasi ambacho ni tofauti na ambavyo sera inasema kwamba, kwa Utafiti na Sayansi ingetengwa asilimia moja ya Pato la Taifa ambazo ni shilingi bilioni 90.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa tukumbuke kuwa changamoto nyingi zinazotukabili sisi Watanzania katika maeneo ya maendeleo, uchumi, afya, elimu na kilimo endelevu, haya yote yanaweza kuwekwa katika kiwango kimoja kwamba, jamii iliyoelimika na kutumia uchumi unaotumia ujuzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. REMIDIUS EDINGTON KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, na mimi napenda kuungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, pamoja Naibu wake na Watendaji Wakuu wa Vyuo mbalimbali vilivyo katika Wizara hii, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kuinua elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kutoa salamu za rambi rambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mungu aipe familia yake na wapiga kura wake subira. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa kuhusu Wizara hii na kwa kweli wanajitahidi kufanya kazi nzuri na inaonekana. Mimi nitapenda kuchangia mawili, matatu, ili kuiboresha.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa ni umuhimu wa kuwatumia hawa wataalam wetu. Sasa hivi Vyuo vyetu Vikuu vina wataalam wengi waliobobea katika fani mbalimbali. Wito wangu mimi ni kuwa, Asasi zote za Serikali na zisizo za Serikali, zijitahidi kuwatumia wataalam hawa katika kufanya utafiti na kuwafanyia mipango yao ya maendeleo na hasa mipango endelevu kama *Strategic Plans* za Asasi zao. Hizi Asasi zikiwa na *Strategic Plans* inakuwa ni rahisi kupima maendeleo yao kila wakati. Kwa sababu kuna vigezo maalum vya kutumia na unaona ile *development trend* inavyotokea. Kwa hiyo, wawatumie sana wataalam wetu watafiti wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, *Marine Science, SUA* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la *Research and Development. Research and Development* katika nchi yoyote na hasa kwa nchi zetu changa hizi za Afrika na nchi nyingine zinazoendelea ni muhimu sana. Sasa hivi sisi ni watumiaji zaidi wa teknoloja za wenzetu na zinatupa tabu kwa sababu zimeendelea mno, sisi kazi yetu ni ku-*catch up*. Ni vizuri tuangalie zile teknolojia ambazo sisi tunaweza kuzimudu na ni nafuu. Sasa hizi hatuwezi kuzipata kama hatufanyi tafiti zetu wenyewe katika mazingira yetu ya Kitanzania, Kiafrika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa ninakuja kwenye suala lile lile ambalo wenzangu wameshalizungumzia sana, nalo ni kuhusu bajeti. Bajeti si kubwa kwenye *Research and Development.* Mimi ninasisitiza Serikali ijitahidi sana kuhakikisha angalau lile lengo iliyojiwekea la asilimia moja katika Pato la Taifa linapelekwa katika Utafiti na Maendeleo. Hii itasaidia sana kuendeleza elimu, lakini vilevile itatusaidia kupata teknolojia ambayo ni endelevu kwa nchi zetu. Natoa ushauri kwa Vyuo Vikuu kuendeleza majadiliano na mashirikiano baina ya Vyuo vyetu katika Afrika Mashariki, katika *SADC* na katika mpango mpya huu wa *NEPAD* wa Afrika nzima ili kuunganisha nguvu tusiwe tunarudia yale kwa yale. Mazingira ya nchi zetu katika Afrika na hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara yanafanana sana. Sasa pengine utafiti unaofanywa Kenya, Msumbiji, Kongo, ukawa unajirudia rudia. Sasa ni muhimu kuwepo na maendeleo na hii itapatikana kama kutakuwa na *joint effort* ya Vyuo Vikuu vyetu kujua nini kinachofanyika na kwa wakati gani.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la mishahara. Hali ni gumu lakini jitihada za makusudi lazima zifanywe kuhakikisha kwamba, wataalamu wetu wa ngazi mbalimbali wanainufaisha nchi yetu. Tumetumia fedha nyingi kuwasomesha sasa si haki wala halali kwa wataalam hawa baada ya kutumia fedha zetu chache na za nchi maskini kama yetu halafu wanaenda kufanya kazi katika nchi zilizoendelea.

Hawa watu tunawahitaji hapa na lazima tuweke vishawishi vya kuwavutia. Kwa hiyo, ni muhimu mazingira yenyewe ya kufanyia utafiti na kuendeleza elimu yawe ni ya kuvutia. Kwa hiyo, natoa wito kwa Serikali kuongeza mishahara na marupurupu kwa wakufunzi wa Vyuo Vyetu Vikuu na Taasisi mbalimbali za Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao wameonyesha moyo wa uzalendo, basi viongozi wahakikishe kwamba, wanalipwa posho zao. Hawa walimu ni watu ambao wanajitolea na wafanya kazi nzuri sana na ya kuendeleza Wananchi wetu, kwa hiyo, zile stahili zao wazipate kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

La mwisho, ambalo ningependa kuchangia ni suala la kuendeleza Taasisi ya *Marine Science* ambayo ilishapata eneo la Buyu kule Zanzibar ambayo ipo Wilaya ya Magharibi. Namwomba tu Mheshimiwa Waziri, kuna baadhi ya watu hawajapata mafao yao basi aimalizie kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni kuwa hiki Chuo, *Original Plan* yake ilikuwa ni kukifanya kiwe Chuo Kikuu cha Sayansi za Baharini, sasa nchi yetu imezungukwa na maji mengi. Tuna Maziwa mengi, tuna mito lakini vilevile nchi yetu ina bahati ya kuwa na Bahari ya Hindi ambayo inasaidia hizi nchi ambazo hazina bahari. Kwa hiyo, tuitumie hiyo bahati tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, kufanya utafiti wa kina katika masuala haya ya tafiti za baharini ili tuwe viongozi kwa wenzetu na hii itasaidia zaidi kuongeza tija kwa wavuvi wetu na hasa wadogo wadogo. Lakini vilevile kuongeza pato la nchi.

Mheshimiwa Spika, hivyo natoa wito kwa Serikali kuendelea na azma yake ya kufanya hii Taasisi ya Sayansi za Baharini iwe Chuo Kikuu kitakachoshughulikia

masuala yote ya utafiti katika Sayansi za Baharini pamoja na viumbe hai hasa uvuvi wa samaki, pweza na kadhalika. Lakini vilevile kuendeleza rasilimali, kuna rasilimali nyingi sana ndani ya bahari ambazo wataalam wanasema kuna viumbe hai wengi kuliko hata sisi wa nchi kavu. Sasa pengine vinaweza vikatusaidia sana katika maendeleo yetu ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja hii, lakini bado jitihada ziongezwe ili bajeti iongezeke mwakani (2005/2006). Hivi Vyuo Vikuu ambavyo tunatarajia viongezeke katika nchi hii vinahitaji rasilimali, lazima tukubali kwamba, tunawekeza katika rasilimali-watu na watu ndiyo watakaoendeleza nchi hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ili nichangie hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijafanya hivyo, nitoe pole kwa misiba mbalimbali iliyotokea. Nimpe pole Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, kwa kufiwa na mtoto wake mpendwa na niwape pole familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyetutoka hivi karibuni. Naomba Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza kabisa, kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Waziri wa Wizara hii, ambaye tunajadili hoja yake pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu, Bibi Ruth Mollel na Wataalam wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiendelea kuifanya katika mazingira magumu. Nawapongeza sana kwa kazi yao nzuri, naamini kwa bajeti hii waliyoitoa leo, wataendelea kufanya kazi nzuri kwa kipindi cha mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama walivyotangulia kuzungumza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati na Waziri Kivuli au Waziri anayesubiri pamoja na mchangiaji aliyetangulia, wameunga hoja hii mkono na wamefanya uchambuzi wa kina na wote wameonesha kwamba, kwa kweli kazi yetu kubwa ni kuunga mkono hoja hii ambayo imetolewa kwa umahiri mkubwa. Kwa hiyo na mimi nataka kuungana nao, kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu nitauelekeza katika maeneo machache tu. Nitauelekeza mchango wangu katika mfumo wa utoaji elimu yenyewe (Elimu ya Juu), ujuzi na uzoefu wa walimu wa Vyuo Vikuu, pamoja na utafiti katika Vyuo Vikuu ndipo nitaelekeza nguvu zangu katika mchango ninaoutoa.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa utoaji elimu ya Chuo Kikuu wote tunafahamu kwamba, Chuo Kikuu kinaweza kikalinganishwa na kiwanda. Kiwanda kinayo tabia moja. Tabia ya kiwanda ni kuzalisha bidhaa na kinazalisha bidhaa mbalimbali.

Sasa kwa upande wa Chuo Kikuu, bidhaa zake kubwa ni wahitimu katika fani mbalimbali, katika fani za Biashara, fani za Uhandisi, fani za Kilimo na Mifugo, Sheria, Ualimu na kadhalika. Sasa kwa kuwa Chuo Kikuu ni kiwanda ni lazima kizalishe bidhaa ambazo zina mvuto katika soko.

Mheshimiwa Spika, bidhaa zinazozalishwa lazima zikamilike. Bidhaa hazitakiwi kuwa nusunusu. Sasa ili bidhaa ziwe na mvuto kwa mteja lazima ziwe na ubora wa hali ya juu na zipatikane kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, huwezi ukakaa ukasema eti bidhaa tunazozalisha hapa ni za Kitanzania , Tanzania haiwezekani. Soko letu sasa limebadilika. Soko letu sasa ni dunia nzima. Soko ni dunia nzima kwa sababu ya utandawazi ambao tunao sasa na hatuwezi kuukwepa. Kwa hiyo, lazima bidhaa inayozalishwa iwe na ubora wa Kimataifa ili iweze kuhimili kabisa ushindani wa soko la Kimataifa. Sasa elimu kama bidhaa nyingine haina budi kutolewa katika kiwango cha ubora wa hali ya juu na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, elimu ya Chuo Kikuu haina budi kuwa na ubora wa Kimataifa na sio Kitanzania Tanzania. Nataka niwapongeze sana vyuo vikuu vyetu kwa kutoa elimu inayolingana na elimu ya Kimataifa. Kwa hiyo, napenda kutoa rai zaidi kwamba elimu yetu itolewe kwa ubora unaohimili ushindani katika soko la ajira la Kimataifa. Kwa hiyo, elimu hii lazima itolewe kwa gharama nafuu kwa sababu wanunuzi wa bidhaa duniani kote wana tabia moja wanapendelea kununua bidhaa kwa bei nafuu, lakini bidhaa iliyo bora. Kwa hiyo, basi elimu ya Chuo Kikuu ili kukidhi mahitaji ya soko haina budi kuwa na mwelekeo ufuatao.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa kwanza kabisa ni kuzalisha au kutoa wanafunzi au wahitimu ambao wana mwelekeo wa soko. Wawe na mvuto na wawe *demand driven.* Lazima elimu inayotolewa na Chuo Kikuu ilenge katika mahitaji ya wateja wenyewe kwa maana ya kuelekea kwenye kujitegemea kwa sababu ndio mfumo tulionao sasa. Kwa maana ya kupata ujuzi zaidi na kuwajengea uzoefu kwa maana ya kufanya kazi kwa vitendo zaidi kuliko nadharia ndani ya ufundishaji wetu. Elimu yetu inayotolewa lazima iweze kulenga katika kupata ajira katika soko la ushindani. Sio ajira hivi hivi tu, lazima iwe ajira katika soko la ushindani. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba elimu yetu lazima ilenge katika ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, elimu yetu iwe na mwelekeo wa kibiashara hata kama ikiwa elimu ya kisayansi ni lazima elimu yetu itoe angalau ufahamu wa kibiashara. Kwa sababu wahitimu wetu wa hivi sasa kwenye fani hasa za sayansi wanaweza wakahitimu wakiwa wanasayansi wazuri lakini wakashindwa kujitegemea kwa sababu hawana elimu ya ujasiriamali wala ufahamu wa biashara. Kwa hiyo, ili mwelekeo wa elimu yetu uwe *demand driven* lazima uwe na mwelekeo wa soko. Napendekeza basi elimu ya vitendo kwenye vyuo vyetu vyote ichukue nafasi kubwa zaidi kuliko elimu ya nadharia.

Mheshimiwa Spika, pili ni juu ya ujuzi, uzoefu na maslahi ya Walimu ama Wahadhiri. Ili vyuo vyetu viweze kutoa elimu inayolenga soko la ndani mfumo wetu na utaratibu wa ajira za Walimu wa Vyuo Vikuu hauna budi kutazamwa upya. *(Makofi)*

Hivi sasa kikawaida Walimu wetu tunawapata kutokana na wanafunzi wanaohitimu. Wale wanaofanya vizuri sana *automatically* wanakuwa Walimu wanapanda ngazi kidogo kidogo mpaka wanafikia ngazi ya u-profesa. Sasa kwa hali hii hawapati uzoefu wa kutosha katika kutenda kazi kwenye viwanda ama kwenye mashamba ama kwenye ofisi zetu za Serikali.

Kwa hiyo, uzoefu wanaoupata ni kupitia utafiti wanaoufanya katika maeneo haya. Sasa nadhani ni wakati mzuri wa kuangalia hali ya soko ili tuwe na Walimu bora zaidi wanaolenga kufundisha kuelekea soko. Walimu wetu wapate pia ujuzi, wapate nafasi ya kufanya kazi kidogo kusudi wajifunze mbinu mbalimbali za kufanyia kazi katika viwanda, mashamba na katika maofisi yetu ya Serikali na kadhalika. Badala ya kuwaacha wapande ngazi peke yake ya kuwa Mwalimu.

Mheshimiwa Spika, upandaji wa ngazi wa Walimu usiangalie kuandika makala peke yake na kufundisha. Maana ndio inayoangaliwa zaidi. Sasa ili Walimu wetu waweze kupanda ngazi kwa mashindano upandaji ngazi pamoja na kuangalia uandikaji wa makala yanayotokana na utafiti tuangalie vile vile ubunifu wao katika kuangalia ni nini sasa kinatakiwa sokoni. Ubunifu wao uwe ni njia mojawapo ya kuwapandisha katika ngazi zao za kitaalamu. Nashauri vile vile Walimu watumie zaidi makala au *case studies* katika ufundishaji wao. *Case studies* hai za kuangalia hali ya kiwanda fulani, kuangalia hali ya ofisi fulani, shamba fulani na kufuatana na hali ya mahali hapo kuandaa *case study* ambayo itawasaidia wanafunzi kupata uelewa katika kujifunza.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni juu ya utafiti katika Vyuo Vikuu. Nawapongeza sana kwamba uko utafiti mwingi umefanyika. Utafiti unaofanywa na wanafunzi na Walimu na uko utafiti unaofanywa na wengine katika fani mbalimbali. Utafiti umefanywa sana lakini mazingira yanayofanyiwa utafiti ni mazingira duni mno. Kwa mfano jana tulikuwa tukitazama mashine mbalimbali zinazotengenezwa *SIDO* pamoja na Mashirika yanayofanana.

Sasa ukizitazama mashine hizi ni kweli zimefanyiwa utafiti mzuri sana. Lakini ubora wake ni wa chini mno ukilinganisha na ubora wa bidhaa za jirani zetu. Kwa hiyo, ndiyo maana hatuwezi tukashindana vya kutosha katika soko la bidhaa za namna hiyo. Japokuwa zimefanyiwa utafiti mzuri na zinaweza kutoa matokeo yanayotakiwa, lakini ukiziweka sokoni mvuto wake si mzuri kama mvuto wa bidhaa za wenzetu.

Kwa hiyo, ili tuweze kuwa na utafiti mzuri sana tunaiomba Serikali iweke mkazo na kuongeza bajeti kusudi utafiti wetu ufanane na hali halisi ya soko tulilonalo. Utafiti wetu lazima sasa uwe unalenga kwenye matumizi ya moja kwa moja. Lakini haitoshi kufanya utafiti. Nimeona utafiti mwingi unaofanyika watafiti wale wale wanakuwa wazalishaji wa bidhaa ile. Hii haitatupa maendeleo ya haraka kwa sababu mtafiti kila siku anataka kugundua au kuvumbua kitu kipya. Kwa hiyo, ukimwambia aanze

kuzalisha kile kitu alichokwishavumbua sio *challenge* kwake tena anataka *a new challenge.*

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza, najua mmeanza, lakini napendekeza iwe sasa ni dhahiri kwamba watafiti kazi yao iwe ni kutengeneza *prototype.* Mkishatengeneza *prototype* sasa *prototype* ile iende kwa wazalishali. *Prototype* naambiwa chasili. Chasili ikishatengenezwa sasa watafutwe watengenezaji viwandani ambao wataitengeneza bidhaa hiyo kwa gharama nafuu kwa maana watatengeneza bidhaa nyingi zaidi ambazo bei yake kwa kitu kimoja yaani kwa *unit cost* itapungua. Hii itatusaidia sana katika kuhakikisha kwamba tunaeneza bidhaa iliyo bora na ya bei nafuu kwa wananchi wetu na kisha bidhaa hii itashindana na bidhaa za wenzetu jirani au zinazotoka nchi nyingine za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napendekeza kwamba utafiti wa msingi ambao unafanyika sasa uwe ni utafiti lenga ambao unalenga kutatua matatizo na kuingia kwenye soko la mashindano. Utafiti wenye mvuto wa bidhaa itakayozalishwa. Utafiti unaofanywa uwe ni utafiti mtiririko, utafiti ambao utaangalia matakwa ya wahitaji au watumiaji wa bidhaa inayotarajiwa. Kwa hiyo, utafiti wetu utazame aina ya mafunzo yanayohitajika yatokane na utafiti unaofanywa yaende kwenye uzalishaji na hatimaye bidhaa imfikie mtumiaji ikiwa na ubora wa hali ya juu ikiwa ya bei nafuu. Mwisho kabisa utaratibu wa utafiti uwepo uratibu katika tafiti zetu baina ya vyuo vikuu pamoja na taasisi nyingine za kilimo.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo kwa siku ya leo. Kabla sijakwenda mbali natoa pongezi kwa Mheshimiwa Dr. Pius Ng’wandu, Waziri wetu wa Wizara hii. Kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Mawaziri wa Elimu katika Bara la Afrika katika kipindi nadhani cha miaka minne ijayo. Hii inaendelea kuonyesha pamoja na wengine wengi waliochaguliwa hasa mwaka huu kwamba nchi yetu kwa kweli ina wataalamu au wajuzi wa masuala mbalimbali. *(Makofi)*

Pamoja na yeye kwa sababu anaongoza Wizara hii niendelee kumpongeza kwa kuongoza Wizara pamoja na Naibu Waziri wake Zabein Mhita, Katibu Mkuu, Bibi Ruth Mollel, Wakurugenzi, Wakuu wa Vyuo na Taasisi mbalimbali na watendaji wote wa Wizara hii kwa kutuandalia hotuba nzuri, yenye kueleweka na inayotoa mwelekeo wa matumaini ya kutekeleza malengo yao pamoja na kwamba kilio ni kile kile fedha hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi pia kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sio kwamba wengine hawafanyi vizuri lakini sio kwa ajili ya maonyesho walioshinda wiki iliyopita hapana. Mimi ninawapongeza sana kwa sababu kwa kiasi kikubwa wamejitahidi kutekeleza kila kilicho chini ya uwezo wao kuhakikisha kwamba wanachuo wenye ulemavu wanawezeshwa katika chuo kile kupata elimu yao angalau kwa urahisi zaidi kwa kupatiwa nyenzo za kujimudu.

Mheshimiwa Spika, chuo hiki kinaimarisha kitengo cha huduma za wanachuo wenye ulemavu, chuo hiki kimerekebisha mazingira ya sehemu kadhaa kadhaa ya chuo ili yaweze kuwa muafaka kwa kukidhi mahitaji ya wanachuo hawa. Kwa kweli nawashukuru sana na nawapongeza. Kwa sababu haya sikuambiwa niliyaona mwenyewe wanachuo hawa waliponialika mwaka jana kwenye sherehe yao ya mahafali, kuagana na kupongezana wanaoingia wakiwa wenye ulemavu. Walinieleza haya na niliwaona hata wanaohusika katika kitengo hiki. Ninawashukuru muendelee na hayo.

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba hapo ni kwamba basi vyuo vingine ambavyo vinatoa kozi za aina ambazo watu wenye ulemavu wanaweza wakazimudu waige mfano huo kwa sababu naamini watu hao wenye ulemavu katika nchi yetu hii baadaye wanaweza wakawa wengi tu wakajiungaunga. Kwa hiyo, vyuo vingine pia viweke provisions kwa sababu kama nilivyosema ninaamini katika maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari miaka ijayo si ajabu wanachuo wengi wenye ulemavu wakaweza kujiunga katika vyuo vyetu vya umma na hata vya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo ninaendeleza kwamba Serikali ione uwezekano wa kusaidia vyuo vikuu angalau kimoja kiweze kutenga nafasi za wanafunzi viziwi kuweza kumudu masomo ya Chuo Kikuu. Kwa utafiti wangu mdogo viziwi wamebarikiwa na kipaji cha hesabu na *computer sciences.* Wakitulia kuangalia tu na ku-*concentrate* pamoja na kwamba hawasikii masomo haya wanayamudu kweli. Mifano hai ninayo. Kwa hiyo, basi hawana nafasi ku-*attend* masomo ya vyuo vikuu katika vyuo vyetu kwa sababu hakuna kilichoandaliwa kwa ajili yao. Mazingira yao ni magumu kwa hiyo naomba katika vyuo vyetu vilivyopo basi kuanzia na cha Serikali kimojawapo kiweze kuteuliwa kuweka hizo *provisions* kusudi na hawa waweze kusoma humu humu kama wenzao. Kwa sasa hivi kwa mfano wanaweza wakapata mikopo, hiyo imeshatatuliwa. Kwa hiyo, nina imani kwamba wataweza kumudu masomo haya ili mradi tu hayo mengine yaweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka jana Chuo Kikuu Huria kilitoa maelezo kwamba wana nia ya kuongeza matumizi ya kompyuta katika chuo kile ili kuweza kuendeleza au kupanua mawasiliano na mambo kama hayo. Katika kuchangia hilo mimi nilitoa rai kwamba chuo basi kihakikishe kwamba kinapata kompyuta angalau chache zinazoweza kutumika na wanachuo wasioona na hata katika bajeti hii wanasema wataongeza idadi ya wanachuo wasioona na kutengeneza moduli za kutosha. Hilo mimi nalichangia. Sasa hapa ninalotaka kujua ni kwa kiasi gani rai hiyo iliweza kufanyiwa kazi. Ningefurahi sana kufahamu kwamba utekelezaji umekuwajekuwaje na kama imeshindikana basi sababu zake ni nini tuweze kushauriana baadaye nini cha kuweza kufanya.

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu walivyotangulia ninaomba kabisa na nakubaliana kilichosemwa na Kamati kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo husika kuhusu utengaji wa fedha za kutosha katika mfuko wa kuendeleza sayansi na teknolojia. Kamati imesisitiza kabisa kwamba hili kama halifanyiki bwana itabidi hata tulete hoja binafsi. Lakini kwa nini tufikie katika hali hiyo. Niendelee tu kusisitiza

kwamba kwa kweli kama nilivyosema jana ni dhamira tu na kujifunga mkanda ndiko ambako kunahitajika kuweza kusaidia Wizara hii na taasisi zake ziweze kufanya tafiti zinazowezekana na tafiti hizo matokeo yake kuweza kusambazwa kwa wananchi kusudi wananchi hao waweze kutumia matokeo ya tafiti hizo. Kwa hiyo, nasisitiza tu kwamba ni muhimu kwa kweli fedha ziweze kutengwa.

Kwa mfano jana hapa hapa kama *CAMARTEC* ililalamika kwamba fedha za utafiti hakuna kama wenzangu walivyotangulia kusema. Sasa mfuko kama huu kama tungeutunisha kwa kupata fedha za kutosha basi taasisi kama hizi ambazo zinaendelea na tafiti mbalimbali zingeweza kuwezeshwa hivyo kuweza kufika mahali panapoeleweka.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Wizara kwa kutoa miongozo ndani ya vyuo vyake na taasisi zake ya jinsi ya kuongeza idadi ya wanachuo wanawake. Wao ndio wanaotoa. Niipongeze kwamba vyuo kimoja kimoja kwa uwezo wake vimejaribu kutekeleza maagizo haya kwa sababu hata hotuba imetueleza hapa kwamba kumekuwa na maendeleo mwaka hadi mwaka wa wanachuo akinamama kuweza kujiunga kwenye vyuo vyetu katika kozi mbalimbali. Hilo nalipongeza kwa sababu tusisahau usemi wa wahenga ambao unasisitiza siku zote, “Ukimwelimisha mwanamke umekwishaelimisha jamii kwa ujumla wake.” Kwa hiyo, nishukuru kwamba Serikali ina lengo hilo na limeona umuhimu huo kwamba sasa akinamama katika kozi mbalimbali kwa kweli wanajitahidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara katika kuendeleza elimu ya juu naomba tu kuuliza kuna mikakati gani inayoandaliwa ili kukidhi haja ya wanafunzi wanaoongezeka na watakaoongezeka miaka miwili ijayo kutokana na maendeleo ya elimu upande wa MMEM na MMES?

Ni vyema mipango hiyo iwe thabiti vinginevyo mafuriko yatakayotokea ya wanachuo wengi kujiunga halafu hatuna nafasi nao kwa kweli itakuwa ni vibaya sana. Itakuwa ni vibaya sana kwa sababu kwa sasa hivi malalamiko tayari yameshatokea wanaoweza kujiunga ni wachache, sasa je tunajiandaa vipi? Hilo ningependa kulifahamu likae wazi ili kama uhamasishaji basi tukaendelee kuufanya huko tunaporudi majimboni kwetu.

Mheshimiwa Spika, niungane na mzungumzaji aliyenitangulia kuhusu umuhimu wa vyuo vyetu kuingiza somo la ujasiriamali. Kwa somo hilo na dozi ndogo hiyo watakayochukua waweze kuondoka pale wakiwa na ujuzi kiasi fulani wa kuweza kwenda kujiajiri wenyewe kwa sababu ajira rasmi sasa hivi hakuna ni chache sana katika Wizara nafasi ni *fields* chache sana. Kwa hiyo, waondoke na hilo waweze kwenda kujiajiri na kwa wale ambao watapata mikopo iwasaidie kuweza kurejesha mikopo hiyo kwa wakati unaotakiwa baada ya kujiajiri kutokana na taaluma ambazo watakuwa wamezipata.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kuungana pia na wenzangu kuhimiza Serikali kutoa motisha ya kutosha. *Package* ya aina aina, wataalamu wa mambo ya kazi wapo, kwa watafiti na wavumbuzi wetu. Kwa sababu kama iliyosemwa hawa tusipowalea wanahama. Sina uhakika katika kuendelea kufanya kazi sehemu za nje Serikali inapata

chochote sijui. Lakini Serikali imetumia fedha zake kuelimisha wananchi hawa ili angalau kwa nia watumike humu humu ndani.

Lakini tunaposhindwa kuwalea kwa kutowapa mahitaji muhimu na motisha inayoeleweka watakwenda nje na sisi badala yake kuajiri wananchi kutoka nje kuja kuhudumia. Sasa tunafanya nini? Tunao tunaowaelimisha wanatoka halafu tunawachukua wa nje kwa gharama kubwa kutusaidia.

Tunao ma-*consulants* wengi tu ambao wana ujuzi. Kwa hiyo, ninaomba kabisa hilo liweze kuzingatiwa kama sio kwa bajeti hii sijui katika *section* ya Utumishi kumewekwa nini huko sina uhakika. Kwa hiyo, nipendekeze kwamba kwa kweli sekta hiyo tuweze kuiboresha kusudi waweze kutoa taaluma na yale waliyonayo humu humu nchini kwa sababu ni nchi ambayo imeweza kuwagharamia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya kwa kweli Wizara na mimi na kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati, mengi walitufafanulia.

Lakini mengine haya nimeona niyasemeseme kwa nia tu ya kuweza kusisitiza na kuimarisha na kuwasaidia nini cha kuweza kufanya kusudi mwakani tuweze kukuta mabadiliko kidogo ya mambo mengine ambayo yameweza kutekelezeka bila gharama. Baada ya mchango huu naunga mkono hoja na nawatakia kila la kheri katika utekelezaji mwema pamoja na fedha kidogo walizo nazo. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara hii muhimu kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii. Nataka nitamke wazi kwamba naiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara tunayoijadili leo ndio mhimili mkuu wa Taifa letu la Tanzania. Kwa sababu tunategemea elimu ya juu ambayo tutakwenda kwenye uchumi moja kwa moja tukijumlisha pamoja na viwanda. Kwa hivyo nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa mafanikio makubwa ambao kwa muda tangu aliokamata Wizara hii ambayo sisi wengine tunaifuatilia na tumebahatika kuichangia tumekuta mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio hayo nataka niitumie nafasi hii niwaombe wataalamu wetu na wasomi nchini washirikiane na Wizara yetu na Taifa letu kuleta mabadiliko makubwa katika Taifa letu. Kama wataalamu duniani wanavyozungumza wachumi kwamba sayansi na teknolojia ndio msingi mkuu wa uchumi wa nchi tele duniani. Kwa hivyo majukumu ya Wizara hii yanajilenga hapo, kwa hivyo sayansi inaweza ika-*deal* kwenye maeneo yake ya teknolojia kwenye viwanda. Wakati mwingine hata kilimo kitaongezeka kwa mafanikio makubwa sana. Kwa hivyo, Mheshimiwa Waziri nataka nirudie kwa kuunga mkono na nakupongeza kwa asilimia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu na kwa kweli nataka nimshukuru Mheshimiwa Waziri kama alivyosema kwenye hotuba yake. Kwa sababu ametueleza waliyotekeleza na ambayo wanategemea kuyatekeleza. Kwa hivyo, imenipa matumaini kwamba niwaunge mkono. Kwa hivyo, Mheshimiwa Waziri yale ambayo uliyoyaona hayakuweza kufanikiwa kutekelezeka kwenye kipindi kilichopita, kwenye kipindi hiki uhakikishe umeyafanyia mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lingine nataka niitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri mgogoro wa Chuo Kikuu uliutuliza kwa hekima kubwa sana. Kwa kweli wale vijana wetu hawakutaka kutuelewa ule Muswada tulioupitisha kwa mafanikio makubwa. Sisi ubunge wetu una mwisho na hatukusita kuwakomboa. Lakini kama nilivyozungumza kwa kweli tuwatake Viongozi wenzetu wa Vyama vya Siasa wasiwatumie wale vijana waache wasome. Wawaache wasome tunategemea mabadiliko ya uchumi wa Taifa letu, maendeleo ya Taifa letu kutokana na vijana hawa ambao sasa hivi wako vyuoni. Vile vile nataka niwapongeze baadhi ya wanafunzi wa vyuo maalum niliwakuta sijui kutoka Iringa na kadhalika walielezwa ukweli wa Muswada ule umuhimu wake. Kwa kweli wale walisaidia sana kama Watanzania kwa hivyo vile vile nataka niwape pongezi Mheshimiwa Waziri kwa kweli kazi kubwa umeifanya na tunataka vijana wale waendelee na masomo yao ili kuleta maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi katika kumwunga mkono Mheshimiwa Waziri nataka niende ukurasa wa 8 ambao amezungumzia mamlaka muhimu Tanzania. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwamba hotuba yake ime-*cover* maeneo yote na hakuna alichokibakisha. Katika eneo hili nikilinukuu hotuba yake inasema: "Katika mwaka wa fedha ya 2003/2004 Mamlaka ya elimu ilitekeleza yafuatayo". Yapo manane, lakini mimi nitanukuu moja. Ilisema kwamba Mamlaka ya elimu iliwekeana mkataba wa maelewano *(MOU)* na Mfuko wa Elimu wa Juu Zanzibar kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa mfuko wa elimu kwa upande wa Zanzibar. Hivi mimi naomba niulize, tangu mwaka 1964 ndio mmeweka juzi au kuna mabadiliko tu kumeongezeka kitu.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar ni sehemu ya Tanzania. Ni lazima twende kama Taifa moja. Huku mbele ya safari nitamnukuu Rais wetu Mkapa alipoielezea nini Tanzania. Lakini ningeiomba Serikali ione umuhimu wa kuipatia uwezo Zanzibar kifedha si kuisaidia. Tunataka kujenga uchumi wa Taifa la Tanzania ambalo linajumuisha Zanzibar ni sehemu ya Tanzania. Hapa Mheshimiwa Waziri kidogo nimeshtuka kwamba tangu mwaka 1964 kama ninyi makubaliano hayo mmeweka juzi mwaka 2003/2004. Kwa hivyo, tuangalie marekebisho yasitokee matatizo kama haya. Hii ni Wizara muhimu basi tunaitegemea.

Mheshimiwa Spika, vile vile nikiendelea katika sehemu hii hii imeelezea kuhusu mwaka huu wa 2004 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unasema kwamba kinatarajia kutekeleza haya yafuatayo. Kuendeleza sehemu iliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya Taasisi ya Sayansi ya Baharini. Naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania isiende kwa eneo hili tu. Suala la elimu liingie Zanzibar nzima ikiwemo pamoja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri wewe umetembelea Pemba na ninapenda nikupongeze sana. Ulifika Chuo cha Fidel Castro na pale ukatoa somo la Elimu ya Uraia, uliona vijana walivyokupokea. Pia, ulifika Shule ya Sekondari ya Utaani pale Wete ukaona vijana walivyokuuliza hata lile swali wakitaka kujua ile faini ya Shilingi milioni 5 kwa nini ilifutwa na ukawapa maelezo mazuri hivyo na wakaridhika.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nimefarijika yeye mwenyewe Mheshimiwa Pius Ng'wandu amefika Pemba akiwa ni Profesa. Pia, Mheshimiwa Mark Mwandosya, akiwa ni Profesa amefika Pemba na Mheshimiwa Waziri Mkuu amefika Pemba. Hebu tuambieni kuna sababu gani Pemba kusiwe na Chuo Kikuu? Kama Maprofesa wawili hawa wamekwenda kuweka ishara ya mnara na ukiwemo wewe Spika naamini si mwepesi, akiwemo Waziri Mkuu, kwa nini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haiipi fedha Zanzibar kwa ajili ya kufungua Chuo Kikuu Pemba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Pemba wanahitaji Elimu ya Juu kuwapunguzia masafa ya kuja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo unakutana na migogoro kama yale maandamano ya juzi ambayo kwa sasa hivi sisi yamekuwa ni funzo kwenye ile Januari 2001, tunayaogopa na hatutaki yatokee tena na tukiwaona wenzetu hawa wa *CUF* tunawaambia ukweli, hatuwafichi kwamba lile jambo lisitokee tena kwa sababu sote tuko hapa kwa faida yetu, kwa faida ya Majimbo yetu, kwa faida ya Pemba, kwa faida ya Zanzibar na kwa faida ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini ukienda kule sasa hivi utakuta mabadiliko makubwa. Wabunge wa Upinzani waliopo kule sasa hivi na wale Wabunge waliokuwepo mwaka 1995 tunazungumza nao vizuri, panapotokea makosa tunaelekezana kwamba tuko hapa kwa faida ya Taifa hili na watu wetu ambao wametutuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumza nikimnukuu Mheshimiwa Rais Mkapa katika hotuba yake ya tarehe 26 mwezi wa Aprili mwaka huu 2004 katika kuadhimisha Muungano wetu wa Tanzania na wewe mwenyewe Spika ulikuwa pale Uwanja wa Amani Zanzibar. Nataka ninukuu maeneo matatu katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais Mkapa. Katika ukurasa wa 20 Mheshimiwa Rais alisema kwamba: "Muungano wetu wa 1964 haukuasisi umoja wetu, ulirejesha tu umoja wetu. Ni vema vijana wetu wajue jambo hili na kulizingatia." *(Makofi)*

Sehemu ya pili alisema: "Niliapa kulinda Katiba ya Nchi, Katiba isemayo wazi kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Taifa moja huru lenye muundo wa Serikali mbili." Lakini sehemu ya tatu katika ukurasa wa 28, Mheshimiwa Rais anasema kwamba: "Ninawajibika kwa dhati kuutetea na kuulinda Muungano huo na zaidi ya yote mimi mwenyewe ninaamini kwa dhati kuwa Muungano wetu na mfumo wake ndiyo sahihi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia vigezo hivi vitatu ndiyo maana ninaitaka Serikali ya Muungano itusaidie, siyo Zanzibar. Itupe fedha tuendeshe masuala ya uchumi kwa sababu sasa hivi ni elimu tu. Tunaona kwenye teknolojia sasa hivi ni *high*

*technology* iliyopo katika mitandao ya simu na Mheshimiwa mark Mwandosya ulipokuja ukatembelea sehemu ile ya *TTCL* uliona mtandao mkubwa wa simu uliopo pale. Tuna mawasiliano ya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama sikosei mwaka 2001 nilikwenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapa hapa katika Ofisi ya Bunge na nilimwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba: "Pemba tumechoka fitina, tunachotaka ni maendeleo.

Fanya ziara uje Pemba, ukikuta maandamano Pemba sema kweli Wapemba hawajatulia, lakini nina uhakika hutakuta malalamiko mengi." Pote alipopita Mheshimiwa Waziri Mkuu Pemba katika ziara aliyokwenda alikuta risala kwamba Wananchi wanataka maendeleo na tunashukuru kwamba Serikali ya Muungano ilipeleka fedha zile za *TASAF* na zilifanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalizungumza hili kwa uwazi, kwa niaba ya Wananchi wa Pemba, kwa niaba ya Wazanzibari na Wananchi wa Tanzania kwa ujumla. Sisi ni Taifa moja, lenye Serikali mbili, anayepinga hivyo yeye ni hiari yake. Sisi huo ndiyo urithi wetu, Baba wa Taifa ameturithisha hivyo na tutatekeleza hivyo. Sisi wengine hapa tunajisema ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kufanya mzaha na suala la elimu. Elimu ndiyo ukombozi wa maeneo yote yale. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo haina msingi mzuri wa elimu. Kwa hivyo, ili kulikwamua Taifa hili ni lazima kuwe na nguvu ya pamoja na ninapenda nirudie kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Amani Karume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais Amani Karume nidhamu yake na upendo wake kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mkubwa sana na tumekuta mabadiliko makubwa ndani ya Zanzibar kwani Serikali ya Muungano inamsadia sana. Napenda nikiri hili na kwa kweli Rais Karume amefanya mambo mengi ndani ya Kisiwa cha Pemba, ndani ya Zanzibar na anastahili kupongezwa. Kama kuna wengine wanasema hakuna mabadiliko, hiari yao. Tukizungumzia uchaguzi, hilo ni suala lingine tusubiri mwaka 2005, lakini ukweli tuseme vile ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ya Muungano, tumeona juzi hapa Waziri wa Ujenzi alipowasilisha bajeti yake ameelezea zile fedha ambazo alipeleka Zanzibar kwa ajili ya kutengeneza barabara. Kwa hiyo, Wizara hii ili kumthibitishia Mheshimiwa Rais kwamba ni Taifa moja lenye Serikali mbili ni lazima mpeleke fedha Zanzibar kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar katika Sekta ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivi? Hebu tuangalie maeneo mawili ambayo haiwezekani katika Serikali ya Muungano tukashindwa. Nataka nimnukuu Kaimu Balozi wa Marekani nchini Tanzania. Hivi karibuni kwenye Vyombo ya Habari alizungumza kwamba: "Marekani itafungua Ubalozi mdogo Zanzibar katika juhudi za

kuimarisha uhusiano wa kibiashara na kukuza vitega uchumi kwa wawekezaji wanaotoka Marekani kuwekeza nchini Tanzania." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna eneo moja ambalo ni muhimu amesema kwamba: "Serikali ya Marekani itahakikisha inasaidia kuimarisha uchumi wa Zanzibar ikiwemo Sekta ya Elimu." Ninampongeza sana. Sasa kama Taifa hili limeona eneo hili la elimu, ni kwa nini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isitenge fedha kwa ajili ya Zanzibar? Wenzetu mna uwezo mkubwa sana, nchi kubwa sana, kama ambavyo nikimnukuu Baba wa Taifa alivyokuwa anazungumza: "Nchi hii ni kubwa kuliko hata Uingereza, kuliko hata Nigeria, ina uwezo wa kuchukua hata watu zaidi ya milioni 200 na tuna madini ya kutosha na nina uhakika mafuta tunayo. Ni kuweka umoja, tukaimarisha Taifa letu, tukaenda kwenye maendeleo."

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, ile dhana ambayo Mheshimiwa Rais Mkapa aliizungumza mwezi Mei mwaka jana 2003 katika hotuba yake ya kila mwezi kuwataka Viongozi mbalimbali nchini kuwasaidia Wananchi wafikie matarajio yao, hapa ndiyo sahihi. Viongozi wa Vyama vya Siasa wasiwadanganye Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikuthibitishie kwamba CCM tunashinda Zanzibar, tusiwagombanishe watu, twendeni kwenye uchumi. Kama juzi walivyokubaliana kwenye daftari wa wapigakura, tujipange tena Mungu atakayemjaalia ndiye atakayekuwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri, kuiunga mkono Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunategemea kwamba haya niliyoyasema humu mtakwenda kukaa kitako kuyatekeleza na ninaamini Mheshimiwa Prof. Mwandosya utawaeleza uliyoyaona ili na Mawaziri wenzako waje Pemba. Kuna *rest house* nzuri pale umeiona, umeona Wapemba walivyokushangilia, Pemba ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda niwapongeze sana Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu, Wataalam wa Wizara hii, Wakuu na Viongozi wa Vyuo vyetu Vikuu na Taasisi zilizopo kwenye Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara hii na Taasisi zake tangu mimi nilivyoanza kuwa na uhusiano nazo. Tunakushukuruni sana na tunawahimiza muendelee kushika gurudumu hilo na muongeze viwango vya ubora wa wanafunzi na bidhaa zingine ambazo mnatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa, Wizara hii na Taasisi zake zinajiendesha kwa bajeti ambayo kwa kweli ni finyu ukilinganisha na mahitaji na matarajio ya nchi yetu. Moja ya maeneo ambayo ufinyu wa bajeti hii unaonekana wazi ni uchache wa wanafunzi katika Vyuo vyetu Vikuu. Ukilinganisha Vyuo vyetu Vikuu vyote vya Serikali na vile vya binafsi utaona kuwa wanafunzi wote walioko kwenye Elimu ya Juu katika nchi yetu ni wachache kuliko wale walioko kwenye Chuo Kikuu cha Makerere, pale Kampala, Uganda peke yao.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, kwa kweli tunahitaji kupanua sana Vyuo vyetu Vikuu. Tunahitaji kupanua mabweni kwa sababu sehemu zingine ukosefu wa mabweni ndiyo kikwazo kikubwa cha kuchukua wanafunzi katika vyuo vyetu. Tunahitaji kutumia fedha zetu za Serikali pamoja na kuwakaribisha watu wa Sekta binafsi wawekeze katika eneo hili. Pia, tunahitaji sana kupanua madarasa. Zimeanza kujitokeza dalili za wanafunzi sasa kwenye vyuo vyetu kuanza kusomea chini ya miti. Kwa hiyo, tunahitaji kupanua madarasa, kuvipa vyuo hivi vifaa vya kufundishia, vifaa vya maabara na utafiti na vifaa vya *Computers (IT)* ili waweze kuingia katika ulimwengu wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, tunahitaji tuanzishe Vyuo Vikuu vipya ili kuweza kuchukua watoto zaidi katika vyuo hivi. Kinyume chake hali yetu itakuwa kama tulivyo katika elimu za huku chini. Katika Sekondari sisi ni wa mwisho duniani na huku kwenye Elimu ya Juu ukiangalia kila watoto 100 sisi ni karibu sana na watu wa mwisho duniani kusomesha watoto ambao wana umri wa kwenda Chuo Kikuu. Kwa hiyo, tunatakiwa tutoke hapo. Baada ya kupanua vyuo vilivyopo ni lazima pia tujenge Vyuo Vikuu vipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zamani sana wakati nilipokuwa kwenye Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA)*, wakati kinaanzishwa mwaka 1984 tayari Chuo Kikuu cha Dodoma kilikuwa kimeishatayarishwa na rasimu ya sheria yake ilikuwa tayari. Lakini tangu mwaka 1984 mpaka leo hakuna Chuo Kikuu Dodoma! Kwa hiyo, kwa kweli ni lazima tujiangalie. Hivi kweli sisi tutashindana na nani? Wanafunzi walioko katika Chuo Kikuu katika Jamhuri ya Kenya ni sawa sawa na wanafunzi wetu walioko *Secondary School, O-level* hapa nchini kwetu. Sasa sisi kweli huko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki tutashindana na nani?

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Tutaburuzwa!

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Tutaburuzwa kweli. Anasema Mheshimiwa Semindu Pawa hapa.

Mheshimiwa Spika, pia, kwa kweli vyuo vyetu vinafanya kazi nzuri sana na wanajitahidi kwa nguvu zote kutoa wanafunzi wazuri na walio na elimu ya kutosha katika fani zao. Lakini pia zimejitokeza dalili kwamba kuna udhaifu kidogo kwa sababu waajiri hasa wa Shule hizi za binafsi huko Dar es Salaam na kwingineko, wanaanza kuajiri wahitimu kutoka Kenya, wakati tunao wahitimu wengi sana ambao wana Shahada za Elimu na hawana kazi. Kwa hiyo, kuna tatizo kwamba labda waajiri wameona

udhaifu katika wanafunzi wetu. Ni vema vyuo vyetu vikaangalia upya ni kwa sababu gani tunao watoto wachache tu ambao wamehitimu, lakini wanaachwa na waajiri na waajiri wanatafuta wahitimu kutoka Uganda, kutoka Kenya, kutoka India kufundisha katika *Secondary Schools.*

Pia waajiri wanatafuta wahitimu wa nchi za nje kufanya kazi kwenye viwanda. Ni kwa nini wasichukue wanafunzi wetu? Hili ni suala ambalo ni lazima tujiulize ndani ya vyuo vyetu na sisi kama Bunge tuishauri Serikali iongeze uwezo wa vyuo vyetu ili kuweza kuziba mapengo ambayo yanaanza kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wahitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wa huko nyuma wana sifa kubwa na hata ningechukua mifano michache tu hata ya watu walioko humu ndani ya Bunge, kama Mheshimiwa Getrude Mongella, ni watu ambao wana heshima kubwa katika Afrika na dunia nzima. Kuna Rais Yoweri Museveni amesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hata wapigania uhuru mashuhuri sana wakina John Garang' wamesoma huku. Kule Kenya watu walioleta msisimko mkubwa sana wa siasa akina Paul Mwite wamesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Spika wa sasa wa Bunge la Uganda amesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na watu wengi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningesimama hapa na kuorodhesha na kusema juu ya watu wengi sana kwamba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vyuo vingine hivi kuna Wataalam wengi wenye sifa kubwa duniani.Kuna maprofesa wengi wa *SUA* ambao wanaongoza Mashirika ya Kimataifa na Idara za Umoja wa Mataifa wanaotoka kwenye Chuo chetu cha *SUA*. Sasa kwa nini itokeee kwamba wahitimu wetu sasa wanaachwa barabarani halafu wanafunzi wa Kenya ambao hata *A-level* hawakusoma. Wamesoma mpaka darasa la 12 halafu wakaenda Chuo Kikuu miaka minne wakamaliza. Wanaajiriwa badala ya watoto wetu waliokwenda *A-level* miaka miwili, wakasoma miaka mitatu na shahada zingine miaka minne. Lakini wanawaajiri, wanawachukua wageni hao badala ya wanafunzi wetu! Kwa hiyo, hili ni suala ambalo ni lazima tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, suala ambalo ningependa sana niliseme japo watu wengine hawalipendi sana, ni kwamba, tungeangalia hivi ni masomo gani zamani tulikuwa tunawafundisha watoto halafu wanakuwa wanajiamini sana na wanakuwa na uwezo zaidi wa kupambana na mazingira ya ajira na katika maisha baada ya kumaliza Chuo Kikuu.

Moja ya masomo hayo ambayo yalikuwa yanafundishwa kwa wanafunzi wote Chuo Kikuu ilikuwa ni *Development Studies.* Ninafikiri wakati umefika tufikirie tena kuwasomesha watoto wetu somo hili la *Development Studies,* hata kama watakuwa Madaktari, hata kama watakuwa Wahandisi, hata kama watakuwa ma-*VET* wote wasome somo hili. Litawapa mwelekeo wa maisha ya baadaye na linawapa nguvu zaidi na kujiamini zaidi katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo linapoteza muda sana wa Watanzania, ati tufundishe kwa Kiswahili au tufundishe kwa Kiingereza. Hali tuliyo nayo sasa ambapo elimu yetu inaonekana duni kupita elimu zingine siyo wakati wa kuanza kusema tufundishe kwa Kiswahili au kwa Kiingereza, siyo wakati wake. *That is*

*a luxury we cannot afford.* Wakati huu tunatakiwa tuwafundishe watoto wetu kwa lugha hiyo tunayofundisha sasa waweze kuwa na *proficiency ya English language* vizuri sana kama watoto wengine wa dunia. Lakini pia waweze kuwa na *proficiency* ya Kiswahili kizuri sana kupita watoto wote wa dunia hii. Hayo ndiyo tunayotakiwa kufanya. Lakini siyo kuanza kusema ati sasa *university* ianze kubadilisha mitaala ili ianze kufundisha kwa Kiswahili, hapana, hapana kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu hawa ambao wanasema watoto wakajifunze kwa Kiswahili wana watoto wao Uingereza wanasoma kwa Kiingereza, kwa nini? Hatuwezi kurudi nyuma, ni lazima tuongeze *proficiency* ya *English language* na tuongeze kujiamini kwa watoto wetu kuongea Kiingereza na kuongea Kiswahili. Kama sisi wenyewe hapa Kiingereza tunakijua vizuri na Kiswahili tunakijua vizuri. Hivi kuna tatizo gani? Watu wazima wanapoteza muda kabisa wanasema tufundishe Kiswahili, tuna uwezo? Wakati huu maabara za Vyuo Vikuu hazina vifaa na katika karakana za kufundishia wanafunzi. Kuna mashine za zamani kabisa.

Mashine moja iliyoko kwenye maonyesho ya *SIDO* hapo nje imewekwa hapa imetengenezwa na *Prospective College Engineering,* mashine hii nadhani wamekatakata na bisibisi. Maneno gani haya! Halafu mnasema tuongee kwa Kiswahili, *we cannot afford that!* Lazima tuweke nguvu zaidi kuwafundisha watoto wetu kwa kiingereza, lakini pia tuwasomeshe watoto hawa waelewe Kiswahili barabara kuliko mtu yeyote katika dunia hii. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine ambalo kwa kweli nataka kuvishauri Vyuo vyetu Vikuu. Suala hili ni kwamba wanafunzi wengi sana wanaanguka mitihani. Kule wanasema hawa siyo *university material,* lakini nadhani *there is a problem.* Tatizo letu hili tunalijua, watoto wetu matayarisho yao kwenye Shule za Sekondari ni mabovu, hakuna Walimu. Lakini kwa sababu hawakufundishwa vizuri wakajaa ndiyo maana yake siyo kwamba hawako *university material, they can be filled* wakawa *university material.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Marekani kuna mifano mizuri sana. Mimi nilisomesha kwenye Chuo Kikuu cha *Oregon,* kule kuna Idara *(Department)* ya kutoa fursa kwa wale ambao hawajajaa sawa sawa, *Department of Educational Opportunities.* Wanawafundisha watoto, wanawajaza pale ambapo wamekosa sifa ili waweze kuendelea. Hatuwezi kufukuza watoto na sisi tunapeleka shule watoto wachache kupita nchi zote duniani. Ni lazima tujiulize, hivi tunawafukuza ili iweje sasa! Kwa hiyo, tunaviomba sana Vyuo Vikuu vianzishe ama ni vitivo vipya vya kuwanoa hawa watoto kuwajazia pale walipokosa uwezo au *opportunities* zingine ambazo zitaweza kufanya hilo.

Najua haya yote niliyosema mtu atauliza na pesa tutapata wapi? Lakini mwaka 2001 tumepitisha sheria hapa tukasema kwamba tuwe na Mamlaka ya Elimu ambayo itapata asilimia mbili (2%) ya Bajeti yote ukiondoa Deni la Taifa. Sasa kama tungefuata utaratibu huu bajeti ya mwaka huu kwa mamlaka zingekuwa kama shilingi milioni 48. Sasa sheria ile ukiiangalia hailingani kabisa na mapendekezo ya mabadiliko yaliyoletwa na Waziri hapa Bungeni. Sisi tumepitisha sheria kwamba: *"Not less than two percent."*

Sasa wanasema: "Isizidi *two percent.*" Hivi wanamdanganya nani? Sheria ile si suala la kuibadilisha, sheria ile imeandikwa kama ambavyo haikupitishwa na Bunge hili. Bunge likipitisha sheria ni lazima itekelezwe na ni lazima iandikwe kama Bunge lilivyopitisha. Haiwezekani sheria iliyopitishwa na Bunge iandikwe vile ambavyo Bunge halikupitisha. Kama Serikali inataka kufanya mabadiliko ni lazima ilete Bungeni, Bunge lifanye mabadiliko hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, leo tutahitaji maelezo kutoka kwa *Attorney General* kwa sababu gani sheria ile haikuandikwa kama Bunge lilivyosema? Haiwezekani sheria zinaandikwa vile ambavyo haikupitishwa hapa na Bunge letu Tukufu. Kwa hiyo, hapo tungepata Shilingi bilioni 48; na kama zingekuwepo; haya maneno ninayosema hapa ya matatizo yasingekwisha, lakini yangepungua kwa sababu Vyuo Vikuu na Taasisi hizi leo zingekuwa na bilioni 48 badala ya Shilingi 4.4 billion.

Mheshimiwa Spika, sijui tutahakiki namna gani...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninaunga sana mkono hotuba hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla ya yote, napenda kuwashukuru pamoja na kuwasifia Waziri; Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, pamoja na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu na wote waliosaidiana kuileta Bajeti hii ya Wizara hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa sababu nilikuwa nimeishazungumza, wale wote waliofiwa nimewapa pole pamoja na wale waliopatwa na matatizo nimewapa pole. Kwa hiyo, hayo yote nimeishazingatia tayari.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ni hoja nzito kwa sababu hakuna nchi yoyote inayoendelea bila ya kuwa na Elimu ya Juu au Sayansi na Teknolojia.

Kabla sijaenda popote napenda kutoa shukrani zangu kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hasa hasa kwa rafiki yangu na mwenzangu sana Profesa Emmanuel Bavu; Mwenyekiti wa Baraza la Chuo kwa umahiri mkubwa ambao kusema kweli ameweza kufanya katika chuo na hasa migomo tunaona inayeyuka kitaaluma au kisayansi bila ya purukushani zozote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile Profesa Bavu tumekuwa pamoja katika kuanzisha Idara moja pale Chuo Kikuu, bahati mbaya Idara ile mpaka leo haijaanza tangu 1969, *Department of Philosophy and Religious Studies.* Yeye alikuwa Mwenyekiti wangu katika *Committee* yetu, lakini mpaka sana tunashangaa na yeye akiwa ndiyo Mwenyekiti wa Baraza, nadhani ni wakati muafaka wa kuanzisha Idara hiyo Chuo Kikuu.

Bahati mbaya sisi wengine tulipomaliza huko nje *Edinburgh University* tukalazimika twende *Kenya, Nairobi University* au kule Makerere wakati ambapo kama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kingekuwa kimeanzisha tungekuja pale.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Profesa Emmanuel Bavu kwa sababu yeye ni Mwenyekiti sasa wa *Council* ya Chuo cha Dar es Salaam atafute mbinu ni jinsi gani ya kuanzisha Idara hiyo ya *Philosophy and Religious Studies. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu ni ufunguo wa maendeleo kabisa, kwa sababu elimu ni mlima mrefu, kadri unavyopanda juu ndivyo unavyoona mbali. Kuona mbali peke yake hakutoshi, isipokuwa unapoona mbali unajua pale pana hatari, pale pana kitu fulani cha kuvutia, pale pana baraka, pale pana hasara, pale pana hivi, hiyo ndiyo maana yake.

Kwa maana hiyo, Elimu ya Juu kwetu hapa Tanzania ni lazima iwe na maana kubwa kwamba ni upeo mkubwa wa kujua mambo na ni kichocheo cha maendeleo na ubunifu na kuonyesha njia/mfano ili wengine wafuate.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu inawezekana kwamba tangu tumekuwa na Elimu ya Juu bado hatujaifanyia usanifu. Wenzetu katika nchi zilizoendelea kwa mfano nikichukua Japan, miaka karibu 38 iliyopita, Japan maeneo mengi ilikuwa ni mashamba ya mpunga tu, lakini kwa jinsi wenzetu walivyopanga taratibu za jinsi gani za kusomesha watoto wao na hatimaye warudi waweze kuendeleza nchi yao, kwa muda wa miaka 25 Japan ikabadilika, mashamba ya mpunga yakabadilika kuwa ni viwanda katika maeneo yote, mashamba yamebakia machache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani kuna haja ya kupanga kusanifu elimu yetu sasa ili iweze kusaidia katika maeneo yetu, katika nchi yetu na katika maendeleo ya nchi yetu. Hawa vijana ambao wanasoma wanarudi namna gani kuendeleza katika maeneo yao? Au kusoma kama alivyosema Hayati Mwalimu Nyerere maana yake ni kwamba, mtu akisoma ndiyo anahama tena hivyo, anahama kutoka kijijini kwake ndiyo haonekani huyo harudi tena mpaka akifa ndiyo pengine anaweza kurudishwa huko.

Lakini vinginevyo ndiyo amehama huyo, hayupo mpaka kuzikwa wakati mwingine hata kuzikwa hazikwi huko kijijini alikotoka. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hii ni nadharia mbovu, mbaya sana. Ni dhana mbaya. Huyu tunamtaka arudi pale alipotoka aendeleze pale awe ni mfano na wengine waige. Kwa hiyo, nasema Elimu ya Juu iwe ni mfano kwa wengine. Walio na Elimu ya

Juu waongoze, wengine wafuate kwa sababu hao ndiyo wana tochi, wana mwanga, waende mbele ili ambao hawana kitu kama hicho wafuate.

Sasa aliye na Elimu ya Juu haonekani mbele anaonekana yule asiyekuwa na elimu, maana yake nini? Ni sawa sawa na mtu asiyeona umemkabidhi njia awaongoze wengine, akiwaingiza katika shimo nani wa kulaumiwa, ni yeye au wewe? Ni wewe uliyempa uongozi huo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nasema sasa imefika wakati watu wa Elimu ya Juu, watu wenye kipato cha juu tutafute njia ya kuwaenzi hawa watu wasiondoke, wasikimbie badala yake waende wakatekeleze yale waliyojifunza, maarifa waliyoyapata Chuo Kikuu waende kule vijijini, waende katika sehemu mbalimbali wakawaonyeshe njia wale.

**MBUNGE FULANI:** Wewe utarudi?

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mimi nimerudi, nilikuwa Chuo Kikuu cha Nairobi na mwenzangu Profesa Kaniki. Profesa Kaniki amekwenda Kusini mimi nimerudi hapa. Wanaoniambia nimerudi, ndiyo nimerudi hapa na nimerudi kijijini kwangu kabisa nilikozaliwa kule Mbwera kabisa. Mimi ndiyo Mbunge wa Jimbo hilo kabisa. Kwa hiyo, kurudi nimerudi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Wizara hii ni Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, jana tumekuwa na semina hapa ya *CAMARTEC* wenzetu wale wamekuwa wakifanya utafiti na tuliona Wabunge jinsi gani utafiti katika nchi hii, umekuwa kitu ambacho hakijaliwi wala hakina thamani kubwa. Tatizo hili kusema kweli si kama tulivyoona jana, katika vituo vingi na vyote vya utafiti hali ni hiyo hiyo, vinalalamika juu ya nyenzo za kufanyia kazi, fedha na kadhalika. Hivi tuna nini, kulikoni? Hivi tutataka maendeleo haya ya kuondoa umaskini pamoja na uchumi *(Economic of Scales)* zitakuja hivi kwa bahati mbaya? Hata kidogo, lazima kufanya kazi. Fedha tunazopata, hivi kweli hatuwezi kumega sehemu kwenda katika utafiti, ili tuweze kuinua hali hii *economic? (Makofi)*

Tumeona tangu mwaka 1955 mambo haya ya ki-*check* vifaa vya kilimo mpaka leo, wameshaandaa matrekta 200 tu, sijui na kitu gani vitu kama hivyo. Wana trekta pale wanasema la miaka 40 sijui ndiyo linafanya kazi, gari la miaka 16 limekwisha kabisa hawapati senti maana yake nini? Hii maana yake ni kwamba elimu tunaivika kilemba cha ukoko tu tunapokuja kusema maneno ya kisiasa tu. Wanaenziwa wanasiasa, wanaenziwa wasanii, lakini watu waliopata elimu, taaluma hawaenziwi hata kidogo, wanaonekana kama ni makabwela maana yake nini? Nchi hii hivi tutaweza kuendelea namna gani? Kwa kupiga domo kaya katika siasa? Hata kidogo! Ndiyo maana kufahamu hiyo ehee! Ebu jamani tuamke tumelala! Ni lazima hawa wana taaluma/wataalamu tuwakamate kwa njia zozote ikiwezekana hata mishahara yote tumalizie kwao, hela zote tunazopata, ndiyo!. Hatuwezi kuendelea kwa domokaya, kwa siasa kwa malumbano ya *CUF* sijui na CCM, *TLP,* CHADEMA na kadhalika. Hatuwezi kuendelea kwa malumbano hayo, tutaendelea kwa taaluma. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Toa *fact* bwana.

**MHE. PROF. JUMA. M. MIKIDADI:** Sasa hii ni *fact* kwa kweli nasema kwamba sasa hivi tunaiambia Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, lazima iunde *think tank* kwa ajili ya maendeleo, ndiyo, masuala ya Sayansi, Teknolojia, lazima tuhakikishe kwamba tunapeleka mambo haya kule vijijini, vijiji vyetu vitaweza kupata maendeleo makubwa kama sayansi na teknolojia itakwenda kule. Kama *CAMARTEC* jana wametuonyesha lakini hawa hawajafika vijijini. Watu wanaangalia haya mambo wanasema ni *AGOA* hata kidogo kama Profesa alivyosema kama mashine mmekatakata na bisibisi, na kadhalika, mnaleta hapa kutafuta nini? Tunachotaka sisi ni watu kuwaonyesha njia kule vijijini. Kila siku maonyesho tu, ni lini watu watatumia? Amenikumbusha sana Mheshimiwa Bendera, kila siku tunaonyesha sisi Tanzania tuna sera ya kila kitu, sera ya wanawake, na kadhalika. Jamani tumetosha sera, *these policies we want now to materialize.* Kila siku sera tu, kila siku tumo mbioni tutafika lini? Mikakati haishi, watu gani watakatika, *I don't know. We don't want this, please* tunataka sasa kufanya kazi. *(MakofiKicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima zote naomba Wizara hii sasa ichachamae katika masuala ya Sayansi na Teknolojia na Elimu Juu, wawe wasimamizi waoanishe, wa-*coordinate* au waratibu na shughuli zote ziende katika utaratibu unaoeleweka, siyo kila mmoja anafanya kivyake hatutaki sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ile sheria aliyosema Profesa Maghemba hapa lazima Serikali ije kutueleza kwa nini inakuja kuandikwa, yule *Attorney General* atueleze kwa nini badala ya kusema kwamba siyo chini ya asilimia mbili anasema siyo zaidi ya asilimia mbili maana yake? Hatutaki, Bunge hili limezoea kuchezewa hatutaki kuchezewa hapa! Alaah! Kwa hiyo, leo, uje kuleta maelezo hayo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya hayo nasema sasa hivi Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, wekeni *think tank* kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii kwa kutumia watalaam wetu, watalaam wetu waenziwe wasiondoke, kusiwe na *blames* hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii, ili na mimi nichangie hotuba ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na mimi nataka kutoa fatwa sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea nimshukuru Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa umahiri wake na ushupavu wake na zaidi alipokuwepo katika Kamati ya Huduma za Jamii, jinsi anavyoshirikiana na Kamati na Naibu Waziri wake na hata watendaji wake, nawashukuru vile vile kwa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza nataka kumshukuru vile vile Mwenyekiti, wetu wa Kamati kwani na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa yale

ambayo ameyasema nayaunga mkono yote. Ni kweli maoni ya kamati tumeyatoa mbele ya kamati na tumewasilisha Bungeni, leo hii yote yale ambayo tuliyoyahisi kuwa yanafaa kuwasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa kuaanza na mamlaka ya elimu ya juu naomba nielekee huko moja kwa moja. Kwa kweli ni mfuko ambao unafanya kazi nzuri nchini Tanzania. Vile vile namshukuru Waziri kwa kutembea Tanzania nzima kueleza mfuko huu na hata kule Zanzibar amefika. Sipingani na wenzangu kuhusu mfuko huu isipokuwa napenda kuboresha zaidi kuwa utaratibu mzima kama alivyosema kuwa kuufikisha Mfuko Zanzibar, unataka utaratibu kwa sababu haya mambo yanabadilika siku zote. Yalipoanza kabla ya uhuru mpaka leo yanabadilika siku zote, ufikiri pale tulipoanza mpaka leo hii, elimu ni ile ile. Zanzibar kulikuwa hakuna vyuo vikuu sasa vipo.

Kwa hiyo, lazima kuna baadhi ya mambo yanabadilika kulingana na wakati. Kwa hiyo, mfuko huu utasaidia kwa hivi leo ulivyoaanza. Sasa naomba utaratibu uwekwe mzuri ambao utahakikisha kuwa unaweza ukafanikisha lile lengo ambalo lilikusudiwa kwa wale walengwa. Kwa hiyo, kwa hili nalishukuru. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri fanya bidii hiyo, muumalize huu utaratibu ili uhakikishe kuwa na wale ambao bado hawajapata mikopo wanapata mara sheria mpya itakapoanza. *(Makofi)*

Halafu vile vile nisisitize kuwa mamlaka hii lazima Mheshimiwa Waziri washawishi Taasisi/Halmashauri nyingine waanzishe mifuko ambayo inahakikisha kuwa inatoa elimu na inaanzisha mifuko na inakopesha au inatoa misaada au inatoa ruzuku kwa wanafunzi ambao wanataka kujiunga na elimu. Kwa hiyo, ipo haja ya kuzihamasisha Taasisi/Halmashauri kuhakikisha kuwa wanaanzisha mifuko hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu Bodi ya Mikopo ya Elimu. Hili ni jambo ambalo kwa kweli linahitaji ufafanuzi na maelezo mazuri. Kwa kweli kuna watu mpaka leo hata Wabunge inaonyesha kuwa hawajaelewa ipasavyo kuhusu mikopo. Kwa hiyo, ipo haja Mheshimiwa Waziri, kulieleza vizuri, kuhusu mikopo ya wanafunzi. Kwa kweli nakupa pole, kuhusu tatizo la maandamano ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu, ni tatizo lakini bado walikuwa hawajaelewa. Lakini wale ambao tayari walikwishaelewa kwa hiyo, hawakuunga mkono lile azimio la Wanafunzi wa Chuo Kikuu kuandamana. Kwa hiyo, ipo haja kuelimisha wananchi na hata Wabunge, kuelewa azma ya Bodi hii ya Mikopo kwa wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee mbele kuhusu suala la zima la Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kama Waziri wa Elimu alivyosema kuwa ni Wizara ambayo kwa kweli inatoa mafunzo, utafiti na kutoa ushauri kwa elimu bora nchini Tanzania. Lakini ipo haja elimu hii Watanzania tuwe *serious* kwa sababu elimu ya juu ni kioo au ni mkombozi wa nchi yoyote ile duniani.

Kwa hiyo, kama hatutakuwa serious hatutafanikiwa kwa sababu siyo Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, tu hata nchi yetu yenyewe iwe *serious* na elimu ya juu ili kuhakikiwa kuwa inaleta mafanikio na ufanisi kwa wananchi wake. Yapo matatizo

mengi ambayo kwa kweli hivi sasa yanaikabili Wizara ambayo matatizo hayo nahakikisha kuwa kama yatapatiwa ufumbuzi yanaweza yakaleta ufanisi.

Tatizo la kwanza kama alivyosema Mwenyekiti wetu wa Kamati, kuna tatizo kubwa ambalo la udahili kwa mfano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, lengo lilikusudiwa ni wanafunzi wasiopungua 7,000 lakini mwaka huu wanaweza wakadahili wanafunzi 2000 na kitu tu hivi. Kwa hiyo, ni kitu ambacho kwa kweli ni lazima kifanyiwe mikakati. Licha ya hivyo na walimu wa vyuo hivi wanakuwa na upungufu mkubwa kuna matatizo ambayo yanaikabilia Wizara ya Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu ni mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni tatizo la utafiti. Tatizo la utafiti nchini Tanzania kwa kweli ni zito na lazima liangaliwe kwa kina zaidi. Utakuta tatizo linalotukabili Tanzania, fedha nyingi ambazo tunazitegemea ni fedha nje. Ukiangalia utafiti huo tunafanya fedha za nje ambazo hazina mwendeleo mzuri wa kuhakikisha kuwa utafiti unaweza ukadumu. Kwa hiyo, ipo haja kuwa tatizo hili tuliondoe au tatizo hili tulipatia ufumbuzi. Ukiangalia mfano mzima kwa Chuo cha Sokoine ambacho fedha ya nje ambayo inategemea kwa utafiti na mambo mengine ya mafunzo ni shilingi milioni 817 tu ambazo zinategemewa nje. Wakati wakizipata kwa ufanisi ndiyo, hawakuzipata kwa hiyo, utafiti huo unakoma. Kwa hiyo, tuhakikishe kuwa fedha za ndani angalau zinakuwa nyingi kuliko za nje. *(Makofi)*

Nilioona mwaka jana, mwaka jana 2003 haikuwa na fedha za ndani ilikuwa *nil* yaani hakuna kabisa fedha ya ndani, isipokuwa inategemea ni fedha ya nje tu. Kwa hiyo, ipo haja kuwa suala la utafiti ni jambo zito na tuhakikishe kuwa fedha ambazo zinapatikana ziwe ni za ndani kuliko za nje kutegemea wahisani ambao wanaweza wakaamua kutoa au wasitoe fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala jingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuwa uhaba wa vyumba vya madarasa na mihadhara. Tulipotembelea kwa mfano Chuo Kikuu cha Mzumbe, wanafunzi ambao katika vyumba ambavyo wanafanyia mihadhara vyumba kwa kweli havitoshi. Huu ni mfano halisi kuwa na vyuo vingine ni hivyo hivyo. Kwa hiyo, uhaba huu tuhakikishe katika mipango *(plan)* yetu tunazoziweka tuhakikishe kuwa na vyuo ambavyo vinatoa mihadhara kama hii na Vyuo Vikuu lazima hili jambo lipo kwa hiyo tuhakikishe kuwepo vyumba vya kutosha vya kufanyia mihadhara ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo nataka kulizungumzia ni uhaba wa walimu wenye sifa. Hili limeonekana kuwa tatizo lipo katika vyuo vingi, wako walimu wachache ambao wana sifa za kufundisha vyuo hivyo. Kwa hiyo, ipo haja Wizara ihakikishe kuwa walimu au Baraza la Ithibati lilihakikishe kuwa walimu katika vyuo wana sifa na wanatosheleza mahitaji ya vyuo ambavyo tunahakikisha kuwa vinafanya kazi hiyo. Kwa hiyo, tatizo hili ninaona kuwa ipo haja kwa Wizara/Serikali kuhakikisha kuwa tunawaajiri walimu walio wengi na wenye sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo lipo ni idadi kubwa ya walimu wenye umri mkubwa ukilinganisha na idadi ndogo ya walimu vijana waliopo kwenye vyuo

vilivyopo Tanzania. Noamba kutoa takwimu ambayo imefanyiwa utafiti na Chuo cha Sokoine, nafikiri wanasema kama ifuatavyo: ‘Watalaam waandamizi walio na umri zaidi ya miaka 45 ni asilimia 71. Walimu waandamizi walio na umri zaidi ya miaka 50 ni asilimia 40 na asilimia 50 ya Walimu na Maprofesa washiriki wanatarajiwa kustaafu katika miaka 7 ijayo”. Je, Wizara imejiandaaje kuhusu suala hili? Kwa hiyo, inaonyesha ni idadi kubwa, baada ya miaka 10 hatuna walimu ambao wana sifa za kusomesha vyuo vyetu vikuu. Kwa maana hiyo, tuhakikishe kuwa Wizara inaweka mikakati ya kuhakikisha kuwa walimu waliopo au wanaotaka kustaafu basi pengo hilo liwe linazibwa mara moja tuhakikishe kuwa upungufu huo hauwezi ukatokea hapo baadaye ambapo walimu hawa wanaweza wakastaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu suala jingine ambalo nataka nilizungumzie ni upungufu wa vifaa vya kufundishia katika taasisi hasa Vyuo Vikuu vya Ufundi. Tulipotembelea Vyuo Vikuu vya Ufundi kwa kweli vina hali ngumu na mazingira magumu. Vifaa walivyo navyo walirithi wakati wa ukoloni mpaka leo wanavitumia hivyo hivyo havijaongezeka wala havijafanyiwa ukarabati wa aina yoyote. Tatizo ni fedha ambazo wanapewa za maendeleo ni chache haiwezi ikakidhi haja.

Kwa hiyo, ipo haja kwa taasisi kama hizi kuziongezea fedha tuhakikishe kuwa zinaboresha miundo mbinu waliyonayo hivi sasa. Kwa mfano Chuo cha Ufundi Mbeya, mitambo ambayo waliyoirithi pale tokea wakati wa Warusi. Walipoondoka tu na ule ufadhili ukawa umeporomoka. Kwa hiyo, ipo haja kuhakikisha kuwa taasisi kama zile zinaangaliwa. Nasikia hivi sasa wanataka kukifanya Chuo Kikuu, tuhakikishe kuwa tunakiboresha na tunakiwekea miundo mbinu ambayo ni ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, halafu jingine ambalo naomba kulisema ni kuwa uwezo wa kumudu lugha. Hili ni tatizo ambalo pia limeonekana katika vyuo vyetu. Wanafunzi wengi ambao wanashindwa kujieleza au kujibu maswali inaonyesha kuwa lugha ambayo wanaitumia inaonyesha kuwa haikidhi haja. Kwa maana hiyo, kama alivyosema Profesa Maghembe Lugha ya Kiswahili kwa kweli si lugha ambayo ya kufundishia ni lugha ya kuzungumza ndani ya nchi tu, lakini ni ya kimataifa inaonyesha kuwa bado hatujafikia hatua hiyo. Kwa hiyo, ipo haja tuhakikishe kuwa tatizo hili la lugha tunaliondosha, ili tuwafanye wanafunzi wetu kama tunawapeleka kwenye soko la ajira na wao waweze wanafanikiwa kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kukueleza suala jingine kuhusu mabaraza yetu ya elimu. Tulivyotembelea Baraza la Ithibati kwa kweli ni baraza ambalo linafanya kazi nzuri, lina watalaam wazuri hawajali muda, hawajali wakati, hawajali siku, ni watu ambao kwa kweli wanajali kazi zao. Lakini tatizo kubwa lililopo pale kwanza wanafanya kazi katika jengo la kupangisha, wamekodi ghorofa moja ambalo hilo ndiyo wanafanyia kazi, ghorofa hilo likizimiwa umeme wao hawafanyi kazi. Kwa maana hiyo, wao hawana kazi kwa muda wote huo ambao tatizo hilo la umeme litakuwepo. Kwa hiyo, natoa ushauri kuwa Wakuu wa Wizara wahakikishe kuwa wana sehemu yao, au wana viwanja vyao Victoria sijui wapi kule wanayo sehemu hiyo, wahakikishe kuwa wanajenga wanapata jengo lao la kudumu kuhakikisha wanafanya kazi zao ipasavyo. Lakini hata

hivyo, naona kuwa ipo haja tuhakikishe kuwa kazi ambazo wanazifanya tuzione kwamba zinakidhi haja kwa hatua tuliyonayo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kuwa baadhi ya matatizo tuliyonayo nikitolea mfano chuo kimoja kama cha Sokoine ambacho kina matatizo ambayo yanalingana na vyuo vingine, tuhakikishe kuwa matatizo kama haya yanatatuliwa. Kuna malalamiko ya wanavyuo karibu vyote kama ukitembelea utayaona. Kwa mfano ufinyu wa bajeti ni lalamiko kubwa ambalo wanasema kuwa linawasumbua kwa bajeti zao za maendeleo ambalo linawafanya washindwe kuweka miundo mbinu mipya wala hawawezi kukidhi haja kwa mfano kununua vifaa au kwa ujenzi au kwa ukarabati.

Kwa hiyo, ipo haja kuwa kama upo uwezekano wa bajeti za vyuo au taasisi za elimu ya juu, ziongezewe. Hiki ni kilio na ni usumbufu mkubwa. Hata tumwambie Waziri kama ni tatizo la nchi kwa hiyo, ipo haja ya kuwa tuangalie Serikali nzima au nchi nzima hili tatizo linaondoka hata tukimwambia kuwa tatizo lipo, lakini hana jinsi ya kufanya. Kwa hiyo, ni tatizo lakini kama walivyosema wenzetu kuwa ipo haja kuwa asilimia ya pato la taifa lihakikishe kuwa linaenda katika elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, pia lingine Chuo cha Sokoine kina upungufu wa malazi ya wanafunzi, ni tatizo ambalo walilieleza ipo haja ya kuwa tatizo hili linaondoshwa mara moja. Halafu cha kuhuzunisha kuwa tumerithi majengo, yaani umerithi tu jengo, au umerithi vifaa na vipo mtu amekugawia hivi hivi, bure bila masharti yoyote wala hakudai baadaye kuwa utoe ruzuku yoyote ile, lakini tunashindwa kuyaendeleza kama karakana zilizoko Chuo cha Kikuu cha Mzumbe, zile walizoziacha. Ni vitu ambavyo kwa kweli ipo haja Serikali ivione kuhakikisha kuwa vinafanyiwa ukarabati au vinatumika ipasavyo au wanatoa ruzuku wa vile vifaa vilivyoko pale ili viweze vikafanya kazi. Majengo yalipo pale ni mazuri mno, lakini yakifika kama miaka kumi ijayo hayawezi kufanya kazi tena kwa sababu hafanyiwi ukarabati na tatizo hili lipo na ufinyu wa bajeti upo pale pale. Kwa hiyo, ipo haja kuwa tatizo hili linaondoka mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Namshukuru Waziri wa Sayansi, Teknolojiana Elimu ya Juu, kwa msaada wake wote aliotuonyesha katika Kamati ya Huduma za Jamii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado kuna muda wa kutosha Mheshimiwa Paul Ntwina.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, muda huu naona ni mwingi kwa sababu mengi yameongelewa na wenzangu, mimi nitaongea yafuatayo kwa ufupi zaidi. Kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita wakiwa na Katibu mahiri wa Wizara hiyo, Bibi Lucy H. Mollel, pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo. Pili ningependa kuwapongeza viongozi wa vyuo vyote ambavyo vipo hapa nchi vya Serikali na binafsi kwa kuhakikisha wanafanya kazi sambamba na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitaanzia alipoishia rafiki yangu Profesa Juma M. Mikidadi, kuhusu namna gani tunaweza kuwaenzi hawa wenzetu ambao wako vyuoni hasa kwa maana ya *doctors* na *professors* ili kuibadili nchi yetu. Huko nyuma nchi yetu ilikuwa ina nguvu sana katika *currency* mbalimbali na uchumi wetu ulikuwa ni mzuri sana. Lakini kwa muda mfupi tu kwa miaka hii michache sijui tulijisahau wapi nchi kama Malaysia, Singapore na kama alivyotaja mwenzangu Japan wamebadilika ghafla hata India yenyewe nakumbuka enzi ile uchumi ulikuwa uki-*compare* na Tanzania tulikuwa tunawazidi. Ombi kama alivyosema mwenzangu ni kwamba ebu tujaribu kuwaenzi hawa watu watusaidie katika kuwasomesha vijana wetu waweze kuibadili nchi yetu ikawa kama zamani wakati nchi ilikuwa katika hali ambayo iko katika maendeleo ya uchumi hasa sasa hivi wa soko huru na utandawazi. *(Makofi)*

Nina eneo lingine ambalo ningelipenda kulisema kabla sijamaliziwa na muda wangu ni udhibiti wa ubora wa elimu yenyewe. Hivi karibuni kumetokea malalamiko ya wananchi wakinung'unika juu vyeti ambavyo vimekuwa vikizagaa naweza kuviita *tiger papers* penginepo lakini ningeomba vyuo hivi kwa sababu vinaweza kwa ukaribu zaidi kutusaidia katika kuondoa wasiwasi huu wa vyeti hivi ambavyo vimekuwa vikizagaa na watu wengi kujiita ma-*doctor* na kadhalika. Naiomba hii Serikali itafute njia nyingine ya kuweza kudhibiti eneo hili lisije likawa ni eneo ambalo linachafua nchi yetu katika upande wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa bajeti ya mwaka 2004/2005 ni mzuri na una maeneo ambayo katika zile *dots* nime-*list down* ziko kama 25. Kuna *dot* ile namba sita nimei-*list* ukihesabu katika vitabu mlivyonavyo inasema kuwasilisha Bungeni, Sheria Elimu ya Juu kama wenzangu walivyosema bila shaka itawakilishwa mapema. Kuna *dot* nyingi nimei-*list* kama 15 ukihesabu kununua mitambo ya mashine ya Chuo cha Ufundi cha Mbeya na kukiimarisha. Wenzangu wamezungumzia sana hilo na nafikiri litaimarika na mwisho kuna *dot* nyingine ambayo nimei-*list* kama 22 kuhamasisha wanafunzi mashuleni kuchukua masomo ya sayansi ya msingi katika ngazi zote. Hili nalo ni muhimu hasa tunakoenda huku katika kuhakikisha kuwa tunakwenda na utandawazi kama nilivyosema mwanzo.

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo ya msingi katika kila chuo hapa nchini. Yapo yale ya msingi ambayo bila shaka Waziri au Wizara hii inayohusika inajaribu kuyaboresha na itazidi kuyaboresha. Kwa mfano wenzangu wamezungumzia juu ya vyumba vya wanafunzi, lakini si hiyo tu hata majengo ya walimu wao, nyumba za kuishi siyo nzuri, siyo za kutosha, nalo ni tatizo ambalo lipo. Vitendea kazi kwa mfano *computer*. Katika eneo lingine kwa mfano pale Mzumbe kuna tatizo la zahanati/hospitali ile ambayo kuna wakati liliulizwa swali hapa, tukajibiwa. Lakini ningeomba kama ingewezekana pia watusaidie pale Mzumbe kuhakikisha inajengwa *mortuary* kwa sababu ni tatizo ambalo ni la msingi, zahanati ile inatumika na wananchi na ingeweza kusaidia kukiwa kumetokea na tatizo lolote wakati wowote ule. Nina imani kama nilivyosema mwanzo matatizo ni mengi yanayohusu vyuo vyote na kwa ujumla wake naiomba Serikali isaidie kuyaangalia ili yaweze kutatuliwa. Pia, liko tatizo la ongezeko la wanafunzi ambalo ni kubwa sana ambalo nalo hili ndiyo chanzo cha mambo hayo yote, ningependa kama Serikali ingeweza kujaribu kutatua hili kwa kuongeza majengo na pale

ambapo majengo yapo basi yale yakarabatiwe ili yaweze kukidhi maeneo ambayo yangeweza kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Waziri pia ameeleza jinsi alivyotoa mgao wake katika Elimu ya Juu, mgao wa fedha 2003/2004 kutokana na Mfuko wa Elimu. Naamini kuwa Serikali kwa upande wake pamoja na mgao huu hizi fedha hazitoshi katika maeneo mengi. Naiomba Serikali kwenye bajeti ya mwaka ujao 2005 utakaofuata ijaribu kuongeza eneo hili kwa sababu bila kuongeza eneo la bajeti bila shaka vyuo vyetu havitaweza kukidhi maeneo ambayo tumeyasema ni matatizo makubwa ya kuweza kuyaboresha. Pia lipo tatizo la msingi katika maeneo mengine ambalo limekuwa likiwatatiza wanafunzi, wanaokaa mbali na vyuo mara nyingi wamekuwa wana usafiri wa kuwapeleka shuleni lakini nalo ni tatizo. Ningeomba Serikali kuhakikisha kuwa kama kuna suala linajitokeza kama hilo wajaribu kusaidia usafiri ili wanafunzi waweze kuwahi masomo kila siku na waweze kusaidiwa. Kama nilivyosema ni kwamba maeneo mengi yanafanana ingawa kwa umuhimu wake unaweza ukasema hasa maeneo yale ambayo yanatakiwa yaelezee lakini yameelezwa na mimi naiomba Wizara hii, nipo nayo karibu zaidi ijaribu kusaidia maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyaeleza. Napenda kuchukua nafasi hii pia kumshukuru sana Mwenyekiti ya Kamati ambaye ni Mheshimiwa Omar Kwaangw' kwa jinsi alivyotembelea vyuo hivi na ku-*outline* matatizo ambayo kama mimi nilivyosema hapa kuwa yanafanana. Ameyaelezea vizuri na si vizuri kuweza kuyarudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Waliojiandikisha kuchangia kwa mdomo humu ndani ya ukumbi wamebaki wawili ambao ni Mheshimiwa Benson Mpesya na Mheshimiwa Profesa Mwakyusa watachangia kipindi cha mchana ile nusu saa ya kwanza baada ya saa 11.00.

Baada ya hapo ningependa kueleza jambo moja limetajwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe akilaumu Serikali kwamba imebadilisha maneno fulani katika Muswada uliopitishwa na Bunge hili. Nilitaka kufafanua tu kwamba kazi ya kuhakikisha kwamba Muswada unaopitishwa na Bunge unamfikia Mheshimiwa Rais katika sura ile ile ulivyopitishwa na Bunge ni kazi ya ofisi yangu, siyo kazi ya Wizara wala ya Serikali, wala ya *Attorney General*. *Attorney General* anatayarisha Muswada anauleta hapa. Miswada mingi inafanyiwa marekebisho *(amendments)* humu ndani. Sasa mwenye wajibu wa kuhakikisha kwamba *amendments* zilizofanywa zinaingia kwenye Muswada kabla haujaenda kwa Mheshimiwa Rais ni Katibu wa Bunge, ndiyo maana anasaini pale mwisho kila Muswada unaokwenda kwa Rais, Katibu anasaini kusema kwamba ndivyo ulivyopitishwa na Bunge tarehe fulani. Kwa hiyo, tutakwenda ku-*check* kama ile *bill* iliyokuja ilikuwa na maneno yapi, tutatazama kama kulikuwa na *(amendments)* marekebisho yoyote, halafu tutampa jibu Mheshimiwa Waziri aweze kulitoa la uhakika atakapokuwa anajumuisha. Baada ya hapo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niwe mtu wa kwanza mchana huu kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ningependa nimpongeze sana Mwalimu wangu Dr. Ng'wandu kwa kazi nzuri anayoifanya ambayo kwa hakika inatupa mwanga Watanzania na uelekeo kwamba ifikapo mwaka 2025 kwa mujibu wa Dira ya Taifa tutakuwa tumefika mbali. Ninafikiri anafanya kazi hiyo kwa ufanisi kwa sababu amempata Naibu Waziri ambaye naye ni makini, anamsaidia vilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukizungumzia juu ya utandawazi kama agenda ya karne hii ya leo. Ukipitia sana katika utandawazi watakwambia kabla ya kufufua viwanda vyako, kabla ya kufanya jambo lolote katika nchi yako, ili ufanikiwe katika utandawazi, kitu cha kwanza ni kuhimiza na kuimarisha elimu ya juu. Kama huwezi kuhimiza elimu ya juu na ukaitoa kwa Watanzania wengi, uwezekano wa kushindana katika suala zima la utandawazi, Watanzania tutakuwa tumeachwa mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nimempongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu, mchango wangu mchana huu nanuia tu kuimarisha zile sehemu nyingine ambazo pengine wazipatie sura mpya na kuziangalia upya.

La kwanza, nasema kwamba bado elimu yetu ya juu haijajibu masuala na matatizo ya msingi ya wakulima wetu Vijijini. Ingawa hapa tunaizungumza sana Wizara ya Kilimo, lakini tunategemea Elimu ya Juu iwe imetoa majibu kwa baadhi ya mambo ambayo tunaona ni tatizo kwa wananchi wetu lakini bado sasa hivi Mtanzania aliyeko Kijijini anatumia jembe la mkono.

Wataalam wetu wa ugunduzi na utafiti wanasemaje juu ya hilo? Ni nani mwenye wajibu wa kuhakikisha kwamba wakulima hawa wanajikomboa sasa na wanapata zana ambazo ni rahisi katika kuzalisha mali? Ni nani mwenye wajibu huo? Wasomi wetu hawawezi kukwepa wajibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe wazi kwamba Taifa hili limetumia pesa nyingi sana kwa ajili ya kuwaimarisha wasomi na Taifa na halijawahi kutoa pesa kwa ajili ya wakulima. Wananchi wamejifunga mikanda ili fedha ziende kwa wasomi hawa ambao baadaye waweze kuwakomboa wakulima wetu.

Lakini jibu hilo bado halijajibika. Elimu yetu bado haijajibu matatizo tuliyonayo kama Watanzania. Tunahitaji kufanya bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa kwamba hatuna fedha za kutosha katika Bajeti zetu. Lakini lugha hii inanikera kila wakati. "Sungura mdogo hatuwezi kumgawana", "Bajeti yetu ni finyu." Nafikiri Waheshimiwa Wabunge na kila mmoja wetu hapa anajua hali ya uchumi wetu. Tatizo tunalolizungumza hapa sio ufinyu wa Bajeti, tatizo letu kubwa ni vipaumbele *(priorities)!* Kama tunataka twende sambamba na karne ya 21 bila kuongeza Bajeti katika Sekta ya Elimu ya Juu tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Wenzetu wote walioendelea wamejitahidi sana ku-*invest* katika elimu.

Lakini sisi bado elimu tunaipa fedha ambazo ni kidogo sana. Tusitarajie mabadiliko katika hali kama hii. Tutakwenda kwa kusuasua kitu ambacho ni hatari sana katika dunia hii ya utandawazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pamoja na matatizo yetu ya kiuchumi, Wizara ifikirie namna ya kuvipanua Vyuo Vikuu vyetu. Idadi ya Wanachuo wanaoingia katika Vyuo Vikuu lazima iongezeke. Lakini kuongezeka huku kuende sambamba na kujali maslahi ya wanataaluma wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi ndugu yangu Zubeir Ngwali alizungumzia hapa juu ya asilimia 71 ya wanataaluma katika Vyuo vyetu wanaotarajiwa kustaafu ndani ya miaka miwili. Wizara imejiandaaje katika wimbi hilo? Maana itafika miaka miwili hatujachukua hatua zinazostahili katika kurekebisha hali ya namna hii na huu ni mfano wa juzi tu.

Kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa alizungumzia juu ya hatari ya kupanda kwa mafuta, lakini Serikali ikasema tusiwe na wasiwasi hilo halitajitokeza. Lakini baada ya kesho yake tumeona mabadiliko katika bei za mafuta. Sasa Serikali imejiandaa vipi katika hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, najua tuna sheria tuliyopitisha hapa juu ya *retiring age* ya wanataaluma wetu. Mimi naomba ikiwezekana sheria hiyo tuipitie upya. Miaka 63 kwa mwanataaluma ndio kwanza ameiva tayari kwa ku-*impart knowledge* wewe unamwambia a-*retire* na ametumia umri wake mwingi katika kufanya kazi ya kutoa taaluma, hawezi kufanya biashara ya nyanya wala ya mchicha! Ninaomba hili lifikiriwe. Wakati unaandaa mikakati ya namna gani utatatua hii asilimia 71 inayotegemea ku-*retire,* tuangalie namna ya kuongeza umri wa wanataaluma wetu ku-*retire,* vinginevyo tutaliacha Taifa hili tukiwa bado tunawahitaji, ni hazina ya nchi hii, tungependa tuwatumie bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na suala zima na kuongeza muda pengine wa wanataaluma wetu, naomba nizungumzie juu ya *MTC* (Chuo Kikuu Kitarajiwa cha Teknolojia) kule Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kabisa kwa dhati ya moyo wangu kwamba ninathamini na kuheshimu jitihada za Serikali na hatua zinazochukuliwa juu ya

kukijenga Chuo hiki kutoka kwenye Chuo cha Ufundi mpaka kuwa Taasisi ya Teknolojia na hatimaye kipate hadhi ya Chuo Kikuu. Ninathamini sana hatua zote zinazochukuliwa na Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla. Lakini ni vyema tukaenda kwa *speed* inayotakiwa.

Chuo hiki tuliahidi katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na mwaka kesho ndio tunasimama tena kwenye majukwaa. Tulijinadi na tukasema mkitupa madaraka ndani ya miaka mitano, *MTC* mnayoiona sasa hivi itakuwa Chuo Kikuu. Wenzetu wanaotaka watawale badala yetu wakasema hizo ni ndoto haitawezekana.

Sasa mwaka mmoja umebaki, mwaka 2005 tunasimama jukwaani, Mheshimiwa Waziri tukawaambie nini? *MTC* Chuo cha Ufundi Mbeya kinakuwa Chuo Kikuu au watafuata yale waliyozungumza akina Dr. Slaa kwamba hayo mnayofikiria sio ya kweli? Tukawaambie nini? Mimi nangojea jibu. Jitihada zote Mheshimiwa Waziri amezifanya vizuri, ametembelea na Naibu wake ametembelea tunashukuru. Lakini tukawaambie nini wale kwa sababu tulishawekeana ahadi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wetu sasa hivi, ni vizuri tukawa na maamuzi ambayo kwa kipindi kama hiki ni *so daring.* Nampongeza Waziri mmoja hapa ambaye ni jasiri naye ni yule ambaye anawawakilisha watu wa Monduli.

Kwa muda mrefu watu wa Mwanza, Shinyanga walikuwa na matatizo ya maji, lakini akaamua kuwa *darin*g pamoja na *treaty* na katika taratibu unaambiwa hutakiwi kuivunja *treaty,* unatakiwa kuirekebisha. Tunahitaji Mawaziri wa namna hii ambao ni *so daring* ambao wanaweza kuchukua hatua wakasema hili nimefanya kwa sababu ya maslahi ya Taifa hili na tusiwaonee haya watu kama hao. Kama wanaomba nafasi tuwapigie debe, tuwashangilie, watatufaa katika Taifa hili. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara hii iangalie namna ya Kurekebisha ile hali ya *MTC* ili hatimaye tupate Chuo Kikuu kule Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nimeangalia katika ukurasa wa 22 juu ya upanuzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ni Chuo ambacho kimefanya kazi nzuri sana kwa muda mfupi kwa miaka machache iliyopita, ninaiomba Serikali iamue sasa kukiimarisha Chuo Kikuu Huria hasa kipindi hiki ambacho tunatarajia kuwa na Wanachuo 19,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo majengo mengi Mikoani ambayo hayatumiki kwa kazi yoyote. Ifike mahali majengo haya ambayo hayatumiki kipewe Chuo Kikuu Huria ili waweze kutoa elimu ya kutosha kwa Watanzania.

Ninajua kule Arusha kuna majengo yaliyokuwa ya *TANROADS* na wale ndugu zangu wa Arusha Chuo Kikuu Huria hawana mahali sasa hivi wenye jengo wanachukua, ingekuwa ni wakati muafaka Serikali ikaangalia namna ya kuwezesha majengo yote yale ambayo ni ya Serikali na hayatumiki kikamilifu yatumike kwa ajili ya kuwaelimisha Watanzania wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka mtaalam afanye kazi yake vizuri, lazima uhakikishe kwamba *Administrative Staff* inalipwa vizuri ili kazi zao ziende sambamba. Ukiwapa maslahi mazuri wanataaluma ukawaacha wale wanaosaidia wanataaluma utakuwa hujafanya lolote, maana hawa ni sawasawa na mkono mmoja wa kulia na mwingine wa kushoto.

Sasa nilikuwa naomba Wizara itueleze, hivi ni *scheme of service* ipi ya hawa *Administrative Staff* itakayofuatwa? Baadhi ya Vyuo mathalan *SUA* na *University of Dar es Salaam,* wameleta za kwao. Vyuo vingine ambavyo hawajaleta watalipwa kwa *scheme* ipi? Kukitokea tofauti, kwa nini tofauti hii ijitokeze?

Ninaomba Mheshimiwa Waziri mwishoni muangalie namna ya ku-*synchronize* hili. Kama *Administrative Staff* wa Chuo Kikuu Huria watalipwa tofauti na wale wa Chuo Kikuu cha Mzumbe au *SUA or University of Dar es Salaam,* tutakuwa hatujawatendea haki. Naomba hili mliangalie najua liko Mezani kwa Waziri au Mezani kwa nani, lakini lifanyiwe kazi. Tunawahitaji hawa *Administrative Staffs* kuwasaidia wanataaluma wetu katika kuhakikisha kwamba nchi hii inakwenda kitaaluma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu, naomba niunge mkono hoja hii ya Waziri wetu, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya mwisho ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu katika hii hoja muhimu ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Ng'wandu, pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu, Mama Ruth Mollel na Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Wametupa ripoti ya utekelezaji ambayo ni nzuri ambayo imeletwa kwetu kwa ufasaha.

Lakini vile vile ningependa kutambua kuwepo hapa Bungeni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Ndugu Ibrahim Mohamed Kaduma, na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Emmanuel Babu. Sio kawaida kwa watu wenye shughuli nyingi kama hao wakachukua muda kuja kuwepo hapa wakati tunajadili Taasisi wanazoziongoza. Nitakuwa sijawatendea haki kutowapongeza wale tuliowapa dhamana ya kuendesha Vyuo vyetu Vikuu. Kuna Makamu Wakuu wa Vyuo wako hapa na Watendaji wengi. Nawapa hongera sana kwa kazi nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti tuliyoletewa katika hotuba inaonyesha utekelezaji mzuri sana. Nimefarijika kwamba katika kipindi cha mwaka uliopita Wizara imeweza kupitisha na kuanzisha Mamlaka ya Elimu, vile vile Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ililetwa hapa tukaijadili na kuipitisha, sasa imekuwa sheria. Wote tunatambua kwamba ilipata tafsiri iliyokuwa potofu lakini nina imani kwamba wananchi sasa wanaelewa kwamba mlengwa wa hii Bodi ilikuwa mtoto wa watu maskini.

Vile vile nimefarijika kuona kwamba idadi ya wanafunzi inaongezeka hususan ile ya akina mama ambao katika mwaka uliopita iliongezeka kwa asilimia 11, nawapa hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji kama huu unaonyesha kwamba Wizara kusema kweli iko *serious* na Elimu ya Juu. Sasa hivi tumeona mwamko na hamasa kubwa kati ya wananchi katika ujenzi wa Sekondari. Wakati tunajadili hotuba ya Waziri wa Elimu tulipewa takwimu ambazo zilijisemea zenyewe na ujenzi wa Shule za Sekondari ulitokana na kwamba vijana wetu wengi waliokuwa wanamaliza Darasa la Saba walikuwa hawana nafasi ya kuendelea na Sekondari. Sasa tuangalie kwamba miaka minne ijayo, matatizo ambayo tumekuwa tukiyaona Shule ya Msingi yanahamia kwenye Sekondari.

Kwa maana hiyo kutakuwa na *bottleneck* kwa vijana wengi watakaokuwa wanamaliza masomo ya Sekondari, lakini tutakuwa hatuna mahali pa kuwapeleka kwenye Vyuo Vikuu. Kwa hiyo, ningesema tu kwamba kazi nzuri imefanyika lakini lolote lililozungumzwa halitoshi. Kwa hiyo, maandalizi yaanze mapema tusije tukawa *taken by surprise* wakati tunaanza kuwa na vijana wengi wanaomaliza Sekondari lakini hatuna mahali pa kuwapeleka katika Vyuo Vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nizungumzie kidogo kuhusu Sheria ya Elimu ya Juu yaani *Umbrella Act.* Kama tunavyojua, kila Chuo kilianzisha na sheria. Baada ya uzoefu wa muda mrefu tumeona katika utekelezaji kwamba kuna vipengele vinavyohitaji kubadilishwa na vile vile kuna haja ya kwenda na wakati. Sasa hivi Vyuo vyetu mazingira ya utekelezaji na utendaji wa kazi yanafanana. Kwa hiyo itakuwa vyema kuwe na sheria ambayo inachukua zile *broad issues* zikawekwa pamoja kuliko kila Chuo Kikuu kikaja kila wakati na sheria yake hapa au kutaka kubadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2001 tulipoingia hapa Bungeni na hata kabla ya hapo, hotuba ya Waziri mwenye dhamana ya Elimu ya Juu zimekuwa zikiahidi kwamba Muswada unaohusu *Umbrella Act* ungeletwa hapa Bungeni. Lakini hadi leo hatujaona. Mwaka jana tuliahidiwa, mwaka huu katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri *bullet* ya tano inasema, katika mwelekeo wa mambo yatakayofanywa kwa mwaka huo wanachokiombea fedha ni kwamba watawasilisha Bungeni Sheria na Elimu ya Juu.

Sasa mimi ninachosema ni kwamba wakumbuke Wizarani kwamba mambo mengi yamesimama kwa sababu yanasubiri hii *Umbrella Act.* Sasa najiuliza kama suala hili limepewa uzito unaostahili? Ningependa wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri atupe kauli kwamba hii *Umbrella Act* inakuja au tuifute katika mawazo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili. Kama tunavyojua, tulikuwa na Shirika la Afya Muhimbili kwa sheria ambayo ilipitishwa hapa ikagawanywa na kuzaa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Chuo Kishiriki kikabaki kama kilivyokuwa.

Baadaye ikaundwa Kamati ya Mpito ili kuangalia mgawanyo wa mali utakuwaje, majengo na hata watenda kazi. Ilivyo sasa ni kwamba watenda kazi, waendeshaji sio matatizo sana, lakini kwa Wahadhiri imekuwa matatizo kwa sababu wamepewa uwezo wa kuchagua wabakie katika Chuo au upande wa Serikali. Baadhi wameamua kubaki na Hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia Wahadhiri ambao wanashughulika na mambo ya tiba ni kwamba hao hao ni Walimu na wakati huo huo ndio Madaktari Bingwa ambao tunawaona pale. Sasa kuna wengine ambao wameamua wabakie Hospitali lakini hii Kamati imetoa ripoti ambayo haijafanyiwa kazi. Kwa hiyo, wasipofundisha utawafanya nini? Kuna wengine hawajazi hata *form* zile za Utendaji, utawafanya nini?

Natambua kwamba Shirika la Afya Muhimbili lilikuwa chini ya Wizara ya Afya. Kamati ya Mpito iliyoteuliwa ili kuangalia mgawanyo wa Watendaji na mali, iliteuliwa na Waziri wa Afya na baada ya kukamilisha kazi ripoti alipewa Waziri wa Afya.

Lakini Chuo Kikuu Kishiriki ndio kinaathirika! Chuo Kikuu Kishiriki kiko chini ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na kwa sababu Serikali ni moja nadhani nililete hapa kwa sababu ufundishaji hauendi kama ilivyotarajia. Ningeomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, mapendekezo ya Kamati yakamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia najiuliza hiki Chuo Kikuu Kishiriki kitakuwa Chuo Kikuu kamili lini? Maana yake wakati kinaanzishwa mwaka 1991 walipewa miaka mitatu kwamba wangejidhatiti mpaka wawe Chuo Kikuu kamili. Lakini mpaka leo hatujasikia chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine natambua kwamba Kanuni zetu haziruhusu kurudia yale yaliyozungumzwa na wachangiaji wengine, lakini nigusie tu kidogo kuhusu Chuo cha Teknolojia cha Mbeya. Huko nyuma tunajua kwamba pesa zilizojenga kile Chuo ziliombwa wakati wa awamu ya kwanza kutoka Urusi na Chuo kile kikajengwa. Marehemu Mwalimu alitamka kabisa nia yake kwamba kile Chuo kiwe Chuo Kikuu cha Teknolojia.

Katika kipindi chote ambacho tumekuwa Wabunge hapa, tumekuwa tukizungumzia habari ya hicho Chuo na nilikuwa nasoma kwenye ripoti ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa tisa, imesema kwamba katika kipindi kilichopita cha mwaka huu uliopita, Wizara imenunua mashine na mitambo yenye thamani ya Shilingi milioni 400 kwa ajili ya Chuo cha Ufundi Mbeya ili kuimarisha ufundishaji wa Stashahada ya Juu ya Uhandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kinachotegemewa kufanyika mwaka unaokuja ambapo fedha ndio zinaombwa sasa katika ukurasa wa 22, wanasema wanatarajia kununua na kufunga mashine na mitambo katika Chuo cha Ufundi Mbeya, kwa lengo la kuboresha mafunzo yatolewayo.

Sasa tunachojiuliza ni kwamba hapa suala la kuwa Chuo Kikuu halijatamkwa na linafifia kidogo kidogo. Nilitaka kujua kwamba hivi nia bado ipo au tunataka kuboresha ufundishaji wa Stashahada tu? Ningeomba Mheshimiwa Waziri ajielekeze kwenye hilo wakati anafanya majumuisho. *(Makofi)*

Ningependa pia Waziri na Serikali tuwaonee huruma watu wanaokaa Kusini mwa Reli hii. Ukiangalia Reli ya Kati, Vyuo vyote vinavyozungumzwa viko Kaskazini ya Reli ya Kati. Nilikuwa naangalia jedwali la muhtasari wa usajili na ithibati ya Vyuo vya Elimu ya Juu. Kuna Arusha, Moshi, Dar es Salaam, Dar es Salaam, Bugando, Mwanza, Moshi, *KCMC,* Dar es Salaam. Watu wa Kusini wanajiuliza hivi na sisi tuko Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nizungumzie kidogo kuhusu Chuo Kikuu cha Mzumbe. Serikali ina Vyuo Vikuu vinne na Chuo Kikuu cha Mzumbe ndio Kitindamimba. Kimefikia hatua ya kuwa Chuo Kikuu baada ya historia ndefu. Ni rahisi kwa Serikali kuhesabu kwamba ina Vyuo Vikuu vinne.

Lakini ukienda kiundani, uendeshaji na *infrastructure* ni vitu tofauti kabisa. Wengi katika wachangiaji waliotangulia wamezungumzia kuhusu ukarabati mkubwa wa majengo unaohitajika, lakini Mzumbe haina hata hayo majengo ya kukarabati. Naona Serikali ichukue hiyo kama ni mtoto anayesimama dede, kwamba lazima imshike mkono.

Kwa mfano kuna shida kubwa ya *accommodation* ya wanafunzi, pia Walimu wenye sifa. Kwa hiyo, rai yangu ni kwamba Serikali ikiangalie hiki Chuo kwa jicho la ziada la huruma kwa sababu kuweza kuwafikia wenzao itachukua muda mrefu kama Bajeti itakuwa inawekwa kwenye ukurasa mmoja na Vyuo Vikuu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nikae na ninaunga mkono hoja na kuwatakia utekelezaji mwema wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. LEAONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nawatakia utekelezaji mwema wa malengo mliojiwekea kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kuwa Mamlaka ya Elimu Tanzania ipewe fedha 2% ya mapato ya ndani kama sheria inavyoelekeza. Kwa mwaka uliopita *TEA* walipewa tu shilingi bilioni 6.7 badala ya shilingi bilioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama fedha zingetolewa kama ilivyopangwa, mafanikio yangekuwa mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri vijana wanaopata *marks* za juu sana kwenye mitihani ya *Form VI,* vijana hawa wapewe upendeleo maalum kuingia Vyuo Vikuu na mfuko huu wa *TEA* usaidie kuwalipia gharama zote za shule na vyuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Walimu Mkoa wa Shinyanga, kutokana na wingi wa watu katika Mkoa wa Shinyanga naiomba Wizara pia ione uwezekano wa kuwa na Chuo cha Ualimu pamoja na uwezekano wa Wizara kujenga Chuo Kikuu katika Mkoa wa Shinyanga maana kwa sasa hakuna mwekezaji ambaye amejitolea katika kuweka Chuo Kikuu, ni vyema Serikali yenyewe ianze kujenga Chuo Kikuu kitakachofundisha *Geology/Engineering* na masomo mengine yanayoweza kuharakisha maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Shinyanga unayo madini mengi na kilimo. Nitapenda wakati Mheshimiwa Waziri anajumuisha aeleze mipango ya Chuo Kikuu Mkoa wa Shinyanga na Chuo cha Ualimu ikoje pamoja na kuongeza fedha kwenye Mfuko wa *Tanzania EducationAuthority (TEA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, asante, nawatakia Wizara utekelezaji mwema wa malengo waliyojiwekea kwenye *finincial year* 2004/2005.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii kwa kiwango cha 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba hoja zangu zifuatazo zijibiwe au zifafanuliwe.

Kwanza, ni nini kinakwamisha Chuo cha *IFM* kisiwe Chuo Kikuu kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam? Kigugumizi hicho kinatoka wapi na kwa nini?

Pili, katika hoja ya Waziri wa Elimu na Utamadanuni, alitaja kuwa Vyuo vya Ualimu vya Dar es Salaam na Mkwawa vitafanywa kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki ambavyo vitakuwa vinatoa wahitimu wa Shahada za Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona ufafanuzi wa ukweli huo, kwani Vyuo Vikuu si vipo chini ya Wizara yake? Ni vizuri ufafanuzi ukatolewa ili wananchi wasikie na kuelewa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Chuo cha Marangu na Butimba visipewe hadhi ya kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki ili kuongeza wahitimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna huyu mtumishi anaitwa Eliwako E. K. Mjemah, amekuwa akimwandikia Mheshimiwa Waziri kuhitaji fedha za mafunzo kwa ajili ya kozi ya *EMBA* lakini bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri asaidiwe maana ana ari ya kujiendeleza, yeye yupo tayari hata kwa utaratibu wa mkopo, mradi ajibiwe na kupewa maelekezo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kutojibiwa na kuelekezwa njia mbadala ili nia yake ya kujisomea ikamilike. Naambatanisha na barua zake alizokuwa anaandika. Naunga mkono hoja mkono.

**MHE. LAKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza pongezi kwa Wizara kwa kazi nzuri ya kuongeza Vyuo vya Elimu ya Juu nchini wala sio ongezeko tu pamoja na mipango na mikakati *(Action Plan).* Ongezeko la wanafunzi kwenye Vyuo Vikuu limekwisha onekana. Kutokana na mikakati iliyowekwa na Wizara nategemea Tanzania itapiga hatua ya ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kuondoa malalamiko yaliyokuwepo ya madai ya wanafunzi wanaosoma nje ambayo yalikuwa kero miaka ya nyuma sasa hayapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi kilichopita kulikuweko na maandamano ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhusu mikopo ya kukopesha wanafunzi wa Chuo Kikuu. Malalamiko hayo bado yanaleta utata hata kwa Watanzania wengi. Hasa wasiwasi ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, namna ya kulipa hizo fedha kwani mkopaji hatajua atapata kazi (ajira) wakati gani aweze kulipa fedha hizo.

Pili, uwezekano mkubwa wa wanafunzi wanaotoka kwenye jamii maskini kuachwa kwa ajili ya kutoweza kukamilisha masharti hasa kumpata mdhamini.

Tatu, wanafunzi wengi ambao wazazi wao hawakwenda shule kushindwa au kutojua kufuatilia utaratibu wa kufuata mikopo hiyo. Pamoja na muda mdogo wa kulipa deni hilo

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jamii ya Watanzania bado wako nyuma sana kielimu pamoja na ongezeko la wanafunzi wa Vyuo Vikuu, bado jamii ya wafugaji hasa Wamasai, Wabarbaigi hawapo kabisa katika Vyuo Vikuu na wachache wanakosa nafasi kwa kutopata uwezo wa kwenda kupata Elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi, naomba sasa wafugaji wapewe kipaumbele na wajiunge na Vyuo Vikuu kwani wameachwa nyuma. Kwa mfano, kuna wanafunzi wasichana waliomaliza *Form VI Maasai Girl Secondary School* wamerudi nyumbani kuolewa. Karibu wanafunzi wa miaka mitatu hawakuendelea na Elimu ya Juu. Ili jamii ya wafugaji waendelee, ni lazima sasa wasaidiwe kipekee kwani wamebaki nyuma. Hatuwezi kusema Tanzania wameendelea kama jamii nyingine wameachwa nyuma. Kwa masikitiko watalii wanakuja kuwaangalia wanyama na Wamasai kwa sababu bado wako nyuma, siyo kwa umuhimu mwingine. Je kwa nini watalii hawaendi kuangalia jamii nyingine wanavyoishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili jamii hii waendelee na kuwaadilisha, jamii hii wapewe nafasi bila kuwekewa vikwazo ili wasiendelee kubaki nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho yake anipe jibu kwenye ombi langu kwani imefika wakati Watanzania wote waende pamoja kielimu. Naunga mkono hoja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya hotuba hii asilimia mia moja. Pongezi nyingi kwa utendaji mzuri wa Wizara katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kwanza, Elimu ya Juu ni budi izingatie ujasiriamali. Watu wapende kazi, wawe na nidhamu katika fani zao *(job ethics).* Daktari ni budi aonekane Daktari, siyo kama ilivyo sasa. *Engineer, Surveyors* na kadhalika hivyo hivyo.

Pili, mazoezi baada ya kumaliza masomo ya Chuo Kikuu yagharimiwe na Serikali, kwa sasa *Engineers* wanahangaika kutafuta ajira ili wapate uzoefu. Ni muhimu hili lifanyike maana siyo vijana wote wanaomaliza vyuo vikuu wanaweza kupata ajira na kujilipia gharama za mafunzo kazini ili kupata uzoefu.

Tatu, jitihada za Serikali kuanzisha vyuo vikuu au *Associated Colleges* ziendelezwe kama ilivyotangazwa na Waziri wa Elimu kama Chuo cha Ualimu Chang'ombe, Mkwawa na kadhalika kuwa Vyuo Vikuu. Hilo lisiishie Wizara ya Elimu na Utamaduni kupanua Elimu ya Vyuo Vikuu indelezwe kwa kujenga vyuo vingine na kupandisha hadhi vyuo kama *College of Business Education (CBE)* na kadhalika. Jitihada zisisimame, kasi iongezeke vijana wanaomaliza elimu ya Sekondari wapate Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache nizidi kukupongeza Wizara kwa kazi nzuri. Asante.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani kwa Serikali kwa kuwadhamini wanafunzi wanaosomea udaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kusomesha Daktari mmoja ni kubwa. Itafaa Madaktari waliopata udhamini wawe *bonded* baada ya kumaliza masomo yao. Wafanye kazi nchini angalau kwa miaka mitatu hadi mitano. Kwa kufanya hivyo tutafikia lengo la Daktari mmoja kwa wananchi 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ongezeko la wanawake katika Taasisi za Elimu ya Juu bado ni ndogo pamoja na juhudi zote zilizoko. Tunahitaji kuweka umuhimu mkubwa katika hili. Aidha, wanawake wahimizwe kuchukua masomo ya sayansi tangu Sekondari.

Tatu, natoa pongezi kwa mipango ya kudahili wanafunzi wa Shahada za *B.Sc. Nursing Management.* Hii ni hatua kubwa ya kunyanyua taaluma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nichangie hoja iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii ya Bajeti kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maandalizi yao mazuri naomba niunge hoja hii mkono kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, napenda nichangie eneo moja kwa lengo la kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia majedwali utaona kuwa Vyuo Vikuu, Taasisi za Elimu ya Juu, maeneo ya Mafunzo ya Kilimo, Maliasili na Mazingira, Mafunzo ya Biashara na Menejimenti, uhandisi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, asasi hizo zote zinajengwa maeneo yale yale kama vile Dar es Salaam, Morogoro, Arusha au Kilimanjaro. Yapo maeneo ambayo yamesahauliwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Serikali iangalie hali hiyo na kuandaa mipango na mikakati itakayofanya Asasi hizo zisambae maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ninalopenda nichangie ni utafiti na teknolojia kwa lengo la kuzalisha mashine mbalimbali au mitambo inayohitajika katika kumwendeleza mwanadamu. Utafiti mwingi mara nyingi unaishia kwenye makabrasha. Kwa sababu tafiti nyingi hazikidhi mahitaji ya Soko *(Demand Drive).* Nashauri kwa mfano pawepo na dhamiri ya kisera, madhalani sekta ya biashara na viwanda, iweke malengo kuwa baada ya miaka mitano hakuna kuuza pamba isiyosindikwa, bali mauzo kwenda nje yawe yamesindikwa kwa kiwango cha nyuzi au vitambaa. Taasisi za utafiti na teknolojia zipewe jukumu la kutengeneza *appropriate technology* ambayo wakulima husika wataweza kuitumia katika mazingira ya wakulima wa pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara sasa iandae mikakati kuhusu namna gani gunduzi au tafiti zilizofanyika zigeuzwe kuwa vitendo.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri na kubwa mnayoifanya katika kusimamia maendeleo ya Sayansi na Teknolojia hapa nchini ikiwa ndiyo njia sahihi ya kuleta maendeleo katika karne hii tulinayo. Hivyo naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha ninayo maoni machache katika kuendeleza na kuboresha shughuli za Serikali Tanzania katika jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafiti wa panya kunusa mabomu ya ardhini pale *SUA,* suala hili linasisimua na lenye manufaa makubwa katika kuokoa maisha ya binadamu kutokana na milipuko ya mabomu yaliyochimbiwa ardhini. Huu ni utafiti wa ukombozi.

Tunashauri wataalam wetu waendeleze utafiti huu kwa kufundisha pia mbwa, siyo kunusa mabomu ya ardhini tu bali kunusa mabomu ya aina zingine na pia dawa za kulevya. Hivi sasa Serikali yetu kupitia Jeshi la Polisi inatumia mamilioni ya fedha kununua mbwa waliofundishwa kunusa mabomu na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, wataalam wetu wa hapa nchini hawaliwezi hili? Wizara ya Mambo ya Ndani tupo tayari kushirikiana na wataalam wao katika kutafiti hili ili tujinasue kutegemea kununua mbwa nchi za nje kwa bei kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti kuhusu Nishati mbadala *(solar energy)* Watanzania wengi nishati yao kuu ni kuni, lakini karne hii ya 21 siyo ya kuni. Lakini umeme hadi sasa umefika. Watanzania 10% tu, tena wa mijini. Itachukua miaka mingi umeme huu *(Hydrol* na *Thermo)* kuwafikia Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya jua *(solar energy)* ingekuwa ndiyo jawabu. Lakini ni jambo la kushangaza kuwa bei za vifaa vya nishati hii ni aghali mno. Wataalam wetu wafanye utafiti zaidi wenye lengo la kuifanya, zana za nishati hii ziwe ndani ya uwezo wa Watanzania wengi kuzinunua na kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki ya Sayansi na Teknolojia Kitaifa, miaka ya 1986 na 1987, Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere, alianzisha wiki ya Sayansi na Teknolojia. Katika wiki hiyo yalifanyika makongamano mbali mbali, wavumbuzi walioonyesha vifaa vinavyovumbua, wanasayansi huko walitambuliwa, na wavumbuzi walipewa tuzo. Wakati ule shughuli hizi zilifanyika Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Mwalimu lilikuwa wiki hii iadhimishwe katika kila mkoa, kama tunavyofanya wiki ya Nane Nane, wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani, wiki ya Wanawake na kadhalika. Lakini suala hili vuguvugu lake hupingwa sana.

Katika malengo ya kazi za Wizara mwaka huu Mheshimiwa Waziri ameweka siku ya Kongamano na Maonyesho ya Wavumbuzi. Ni jambo zuri, lakini wekeni mipango ya kuwa na wiki moja iadhimishe kila mkoa ili wavumbuzi wadogo watambuliwe katika Mikoa yao. Mwalimu alielekeza wiki hiyo iwe mwezi Oktoba kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezwe wosia huo ili kuleta uelewa na *SLT* nchi nzima na kuwaenzi wavumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Uongozi wa Vyuo Vikuu vyetu vyote kwa jinsi wanavyoendesha shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kukazia tu kuwa Wizara iendelee na idumishe mawasiliano na mahusiano yake na wanavyuo wetu ili kutatua matatizo wanayohisi kuwepo na kuyatatua yakiwa bado teketeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Mlimani) hivi sasa wameielewa dhamira na nia safi ya Serikali kuhusu sheria ya kuundwa kwa Baraza la kukopesha fedha wanafunzi wa vyuo vya Elimu ya Juu wanaolazimika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Elimu ya Juu linahitaji kupatiwa mahali pazuri panapokidhi mahitaji ya shughuli yao muhimu. Kiwanja tulikitembelea na kuona kuwa kingewafaa kama tu wangepewa uwezo wa kuendeleza ujenzi wa majengo wanayoyahitaji

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho je, mikopo inalengwa kutolewa kwa baadhi tu ya Taasisi ya Elimu ya Juu na siyo kwa Taasisi zote?

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Ustawi wa Jamii inalia eti haihusiki na mikopo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwuliza Mheshimiwa Waziri hii ni kweli? Naomba jibu na naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji Wakuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuboresha elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa idadi ya vyuo vikuu katika fani mbali mbali ni ishara nzuri ya kuongezeka kwa idadi ya Watanzania wanaopata Elimu ya Juu. Hata hivyo lazima pia tuendele kutoa elimu ya kati kwa wananchi badala ya kuvibadilisha vyuo vyote vilivyokuwa vinatoa elimu hiyo kuwa vyuo vikuu badala ya kujenga vyuo vipya pale inapokuwa lazima.

Mheshimwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa kazi za Wizara hii kwa mwaka uliopita tungependa kufahamu kazi zilizofanyika katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ni majengo yapi yaliyokarabatiwa na ya michepuo ipi *(faculty)* kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi na imefanikisha vipi katika azma hiyo kwa wanafunzi wanaoingia Chuoni hapo kwa mwaka 2004? Mbona mwaka huu 2004 idadi kubwa ya wahitimu waliofaulu vizuri wamekosa nafasi?

Pili, kuanzisha Chuo cha Madini, kutokana na kuongezeka kwa kasi ya uchimbaji wa madini nchini na ushauri uliowahi kutolewa hapa Bungeni juu ya kuliandaa Taifa letu kuwa na wazalendo wasomi katika fani ya Madini inaonekana bado kuna ucheleweshaji wa kutekeleza azma hiyo. Kuna sababu gani za msingi za kuchelewesha kuanzisha Chuo cha Madini Nzega? Hivi ni kweli tunasubiri wenye mgodi wa Nzega wamalize kazi ya uchimbaji ili wakabidhi eneo na vifaa wanavyotumia sasa ili tuweze kuanzisha Chuo cha madini Nzega?

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo tetesi hizi ni za kweli hatuoni kwamba tutaweza kushindwa kuanzisha chuo hicho tukizingatia kwamba upo uwezo wa kugundua Hifadhi mpya ya madini katika eneo husika na kuongeza muda wa utendaji? Ni vyema Mheshimiwa Waziri akatoa maelezo juu ya mpango huu.

Tatu, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, kabla ya kuwa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo hiki kilikuwa miongoni mwa vyuo vichache vya mfano katika eneo la Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umri wa Chuo hicho majengo yake na hata vifaa vilivyopo hadi sasa ni vya zamani, vimechakaa na hata baadhi ya vifaa vyake kupitwa na wakati kiteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendeleza hadhi na sifa iliyokuwepo hasa tukizingatia kwamba nchi nyingine sasa zimeanzisha Taasisi kama hizo na kuzijenga kisasa na kuwa na teknolojia ya kisasa na lazima tuongeze kasi ya kuboresha majengo yakiwemo madarasa, mabweni, maabara na wataalamu ili kuiweka Taasisi hiyo kama mfano bora katika eneo la Afrika Mashariki na ya kati vinginevyo tuliotangulia tutaachwa nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Wizara kwa mwaka 2004/2005 kukarabati maabara na mabweni manne, haitoshi. Kwanza hatuna uhakika kama ukarabati katika maabara hizo utahusisha ununuzi wa teknolojia mpya za kisasa kwa maabara hizo au itaishia katika kukarabati vifaa vilivyopo vya teknologia ya zamani.

Mwisho, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, mkazo uliwekwa katika kusaidia wanafunzi wanawake wanaojitokeza kuingia katika fani ya ufundi. Je, ni wanafunzi wangapi ambao wamesaidiwa kusomeshwa na Wizara hii katika mwaka uliopita kwa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na katika michepuo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa uwasilishaji mzuri wa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia wasaidizi wake akiwemo Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita na Katibu Mkuu, Ndugu Ruth Mollel.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu wa mawazo na ushauri kwa machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni idadi ndogo ya nafasi za Vyuo Vikuu kulinganisha na idadi ya wanafunzi wanaopata alama za kuwawezesha kujiunga na vyuo vikuu. Idadi inazidi kuwa kubwa toka mwaka hadi mwaka, hali inayoonyesha kwamba shule za Sekondari, wazazi na wanafunzi wanajitahidi kufundisha, kuhamasisha na kujifunzia lakini idadi ya wanaopata nafasi inazidi kupungua. Inawezekana tumeongeza idadi ya shule za Sekondari bila kuongeza Vyuo Vikuu. Pia inawezekana tumeongeza idadi ya kuzaa bila kuongeza nafasi za kusomea. Ama tumeelewa maana ya Elimu na sasa tunaongeza jitihada katika kupeleka na watoto shule na kujenga mazingira mazuri ya kujifunzia, bila kuongeza nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kama ifuatavyo:-

Kwanza, watu binafsi na Taasisi zozote zilizotayari kuanzisha na kuendesha Elimu ya Vyuo vikuu, wapewe nafasi bila urasimu.

Pili, nashauri, Serikali iongeze nafasi za Vyuo Vikuu, tatu, nashauri Serikali iongeze bajeti ya kuwasomesha Watanzania wanaopata nafasi katika Vyuo Vikuu vyote kama vya Serikali na binafsi pia.

Nne, Serikali ione uwezekanao wa Ofisi za Ubalozi kupunguza urasimu watoto wetu wanapopata nafasi za kwenda kujisomea nje ya nchi, hasa Ulaya na tano, nashauri Vyuo vingine vya namna nyingine badala ya kufanywa vyuo vikuu, vijengwe zaidi na nishani zake zipewe uzito ili zikubalike katika nchi na nje ya nchi katika Serikali, Taasisi na Mashirika mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja zangu ni kuishauri Wizara iwaenzi wote wenye ubunifu, bila kujali wanagundua nini? Hapa ninatoa mifano, wanaogundua zana za kilimo, ufundishaji, masuala ya sayansi waenziwe sawasawa na wanaogundua uhunzi wa bunduki au bastola. Kugundua uhunzi wa bunduki au bastola, kwangu siyo tatizo, tatizo ni matumizi yake, lakini wagundizi hawa wakipewa nafasi tunaweza kuwa na viwanda vya zana za kivita hapa hapa nchini sioni ubaya. Nalisema hili kwa kuwa wavumbuzi wa uhunzi wa zana hizi huishia jela.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naipongeza Serikali kwa kuwapa nafasi wasichana katika Vyuo Vikuu, nashauri jitihada ziongezwe ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni ili wasichana wahamasishwe kujifunzia kwa bidii na kufaulu elimu ya sekondari katika masomo yote ili kujiongezea nafasi zao katika Vyuo Vikuu na kuziba pengo la wanawake wachache katika nafasi mbalimbali za Kitaifa, Kimataifa na kijamii vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nitumie fursa hii kwa Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Wakuu wa Idara kwa hotuba nzuri ilivyotolewa, ambayo ni matokeo ya ushirikiano wao mzuri. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni moja ya Wizara ambazo hazipigi kelele sana lakini maendeleo yake yanaonekana dhahiri yakionekana katika ongezeko la Wanachuo mwaka hadi mwaka na katika mabadiliko ya miundombinu. Ni imani kubwa vile vile pia tukiwa nayo itakuwa inaendelea vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza watumishi wote wa Wizara hii wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wakuu ambao licha ya kupotelewa na Makatibu Wakuu wao wawili, pia kwa mfululizo hawakutetereka na Wizara kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Wizara imeendelea kuwa imara, Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nguvu. Nampongeza sana Katibu Mkuu, Bibi Ruth Mollel, ambaye naye amefika na kukikalia kiti hicho bila wasiwasi wowote. Tunamtakia kila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba msaada wa maelezo. Hivi sasa kuna wananchi wengi wakiwemo wanaume, wanawake na watoto ambao wanatumia sana simu za mikononi. Naomba kuthibitishiwa tena kama simu hizi kweli hazina mionzi inayoweza kusababisha madhara kwa binadamu. Kama zina mionzi ni madhara yapi yaliyopo ya muda mfupi na mrefu kwa binadamu? Zipo tahadhali zipi ambazo binadamu/mtu anaweza kuzichukua ili asiathirike au apunguze athari za mionzi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizidi kuipongeza Wizara hii kwa kuongeza wanachuo katika vyuo vyake na kuwawezesha wanachuo hata wale ambao wazazi wao hawana uwezo wa kusomesha watoto wao kuendelea na masomo hadi kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo bila kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi Taifa haliwezi kuendelea, hivyo kinachofanywa na Wizara hii ni kitendo cha maendeleo. Serikali kupitia Wizara hii iendelee kujijengea uwezo wa kusomesha watu wake zaidi, wazo la awali tunategemea zaidi kutoka kwa Wizara hii. Tunaamini wazo litakalokuwa na uelekeo huo wananchi hawatasita kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kuomba Wizara hii iendelee kutafuta uwezo wa kuendeleza tafiti mbali mbali za hapa nchini au kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kutumika au kuleta maendeleo katika nchi yetu. Teknolojia yetu wenyewe ndiyo itakayotuwezesha kwenda mbele mapema na kwa haraka zaidi na hivyo kutuondoa katika dimwi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kupitia Wizara hii ni vyema Mashirika kama *CAMARTEC, TIRDO* na viwanda mbalimbali na Mashirika mengine yanayofanya tafiti mbali mbali vikafanya kazi kwa pamoja ili kiasi cha fedha kilichopo kiweze kufanya kazi moja inayoonekana badala ya kugawana kidogo kidogo na kazi au matokeo ya kazi yao mmoja mmoja isiwe na manufaa makubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapig kura na wananchi wa Jimbo la Kwimba, naunga mkono hoja.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu wake na wataalam wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya japo wanafanyia kazi ndani ya mazingira magumu na Bajeti finyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

Kwanza, kama ambavyo Serikali imeona kwamba hivi sasa ni wakati muafaka wa kutoa ruzuku kwa Shule za Sekondari binafsi, je, Serikali ina mpango gani wa kufanya hivyo hivyo kwa wamiliki wa Vyuo Vikuu binafsi?

Pili, Wizara imefikia wapi katika kuhakikisha inakisaidia Chuo Kikuu cha Bukoba ili kiweze kuendelea na mpango wake kama ulivyokuwa umepangwa? Je, vikwazo vilivyojitokeza katika uanzishwaji wa Chuo hicho Serikali inasaidiaje katika kuviondoa hivyo vikwazo ili Chuo hicho kiendelee? Kwa kuwa wazo la kuwepo Chuo hicho ni zuri, Serikali naiomba iingilie kati kuhakikisha Chuo hicho kinaendelea kuwepo kwani ni faida kwa nchi nzima.

Tatu, Serikali ina mpango gani wa kuwapa fursa au kuwatengenezea mazingira yaliyo bora zaidi waganga wa jadi kuliko ilivyo sasa ambapo wanafanya kazi zao kwa kujificha au kwa kuhofia urasimu uliopo Serikalini au kutofaidika na chochote endapo dawa zao zitaonekana zinafaa katika kutibu magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kwa kiasi gani Serikali imefuatilia ukweli kwamba wapo watu wenye uwezo wa kusafiri angani kwa nyungo na kutua mahali popote pale kama ambavyo imekuwa inatolewa taarifa na baadhi ya vyombo vya habari?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ukweli huo upo basi watu hao Serikali itoe tamko la kuwaondolea woga ili wajitokeze na kuwekeza katika sekta ya usafiri huo ulio rahisi na usiotumia gharama kubwa.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za Waziri Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu katika kupanua na kuboresha Elimu ya Juu zinaonekana wazi kwa kila mtu mwenye nia njema. Natoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ndiyo nchi ya mwisho katika Afrika kwa kuwa na idadi ndogo ya wanafunzi katika Vyuo Vikuu. Hivi sasa wanafunzi walio na sifa za kujiunga na Vyuo Vikuu ni wengi kuliko uwezo wa Serikali wa kuwapa nafasi ya kusoma katika Vyuo Vikuu hivyo. Kwa mfano, mwaka 2004 vijana 6,000 wameomba kujiunga na Chuo Kikuu cha Mzumbe. Zaidi ya nusu ya vijana hao wanavyo vyeti vya kidato cha VI daraja la kwanza. Lakini Serikali imetoa nafasi kwa vijana 250 tu vijana 5,750 wametupwa nje. Hivyo hivyo katika vyuo vingine hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kufanya mambo mawili, kwanza Serikali iongeze Bajeti ya Wizara hii. Ongezeko lolote katika mapato ya nchi kutokana na makusanyo ya kodi yaelekezwe katika Wizara hii ili kuongeza nafasi za wanafunzi katika Vyuo Vikuu.

Pili, Serikali, haraka iwezekanavyo, ianzishe *Education Development Levy* ambayo kila Mtanzania achangie. Hili siyo jambo la mzaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule utaratibu uliokuwa unaandaliwa wa kuwapa mikopo wanafunzi umefikia wapi? Serikali iharakishe kutoa mikopo kwa wanafunzi. Naunga mkono hoja ya Waziri.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, amemwomba Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwamba Pemba kiwekwe Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zinafanywa, si kwa kufungua Chuo Kikuu, lakini Vyuo Vikuu vilivyopo vinataka kuhudumia Pemba kama vile Chuo Kikuu Huria kimefungua Tawi Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, si rahisi kila mmoja adai Chuo Kikuu katika Jimbo lake. Mimi wa Lushoto ndiye nipewe kipaumbele, maana mandhari yake ni bora sana.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba nianzie na mchango wangu huu kuwashukuru Waziri Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Ng'wangu na Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa juhudu zao kubwa na ushirikiano waliokuwa nao katika kuziendeleza kazi ngumu walizokabidhiwa kwa niaba ya Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niwashukuru kwa juhudi zao na ushirikiano wao katika kufanikisha maendeleo ya ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kudumisha Muungano wa nchi zetu zilizounda Muungano huo. Suala la Elimu ya Juu, ikiwa ni jambo la kwanza kuwa ni la Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi niliyoshuhudia katika kipindi changu hiki ni ya aina yake. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri ina watendaji wao wote kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa juhudi imeanza zamani, lakini hivi sasa matokeo yake yapo wazi kabisa katika kuliimarisha suala la Elimu ya Juu kule Zanzibar kama ilivyo Tanzania Bara. Cha dhahiri hivi sasa Zanzibar kuna Vyuo Vikuu vinne vinavyotambulika baada ya kufanikiwa masharti ya kuwa vyuo chini ya taratibu tulizojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu za ziada ni kule kufanikisha kwa upatikanaji wa fedha za ujenzi wa Taasisi ya Sayansi za Majini *(Institute of Marine Sciences)* kule Buyu, Zanzibar. Kwa kweli mambo ni poa kabisa. Hivyo, ninawaahidi kuwa mimi binafsi nitashirikiana na Wizara hii kwa kadri ya uwezo wangu niliopewa kuona kuwa tunazidi kufanikiwa kwa kila hali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile mchango wangu mkubwa ulikuwa katika Kamati iliyojadili Wizara hii, hivyo sina zaidi ila kuiomba zaidi Wizara na Serikali kukipangia fedha zaidi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa vile mambo yamewazidia na lengo lao ni la mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuiomba Serikali kulifikiria suala la utafiti. Fedha za utafiti ni haba mno, hazitoshi hata chembe. Hebu tulizingatie suala la kutenga asilimia moja ya pato la nchi kwa kudumisha utafiti, kama kweli nchi hii inatakiwa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia. Ninaamini kwa kufanya hivyo, umaskini utaondoka na taaluma itafika vijijini kwa utekelezaji wa matokeo ya utafiti huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu haya, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi za dhati kwa kazi mnayofanya. Napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

(1)(a) Kwa vile gharama za Chuo Kikuu zimeendelea kupanda na kwa kuwa vita dhiti ya umaskini ni ndoto iwapo hatutaweza kuwaelimisha vijana wetu katika ngazi ya Chuo Kikuu. Sasa hivi uwiano wa wataalam wetu katika nyanja kadhaa unatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ilipe gharama za Chuo Kikuu na kufanya upendeleo maalum katika nyanja husika, mathalan Udaktari, *Engineering,* Wataalam wa Utafiti na nyanja mbalimbali. Vigezo vya uteuzi viandaliwe kwa umaskini, kwa mfano, *special scholarships,* vinginevyo, kamwe hatutapiga wala kushinda vita dhidi ya umaskini.

(b) Wizara iwasiliane na *Line Ministries* kujua maeneo ya kipaumbele ili tuweke nguvu zetu pale panapohitajika zaidi.

(2) Naomba Waziri wakati wa kuhitimisha, anifafanulie kwa kina suala la Chuo Kikuu cha Zanzibar, limefikia wapi? Sheria husika zimerekebishwa au nini nafasi ya Muungano katika Chuo Kikuu cha Zanzibar, ikizingatiwa kuwa suala hili ni la Muungano na ni la Kikatiba? Naona mambo yameenda kimya kimya tu.

(3) (a) Utafiti ni silaha moja kubwa katika mapambano dhidi ya umaskini na hata kufanya au kupiga hatua kubwa katika nchi kuendelea. Nasikitishwa sana na kiwango cha fedha kinachotengwa na Serikali katika ujumla wake kwa ajili ya utafiti wa vyuo na hata kwenye Taasisi mbalimbali chini ya Wizara nyingine. Je, Serikali itachukua hatua madhubuti lini na kufanya utafiti kuwa kipaumbele muhimu? Tafiti ndogo katika randama za Bajeti za Wizara mbalimbali zinaonyesha kuwa semina, warsha na mikutano imepangiwa jumla ya shilingi bilioni 7.9. Je, ni kweli kuna dhamira ya nchi yetu kuendelea mbele iwapo semina na warsha zinapewa kipaumbele kuliko utafiti?

(b) Kwa vile Wizara hii ndiyo yenye jukumu la kukuza na kuendeleza Sayansi na Teknolojia, ni lini Serikali itaweka uratibu wa Tafiti na Idara au vitengo mbalimbali vya utafiti chini ya usimamizi wa Wizara kwa ajili ya *coordination* nzuri zaidi, kupanga raslimali vizuri zaidi na matumizi na hasa *distribution* ya matokeo ya tafiti hizo?

(4) Ni lini sasa Serikali italeta mapendekezo ya sheria ili wafanya biashara wanaochangia Mfuko wa Elimu na mifuko mingine ya aina hiyo inayohusu huduma za jamii wapate msamaha wa kodi kama wanavyofanya wenzetu katika nchi zilizoendelea? Waziri anafahamu kuwa watu wengi wana nia ya kuchangia maendeleo ya nchi yetu, lakini hawapati vivutio vya kufanya hivyo. Je, Waziri anakubaliana nami kuwa kuna haja sasa ya kufanya mabadiliko makubwa ya kisheria katika eneo hili ili kuwa motisha kwa wananchi na wafanyabiashara kuchangia kwa kiwango kikubwa?

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali kabisa napenda kumpongeza kwa dhati kabisa kwa juhudi anayofanya Waziri na wataalam wake katika kubuni sera mbalimbali zinazohusu Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udhamini wa Serikali kwa Wanachuo wa Vyuo Vikuu, nitapenda kuipongeza Serikali kwa juhudi inayofanya katika kuwadhamini Wanachuo Vyuoni, hasa wale wanaotoka katika jamii maskini. Nashauri kwamba kwa kuwa vijana wengi wanaoomba udhamini, wanaenda kuishi vijijini, ni vyema taratibu zinazofuatwa katika kuwapata vijana hao, zieleweke vizuri kwa Viongozi wa Wilaya, Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Wizara au Vyuo vinavyohusika waweke taratibu wa kuwashirikisha viongozi wa ngazi hizo ili kuwapata waombaji wanaostahili tu. Wapo vijana ambao wanapata alama nzuri katika mitihani na wanatoka katika familia maskini sana, lakini wanashindwa kupata mikopo hiyo na hivyo kushindwa kuingia vyuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu kwa wadau kuhusu uchangiaji wa Mfuko wa Elimu, kazi iliyofanyika kwa wadau mbalimbali na Waziri wa Sayansi,

Teknolojia na Elimu ya Juu. Nashauri kwamba ni muhimu elimu hiyo iendelezwe sasa hadi vijijini. Uandaliwe utaratibu sasa na viongozi wa mfuko, wakishirikiana na viongozi wa Mikoa na Wilaya, kuendeleza elimu hiyo hadi vijini na kuanza kuwaomba wananchi kuhamasika zaidi na kuanza kuchangia. Ufuatiliaji sasa unahitajika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naungana na Waziri kwa hotuba yake nzuri na naiunga mkono kwa asilimia mia.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara hii. Nasema hongera, hongera sana kwa kutoa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii kwa kuongeza kuomba kuwa Serikali iweze kujenga Chuo cha Ualimu cha Stashahada katika eneo la Mgodi wa Mwadui, kwani miundombinu katika eneo hilo ni kubwa na wa kutosha kabisa. Aidha, kilichokuwa Kiwanda cha Nyama Shinyanga, ambacho hakijaisha kwa muda mrefu, kijengwe Chuo cha Madini ili kiwe karibu na Mgodi wa Mwadui kwa lengo la kufanya utafiti wao. Mkoa wa Shinyanga na Taifa letu kwa ujumla, litaongeza uwezo wa kuwa na wataalam wazuri na wenye fani za kutosha. Naomba hili lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoani Shinyanga, basi uwepo mpango mahsusi wa kujenga jengo la Chuo Kikuu Huria ili kuwa mfano kwa mikoa mingine. Hii italeta changamoto kubwa kwa kuinua na kupanua wigo wa Elimu Mkoani Shinyanga. Naiomba Wizara na Serikali kuliona hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na kusisitiza kuwa uwepo mpango wa dhati wa kupanua zaidi/kuongeza mikondo katika Shule ya Wasichana ya Maswa ili iweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi kila mwaka badala ya kuanza kujenga shule nyingine mpya. Aidha, kuwe na *combination* nyingi za kuweza kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya. Pia pongezi nyingi kwa kuhamia kwenye jengo bora lililokarabatiwa hivi karibuni. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu jinsi anavyotarajia ku-*keep standards* za *degress* za *UDSM,* ambapo moja kati ya matakwa *(requirements)* ni kufanya mafunzo ya vitendo *(practical training)* kwa wanafunzi kwa wiki *(weeks)* zilizopangwa? Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba wanafunzi watafanya wiki mbili au pungufu ya muda uliopangwa kulingana na viwango vya elimu wanayotakiwa kuipata kwa digrii wanasomea!

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Waziri ana mpango gani wa kuendeleza uandaaji wa Walimu/Watafiti ndani ya vyuo vyenyewe kama ilivyokuwa awali? Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba kama *UDSM* wameweza kufikia karibu 100% ya *Ph.D.,* miongoni mwao kwa utaratibu huo badala ya kutumia utaratibu wa sasa wa kutangaza ili kupata watu wenye sifa ambapo aghalabu ni vigumu kuwapata kutoka uraiani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wa *phasing-out* ya wanafunzi wa ufundi, biashara, na kadhalika katika *O-Level,* je, vyuo kama vile *Technical Colleges* na kadhalika, vitapata wapi wanafunzi katika siku za usoni? Hivi kweli kulikuwa na mawasiliano baina ya Wataalam wa Wizara ya Elimu na Utamaduni na wale wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kiasi cha Wizara ya Elimu na Utamaduni, kufikia uamuzi huu wa *phasing-out* ya elimu maalum katika *O-Level?*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ili nichangie katika hotuba hii. Nianze kwa kumshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri sana wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, Wizara hii pamoja na kuomba pesa walizozitaja, ni kidogo mno kulingana na umuhimu wa Wizara. Hata hivyo, kutokana na uwezo wa Serikali, nakubaliana na ombi lao hilo na naunga mkono 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kumpongeza Waziri kwa kupanua Elimu ya Juu kwa kukubali Chuo cha Ushirika Moshi kiwe Chuo Kikuu Kishiriki cha *SUA.* Hii itaongeza wataalam wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuviinua vyuo mbalimbali, amezungumzia pia Chuo cha Ufundi Mbeya kuboreshwa na baadaye kuwa Chuo Kishiriki cha Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri na kuiomba Serikali kupitia Wizara hii, iangalie uwezekano wa Chuo cha Kilimo Ukiriguru kuwa Chuo Kikuu Kishiriki. Hii itasaidia kuongeza wataalam ambao watasaidia kuinua na kuboresha uzalishaji wa mazao nchini na kuliokoa Taifa katika janga la njaa. Ikumbukwe kuwa nchi yetu inategemea kilimo kama uti wa mgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwa Waziri aone umuhimu wa Chuo hicho cha Ukiriguru ili nacho kiwe sehemu ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kumpongeza Waziri kwa kuzidi kutoa elimu yeye mwenyewe kuhusu Mfuko wa Wanafunzi. Jamii inazidi kuelewa. Naomba juhudi za kuelezwa, uongezewe nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha, kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa hotuba yake nzuri na ya kuvutia na pia ya kutia moyo, ambayo ameitoa asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada zake katika kuimarisha Elimu ya Juu. Kipekee naipongeza Serikali kwa msimamo wake wa kuimarisha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania *(OUT) (U).*

Hata hivyo, kufuatia majukumu yaliyotolewa kwa *OUT,* kiasi cha shilingi 244,341,100/= kama ilivyoonyeshwa katika Kiambatanisho Na. 6 kama mgao wa fedha 2003/2004 kutoka Mfuko wa Elimu, ni kidogo mno hasa ikizingatiwa kuwa tumeanza kupanua mipango yetu ya Elimu ya Msingi (MMEM) na ile ya Sekondari (MMES).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema upanuzi huo uende sambamba na upanuzi wa mipango yetu ya Chuo Kikuu *(OUT) (U)* ili tutakapoanza kupata matunda ya mipango hiyo, *OUT* iwe tayari kuwaendeleza wale wote ambao watahitaji kupata Elimu ya Chuo Kikuu. Nashauri Serikali iongeze kiasi kinachotolewa kwa *OUT* ni kidogo mno na hakiendi sambamba na matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Jimbo langu la Siha lipo tayari kupitia wadau mbalimbali na taratibu zilizowekwa za kutafuta mahali ambapo *OUT* inaweza kuanzisha kituo chake ili huduma zake ziweze kuwafikia wananchi walio wengi na kwa urahisi zaidi. Naupongeza uongozi na watendaji wote wa *OUT* kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naahidi nitatoa ushirikiano wangu wote kwa chuo hiki muhimu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Naibu Waziri Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kwa namna moja ama nyingine kuandaa mpango mzuri wa bajeti hii yenye lengo la kuinua taaluma ya Watanzania wenye nia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia Bajeti hii, napenda nitamke rasmi kuwa naunga mkono Bajeti kwa asilimia mia kwa mia. Ninawatakia utekelezaji mwema na kuendeleza mshikamano wao kama ilivyo desturi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kufungua Matawi ya Vyuo Vikuu Huria Mikoani na kadhalika. Hiki ni kitendo cha maendeleo kwani wananchi wengi sasa wameamua kujiunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ihakikishe inafungua Maktaba Mikoani ili wananchi wanaojiendeleza kwa kutumia vituo hivi, wapate mahali pa kupata *material* yanayohusiana na masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuwa mstari wa mbele kuwasaidia kuwalipia ada wanafunzi wanaofaulu kujiunga na masomo ya Chuo Kikuu,

wenye wazazi/walezi wasiokuwa na uwezo. Serikali iwafikirie wanafunzi wanaojiunga na vyuo hivi kwa udhamini binafsi *(private sponsored),* kwani wengi wao wazazi wao hawana uwezo, ingawa huwa wana nia ya kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naiomba Serikali iwe inazitangaza nafasi za masomo nje ya nchi kwa njia ya magazeti, redio na vyombo vingine vya habari, ili wananchi wengi wenye nia ya kusoma wapate habari kwani wengi wao wanakaa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali pamoja na jitihada yake kubwa ya kupanua wigo wa Elimu ya Juu, naiomba iongeze idadi ya Vyuo Vikuu kwani ardhi na nia ipo, hali ambayo itawasaidia Watanzania wengi kupata nafasi humu humu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwani imekuwa macho na makini katika kutuliza migogoro ya wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu kila inapotokea. Naiomba Serikali ifanye uchunguzi wa kina katika kutafuta vyanzo vya migogoro na kutafuta suluhisho kwa kushirikisha wadau mbalimbali, tukiwemo sisi Wanasiasa. Nina hakika hali hii itakuwa imefika ukomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itoe muda wa kutosha wa mazoezi *(field attachment)* kwa wanafunzi, ili wanapomaliza wawe wameiva vya kutosha katika masomo yao na kuwasaidia katika ajira zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, naomba nirudie kuwapongeza na kuunga mkono hoja hii kwa asilimia zote 100.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hakika hotuba hii ni nzuri, imeeleza shughuli zake wa ufanisi, utekelezaji wenye mafanikio na malengo yenye dira ya maendeleo kwa kizazi hiki na cha baadaye. Bila kigugumizi, nasema naunga mkono bajeti hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na maombi ni kwamba uteuzi wa wanafunzi kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ardhi na kadhalika unalalamikiwa na watoto na wazazi wao kwa sababu vigezo vya uteuzi havipo wazi. Kwa hiyo, vigezo gani vinatumika? Waelimishwe wananchi kwenye vyombo vya habari na magazeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wanafunzi hushindwa kuteuliwa kwa vile chaguo lake *(combination)* ya masomo aliyotarajia kufaulu vizuri kashindwa. Lakini anafaulu vizuri *combination* nyingine. Je, Serikali haioni kuwa ni vema kuwa na kitengo maalum cha kuchanganua matokeo ya wanafunzi wa aina hiyo ili wazazi wawe na imani na utaratibu wa uteuzi wa wanafunzi hasa wale wanaopata *division one* na hawateuliwi kujiunga na Chuo Kikuu na hawapewi maelezo ya kutoteuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhamisho, kuna utaratibu gani kwa wanafunzi wanaougua kupewa uhamisho kwa shule au chuo kingine, ili wazazi wasilazimike kufuata watoto wao mashuleni na kuwagharamia wenyewe nauli na matibabu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usajili, nimeshangazwa kuona *Buhare Community Development Training Institute,* Musoma, ina usajili wa muda, wakati chuo hicho ni cha miaka isiyopungua 37. Je, nani anawajibika kuhakikisha vyuo vya umma vinasajiliwa na kupata usajili? Inachukua muda gani tangu kuanza kazi zake au ni kabla ya kuanza kazi zake?

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uongozi wake mzuri katika Wizara yake. Vile vile nawapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara yake kwa ushirikiano wao na kumsaidia. Hii imejionyesha kwa maandalizi ya hotuba yake ambayo ni nzuri, inayojieleza vizuri. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *The Higher Education Students Loan Board,* bodi ya kuwakopesha vijana wetu ili wasome, ifafanuliwe vema kwa wananchi. Wengi hata sasa wananung'unika kwamba walionacho wanataka watoto wao tu wasome, waelezwe kwamba hati za nyumba zao au za mashamba yao hazitapotea. Naomba mafunzo hayo yawafikie wanafunzi wa Kidato cha V na VI. Kwa kuwa hao wakielewa, elimu hiyo itawafikia wazazi wao kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kukarabati Chuo cha Mbeya. Lakini naomba jitihada ya kuendeleza chuo hicho, iongezwe zaidi ili chuo hicho kipate hadhi ya kuwa Chuo Kikuu cha Ufundi. Marehemu Mwalimu Julius Nyerere, alitaka hivyo. Sasa hivyo ndivyo Hayati Baba wa Taifa alitaka. Nini kinatukwamisha? Namwomba Mheshimiwa Waziri akawasiliane na Halmashauri ya Mji Mbeya au Mkuu wa Mkoa au Waziri wa Ujenzi, mjenge barabara ya kwenda kule chuoni kwa sababu wananchi wanaingilia eneo la chuo. Mipaka ionyeshwe na uzio ujengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ya wanafunzi 9 katika Vyuo vya Ufundi kutoka 10 kwenda 19 si ya kujivunia, kulikoni? Mwakani, Mheshimiwa Waziri aongeze zaidi, aombe fedha, tutamuunga mkono. Tunahitaji mafundi wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri awasilishe haraka Bungeni *Bill* ya Elimu ya Juu (Vyuo Vikuu), ya kuanzisha mfuko wa utoaji wa huduma kwa wateja, kwa kukamilisha Mkataba wa Hiari wa utoaji huduma. Utendaji wa kazi katika nchi yetu una shida nyingi. Kukiwepo na sheria ya kuwawajibisha watu wasiojituma, kutapunguza matatizo mengi na nchi itasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani na pongezi kwa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa kazi nzuri za kila siku. Pongezi kwa Wakuu wa Vyuo Vikuu na Makamu wa vyuo hivyo, kwa uvumilivu na kuhimili vishindo vya matukio ya vurugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu chanzo cha vurugu katika vyuo. Vyuo Vikuu vyetu ni sehemu ya eneo la wasomi. Hivyo, Watanzania tunategemea mshikamano na utulivu wa hali ya juu. Pale inapotokea vurugu, sisi hushangaa sana. Nini hasa chanzo cha migogoro ya vyuo kati ya wanafunzi wa chuo hadi chuo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuhamia Dodoma, hapo awali Wizara hii haikuwa na Ofisi, ilitumia iliyokuwa Makao Makuu ya Msajili wa Majumba iliyoko Mtaa wa Jamhuri, Dar es Salaam. Baadaye Wizara ikahamia Mikocheni katika eneo la *TIRDO.* Hivi sasa wanakarabati jengo lile lile la zamani.

(a) Kwa nini hamkuomba nafasi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuweka ofisi zenu au *UCLAS,* ambazo kuna nafasi nzuri ya kuwa pamoja na wanafunzi?

(b) Kwa nini msinunue jengo la *TPB* la Dodoma, likawa lenu kabisa, badala ya kuwa na maisha ya kuhamahama?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira mpya, kama kuna ajira mpya katika Wizara hii, naomba waajiriwe *fresh from University, students* wanaomaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuendeleza Utafiti. Wizara isione kigugumizi juu ya kuendeleza utafiti, uvumbuzi, ugunduzi na uundaji wa zana za kisasa. Hivyo basi, Chuo/Kitivo cha Uhandisi kishirikiane na *TEMDO, TIRDO, CAMARTEC, TBS, NYUMBU* ili kutoa tafsiri nyepesi kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mishahara ya Maprofesa. Kuwe na tofauti ya maandishi ya Shahada za *Doctorate* wote. Naona wanatumia *Dr.* halafu jina lake. *Dr.* itumike tu kwa *Medical Doctor. Ph.D.* iandikwe *DR.* herufi kubwa kwa waliopitia ngazi ya *1st, 2nd and Ph. Degree.* Lakini kama ya heshima tu, iandikwe *dr.* herufi ndogo.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Ardhi wakati wanafunzi wake wanapofanya mazoezi ya vitendo, huwa wanakwenda katika miji na vijiji mbalimbali katika Tanzania. Kwa vile katika kazi hizo wanafunzi hao hufuatana na Walimu wao, hivyo kazi ya upimaji na upangaji miji hufanyika kitaalam pamoja na kushirikisha mawazo ya wananchi wa maenedo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni mara chache sana kazi hizo hurudi katika miji au vijiji husika ili kuendelezwa, na badala yake hubakia katika maktaba za chuo na hufanya kazi za utafiti tu kwa vile kazi hizo zinagharimu fedha nyingi. Serikali ingeandaa utaratibu mzuri na unaoeleweka ili kazi hiyo muhimu iweze kusaidia maendeleo na upangaji bora wa miji na vijiji vyetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi ya Baharini pamoja na umuhimu wa taasisi hiyo, lakini kwa sasa wanashindwa kuendeleza tafiti za baharini kwa vile hawana vifaa vya kuwawezesha kufika baharini pamoja na vifaa vya utafiti. Hivyo, ni vyema Serikali ikasaidia ufumbuzi wa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuongoza Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isaidie kuwezesha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, barabara ya Sangasanga hadi Mzumbe (Chuo Kikuu cha Mzumbe).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wengi sana wanakosa kujiunga na Vyuo Vikuu kwa kupata *grade* za chini katika masomo yao ya Kidato cha Sita. Hali hiyo hupunguza idadi ya wanafunzi ambao wangejiunga na Vyuo Vikuu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mwanafunzi aweze kujiunga na Chuo Kikuu, ni lazima apate alama A, B, C, na D katika masomo mawili na kuendelea. Wanafunzi ambao wanapata alama "E" katika masomo yao, hawapati nafasi hizo. Hali hiyo ni kuwanyima haki wanafunzi hao ya kupata elimu ya juu. Naomba Serikali ikalegeza hali hiyo ili wanafunzi wenye alama "E" katika masomo yao nao waruhusiwe kujinga na Elimu ya Juu katika Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo hapo juu inawaathiri sana wanafunzi wa masomo ya Sayansi hasa wasichana. Mara nyingi wanafunzi wa masomo ya Sayansi hawapati alama za juu kutokana na ufundishaji katika shule zao kuwa siyo nzuri sana. Hata hivyo, wanafunzi wenyewe huweka bidii katika masomo yao hadi kufanikiwa kupata alama za "E" katika masomo hayo.

Hivyo, ningeomba wanafunzi ambao wanapata masomo mawili yenye alama "E" nao wakaruhusiwa kujiunga Elimu ya Vyuo Vikuu, kuliko ilivyo sasa ambapo wanafunzi hao hawaruhusiwi. Hali hii ni kwa kutambua kuwa katika Vyuo Vikuu, mwanafunzi huchukua somo moja au mawili ili kupata shahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa wanafunzi wanaopata alama za "E" katika masomo yao hawawezi wakachaguliwa moja kwa moja, basi angalau waruhusiwe kufanya mitihani ya majaribio ya kujiunga na Elimu ya Vyuo Vikuu. Hii itakuwa ni kuwapa nafasi nyingine wanafunzi hao ya kujaribu tena kupata masomo hayo. Inawezekana wapo ambao hawakuwa tayari kufanya mitihani wakati wa mitihani yao, ndiyo maana walipata alama za chini. Kwa kupewa nafasi ya kufanya mitihani ya majaribio, inawezekana wanafunzi hao wakafanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, naomba Serikali ikawapa nafasi hiyo wanafunzi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa asilimia mia moja.

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kuzungumza, naomba kwa niaba ya Wanawake wote wa Mkoa wa Dodoma na kwa niaba yangu mwenyewe niwaunge mkono wale Wabunge wote ambao wamepata maafa mbalimbali na hasa kwa familia ya wananchi wa Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego.

Aidha, ningependa nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa ushirikiano wake na uongozi wake thabiti ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu tuliyopewa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri, ningependa nitamke kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nianze kwa kuchangia hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu. Hoja hii imewasilishwa na Mheshimiwa Margareth Mkanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni mojawapo ya uanzishwaji wa Vyuo Vikuu pamoja na Taasisi ni kuwepo kwa miundombinu kwa ajili ya walemavu. Wizara yangu inafuatilia kwa makini kuhakikisha kwamba Vyuo vyote vinatekeleza kanuni hiyo kwa ukamilifu ili kutoa nafasi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa aina mbalimbali waweze kupata nafasi za masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya walimu wenye sifa na dira mpya pia kuzingatia ongezeko la mahitaji ya wanafunzi, viwango vya ubora vya walimu wa Vyuo na Taasisi zimewekewa mabaraza husika. Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu na Baraza la Elimu ya Ufundi pamoja na Vyuo vyenyewe. Aidha, kuna mipango na mikakati ya kuendeleza walimu, kuboresha viwango vyao hadi Udaktari wa Falfasa

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja kuhusu fedha kwa ajili ya Taasisi za Elimu ya Juu Zanzibar hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali. Utaratibu wa bajeti kwa taasisi zilizo chini ya Serikali ya Muungano hufanyika kupitia Bunge la Muungano lakini hata hivyo Vyuo vilivyopo Zanzibar vinaweza kuomba fedha kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya kuhusu usajili wa muda uliopewa *Buhare Community Development Training Institute,* Musoma. Wakati chuo hiki kimekuwa kikitoa mafunzo kwa miaka isiyopungua 37. Mheshimiwa Mbunge aliuliza nani anayewajibika kuhakikisha kuwa vyuo vya umma vinasajiliwa na usajili kamili unachukua muda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu ya Mheshimiwa Esha Stima, kwamba Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ndilo lenye jukumu na kuratibu, kusajili na kutoa Ithibati kwa vyuo vya ufundi vyenye uwezo na kutoa mafunzo yenye ubora kwa viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili wa vyuo uko katika hatua tatu ambazo ni ya kwanza, usajili kamili hutolewa kwa vyuo vilivyokamilisha masharti yafuatayo:-

Miundombinu inayofaa kwa ajili ya mafunzo, walimu na wataalam wenye sifa zinazokubalika, vifaa vya kufundishia ikiwa pamoja na maktaba, mitaala iliyokidhi mahitaji ya soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili wa muda hutolewa kwa mbinu ambavyo vina mapungufu katika uwezo wa kutoa mafunzo.  Kwa usajili huu Chuo kinatakiwa kurekebisha mapungufu hayo katika muda wa miaka miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna mfadhili wa awali hutolewa kwa vyuo ambavyo vinaanzishwa au vyuo ambavyo havina uwezo wa kuendesha mafunzo kwa usajili huo.  Vyuo haviruhusiwi kupokea wanafunzi. *Buhare Community Development Institute* kimepewa usajili wa muda kwa sababu kimeonekana kuwa na mapungufu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kina upungufu mkubwa wa walimu wenye sifa zinazokubalika, mitaala inayotumika kufundisha imepitwa na wakati na maktaba haina vitabu vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja kuimarisha Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Chuo Kikuu.  Hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na mwisho imechangiwa vile vile na Mheshimiwa Benson Mpesya.

Napenda kupokea ushauri wa Kamati ya Huduma za Jamii ya Waheshimiwa niliowataja, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Rhoda Kahatano na Mheshimiwa Paul Ntwina, kuhusu namna ya kuimarisha Chuo cha Ufundi Mbeya hatua kwa hatua kwa kukipatia wataalam wenye sifa na vifaa ili hatimaye kiwe Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulithibishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu itaendelea na juhudi zilizokwisha anzwa za kukiimarisha Chuo hiki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwaajiri walimu wapya na kuwaendeleza wale waliopo kwa kuwapatia mafunzo ndani na nje ya nchi ili wapate sifa zinazotakiwa na hii imekwishaanzwa, kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika maabara na karakana.

Napenda nimthibitishie Mheshimiwa Paul Ntwina na Mheshimiwa Benson Mpesya na wananchi wa Mbeya kwa ujumla kwamba Wizara yangu itaelekeza yale iliyoahidi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara inayoelekea Chuoni kutoka barabara kuu iendayo Zambia tayari Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya imekwishaagiza barabara hiyo katika mpango wake na tayari imekwisha ingiza barabara hiyo katika mpango wake wa kujenga barabara hiyo katika kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Chuo kitatoa lami ambayo tayari ipo chuoni kama mchango wake katika kuharakisha na kufanikisha ujenzi wa barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la hati ya kumiliki eneo lililotengwa kwa ajili ya chuo, tayari chuo kimeshapatiwa *offer* na taratibu zinaendelea ili kupata hati miliki. Aidha, mipaka ya eneo la Chuo lililokwishapimwa na kulipiwa fidia imewekwa bayana. Wizara yangu itafanya jitihada za kutafuta fedha ili kuliwekea uzio eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa pia kuna hoja ya ukarabati wa miundombinu ya uingizaji wa teknolojia mpya na idadi ya wanafunzi wa kike katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi imeweka mikakati mbalimbali ili kuboresha miundombinu yake. Taasisi imepata fedha kutoka Mfuko wa Elimu na nchi fadhili za Sweden, Japan, Korea na China ili kununua vifaa vya kisasa vya teknolojia na mawasiliano na ukarabati wa miundombinu kwa kupitia *SIDA,* Taasisi itanunua kompyuta 200 kwa mwaka 2004/2005. Taasisi tayari imekamilisha *local area network* na itaunganishwa kwenye *internet* katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 kutokana na ufadhili wa *SIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zote hizi ni juhudi za kuifanya Taasisi hiyo kuwa mfano katika Afrika Mashariki na Afrika ya Kati. Aidha, Wizara ikishirikiana na Taasisi inafanya juhudi kuwasiliana na wadau wengine ili kuipatia Taasisi hii teknolojia ya kisasa inazingatia mabadiliko ya soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wa kike waliodhaminiwa na Wizara katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na fani zao katika mwaka wa fedha 2003/2004 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhandisi Ujenzi, mwaka 2003/2004 walikuwa wanane, Uhandisi Mitambo hapakuwa na msichana, Uhandisi Umeme 11, Uhandisi Barabara hapakuwa na msichana, Mhandisi Mawasiliano Angani 19, Sayansi ya Teknolojia za Maabara watano na masomo ya kompyuta wanafunzi wa kike 7.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi Ufundi Sanifu mwaka 2003/2004 walikuwa 30, Stashahada ya Juu ya Uhandisi mwaka 2003/2004 walikuwa 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya kuhusu upatikanaji wanafunzi katika vyuo vya Ufundi. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Msekela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya Ufundi hupata wanafunzi kutoka Shule za Sekondari za kawaida na za ufundi waliomaliza Kidato cha Nne na kufaulu vizuri masomo ya Sayansi za Msingi, Fizikia, Hisabati na Kemia na mengineyo. Kwa vile masomo hayo hayajafutwa katika shule za sekondari, *phasing out* ya masomo ya ufundi katika shule za sekondari hakutaathiri upatikanaji wa wanafunzi kwa ajili ya vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kuhusu kutumia miundombinu iliyoko katika eneo la mgodi wa Mwadui pamoja na majengo ya kiwanda cha nyama kama chuo cha madini na chuo cha mafunzo ya Stashahada ya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itazingatia ushauri huu wa Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte wakati wa kushughulikia uhuishaji wa matumizi ya miundombinu mbalimbali ya vyuo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki na Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoliarifu Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Waziri mwaka 2003 kuwa Wizara imeandaa mwongozo wa kuwahudumia wavumbuzi na wabunifu kwa lengo la kuendeleza vipaji vyao na ubunifu zaidi kila inapobidi. Aidha, utaratibu wa kuwapata wabunifu na wagunduzi kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini unaandaliwa. Utaratibu huo ni pamoja na kuangalia namna gani masuala ya Sayansi na Teknolojia yanaweza kuchambuliwa katika ngazi mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini kama ifuatavyo:-

Kuhusu usafiri wa anga, Wizara yangu itahitaji kulifanyia kazi suala hilo hasa ikizingatiwa kuwa masuala ya ungo ni masuala yanayohitaji utafiti wa kutosha ili ku-*establish* ukweli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ilitokana na kwenye gazeti iliandikwa kuna mganga ambaye alisema angependa kumthibitishia Mheshimiwa Waziri kwamba anaweza kusafirisha watu katika ungo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itashukuru kama Mheshimiwa Mbunge ataweza kutupatia wanaohusika ili tuweze kushirikiana nao kwa lengo la kufanya utafiti huo wa kusafirisha watu katika ungo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bujiku Sakila, alikuwa na hoja ya kuhusu madhara ya simu za mikononi. Suala la madhara ya simu ya mikononi limeelezwa mara kadhaa katika Bunge hili Tukufu pamoja na vyombo vya habari na mikutano mbalimbali. Hata hivyo, simu za mikononi zinazotumia mionzi zinatumia mionzi isiyo ayonisha. Viwango vikubwa vinaathiri chembechembe za mwili kwa kuzipandishia joto na kusababisha madhara. Hadi sasa tafiti mbalimbali pamoja na zile zilizofanywa na Shirika la Afya Duniani zimeonyesha kuwa viwango vya mionzi ya simu za mikononi na *antenna* zake katika minara siyo ya kuleta madhara. Kwa hiyo, tungeomba tu mtoe wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bujiku Sakila, anaweza kuendelea kutumia simu yake ya mkononi. Hata hivyo, nadharia inaonyesha kuwa viwango vya mionzi vikiwa vikubwa madhara yanaweza kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Remidius Kissassi, namshukuru sana Mheshimiwa Remidius Kissassi, kwa ushauri wake kuhusu kuboresha mazingira ya wataalam na hususan kuboresha mishahara yao. Aidha, namshukuru pia Mheshimiwa Remidius Kissassi, kuhusu ushauri wake kuendeleza raslimali za baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Musa Lupatu, pia namshukuru kwa ushauri wake vile vile wa kuhusu kuboresha mazingira ya wataalam kufanyiwa kazi na hasa mishahara yao kama alivyoshauri pia Mheshimiwa Remidius Kissassi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Margareth Mkanga, namshukuru kwa msisitizo wake wa kuongeza kiasi cha fedha kwenye mfuko wa kuendeleza sayansi na teknolojia. Aidha, alisisitiza pia umuhimu wa kuboresha mazingira ya kutendea kazi na mishahara ya wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw' pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati kwa mchango wao pamoja na Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hoja yetu kwa maoni yao. Napenda pia kumshukuru Mchangiaji Mkuu wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kwa mchango wake nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nimempongeza kwa mchango wake niliuona katika Kamati. Lakini baada ya kusoma ambayo ameandika, kweli ningependa kuungana

na wenzangu ambao tayari wameshampongeza kwa maandishi kwamba haijapata kutokea mchango huu ni nzuri sana. *(Makofi)*

Aidha, nachukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hotuba yangu kwa mdomo na kwa maandishi. Waliochangia kwa mdomo ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Benson Mpesya na Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wafuatao wamechangia kwa maandishi, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Herbert Mntangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa John Magufuli na Mheshimiwa John Mwakipesile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyoona wengi wamechangia katika hoja hii na ingekuwa imepatikana nafasi wengi zaidi wangeweza kuchangia. Hii ni kuonyesha umuhimu wa hoja hii ambayo tumeleta mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ambazo zimejitokeza ni nyingi na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wangu kwa kuzipitia katika mchango wake, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla hoja zinaweza kuainishwa katika makundi yanayofikia 30. Kwa hiyo, kwa muda ambao nimepewa haitawezekana kujibu hoja kwa hoja. Lakini kwa heshima kabisa nataka kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba ushauri huu kama kawaida yetu tutatekeleza kwa mujibu wa uwezo wetu katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yale ambayo yanahusu Serikali nzima, Serikali kwa kupitia Wizara hii imesikia na hasa ambalo linaonekana kwa wazi kabisa ni lile linalohusu ufinyu wa Bajeti. Hili Serikali imelisikia, Wizara yangu imesikia na tutafanya tuwezalo kujaribu kuweka shinikizo kama mnavyoweka ninyi wenyewe hapa kwa

kuzingatia uwezo wa Serikali na mapato yetu, ili stahili ya Elimu ya Juu iweze kuwekwa pahala pake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kubwa ambayo inajionyesha hapa ni utafiti. Kwa sera zetu, utafiti umetiliwa umuhimu. Kama alivyoonyesha Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara haizidi asilimia 0.6. Lakini sisi katika nchi ya Tanzania tulilenga katika asilimia 1. Utafiti bado tunafanya katika Wizara yangu wa kuangalia Serikali imetoa kiasi gani kwa utafiti kwa ujumla, nakubaliana kabisa kwamba ukiangalia kwa ufinyu kwamba utafiti unakwenda kwenye Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, utakuta kwamba ni bajeti ndogo sana. Lakini kwa taarifa nilizonazo na kwa utafiti nilioufanya ambao bado hatujaukamilisha inaonekana kwamba tungefikia katika Wizara mbalimbali asilimia 2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utafiti utakapokamilika kikamilifu niko tayari kuweka taarifa hiyo ya utafiti mbele ya Bunge lako Tukufu. Uwezo wa kufanya utafiti ninao kwa sababu Taasisi zangu ziko pale za utafiti, zinaweza kwa ukamilifu kabisa. Sasa hivi katika Wizara sita tulizofanya utafiti ni asilimia 2.6 ya Pato la Taifa limekwenda au gawio la fedha limekwenda katika utafiti. Kwa hiyo, hatujafanya vibaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya utafiti na matokeo ya utafiti. Haya nakubaliana kabisa na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge kwamba sisi kama chemchem na chanzo cha mawazo na chanzo cha teknolojia inahitajiwa kusambazwa teknolojia hiyo kwa wale walengwa na ningependa kuungana na Mheshimiwa Benson Mpesya katika mazungumzo yake ya hapa, alisema mwishoni hapa kwamba walengwa wakubwa ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Benson Mpesya yeye kasema kwamba bado Taasisi za Elimu ya Juu hazijajielekeza kwa wakulima. Mimi nisingependa kukubaliana naye, si kweli. Kwa sababu miundombinu yetu katika vyuo vyetu vya utafiti, vyuo vikuu, vituo vya utafiti katika kilimo, vituo vya utafiti katika upande wa mifugo inajielekeza kumsaidia mkulima. Mbegu bora za mtama, mbegu bora za mahindi kama katumani, kama vile mbegu bora zile za mifuko hapa, yote hayo yanawasaidia wakulima. Yote haya ni sayansi na teknolojia. Kwa hiyo, mkulima amesaidiwa sana na utafiti wetu na hayo ni matokeo ya Taasisi zetu za utafiti na elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachohitajiwa sasa ni mtandao mzuri wa kupokea yale ambayo yamefanyiwa utafiti na vyuo vyetu katika ushirikiano wa kuyasambaza kwa wakulima. Mnasema kwa Kiswahili sijui Huduma za Ugani hizi ziweze kuboreshwa hayo Serikali imeyasikia na itayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *DIT* kutunga mitihani na kutoa tuzo, kazi hiyo imeanza kufanyika. Napenda kuwapongeza Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Dar es Salaam pamoja na Baraza la Ufundi katika nchi kwamba tayari kazi hii imeanza kufanyika.

Kuhusu wanataaluma wetu kuhama na kwenda nchi nyingine, hili ni tatizo katika dunia nzima sasa, hasa dunia ya tatu ambapo bado hatujaweza kuwachukua hawa wataalam wetu na kuwatumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama nilivyosema katika hotuba yangu ya mwaka 2003/2004, watu wenye busara huvuna hata kwenye matatizo. *Wise people find opportunity even in the problem, not only so wise people find in an opportunity a problem. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la watu kwenda nje na kupata uzoefu katika nchi zilizoendelea au hizi ambazo zinafanya kama sisi, linaweza likabadilishwa na likaleta manufaa kwa uzoefu huu ukaletwa katika nchi hii ama kwa mapato ya fedha kule wanaleta *remissions* za fedha katika nchi hii au wanaporudi hapa wanakuja na shehena ya uzoefu na maarifa mapya. Kwa hili linaweza kubadilishwa kama *export of technology. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kuhusu *Institute of Marine Science* ya Chuo Kikuu Dar es Salaam. Hili sioni kama ni tatizo. Kila mtoto anapozaliwa anaanza kwanza kutambaa halafu baadaye anatembea. Hufikirii kwamba mtoto utakampomzaa atabaki mkononi pale unamshikilia, hatembei, hata Chuo hiki kitatembea. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tulianza na wanafunzi 14, leo ni 10,000 wapo na kitatembea hata hivyo, hamna tabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu unakuja matumizi ya wataalam, matumizi ya wataalam kwa kweli ni tatizo la Kitaifa na ni tatizo la kiuchumi. Tatizo ni uchumi kuweza kubeba utaalam wa watu wetu, tutawatumia vizuri na mpaka sasa wataalam wetu wanatumika vizuri. Wengi wapo hapa kwenye Bunge wanatumika vizuri. Nadhani wote mnathibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanafundisha, wengi wanafanya kazi nzuri kabisa, ni wachache kabisa ambao kweli ni wataalam wanaweza kudai kwamba hawatumiki vizuri. Ningependa kupata ushuhuda huo. Kwa kweli kama hawatumiki sawasawa ni wachache sana. Kwa hiyo, hili tunahakikisha tumesikia na kwamba pale ambapo kuna ubovu au ulegevu hapa na pale utasahihishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Mbeya Technical College* kutoka hali yake ya Chuo cha Ufundi cha kawaida kuingia *The Institute of Science and Technology* ambayo kwa kifupi ni ni *MIST* na baadaye kuingia katika hatua ya *MUST* yaani *The Mbeya University of Science and Technology* ni dhana na azma ya hakika, nani ambaye anasita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa na mimi mwenyewe na Mheshimiwa Naibu Waziri na watu wote ambao tunatoka sehemu hizo pamoja na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, hatusiti hata kidogo azma ya Serikali kukigeuza chuo hiki kuwa chuo cha ufundi. Tumeelekeza nguvu zote, unatafuta ujasiri gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri wote hapa ni wajasiri. Hakuna Waziri peke yake ni jasiri. Sasa fedha zimeelekezwa kwenye elimu ya msingi na elimu ya sekondari. Ujasiri tuliofanya hapa ni kuleta Sheria ya kuanzisha mfuko wa elimu ndiyo ujasiri uliofanyika. Je, tutafute njia nyingine? *(Makofi)*

Mehsimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ningependa msibague kwamba kuna Waziri mmoja jasiri na mwingine si jasiri, wote hapa ni majasiri na Wabunge wote ni jasiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema na narudia na Wabunge ni jasiri, kama msingekuwa jasiri msingeingia kwenye Bunge hili. Kwa hiyo, *Mbeya Technical College* inaelekea kwa uwazi kabisa katika hali ngumu hii kuelekea kuwa *MIST,* angalia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tulianza na wanafunzi 14 na walimu 20, leo angalia tulipofikia. Hatukuwa tunataka fedha na bahati tukajiegemeza kwenye Chuo Kikuu cha London, lakini *Mbeya Technical College* haitajiegemeza kwa Chuo kingine chochote, yenyewe itafikia Chuo Kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swala la mitaala bora na ajira za wahitimu wetu lilijitokeza swali hili Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, amelizungumzia nashukuru sana, nchi imesikia na wananchi wote wamekwishaelewa kwamba tuna duku duku hili na wataalam wetu Wakuu wa Vyuo na Makamu Wakuu wa Vyuo wameshasikia hilo na sisi sote tuna azma ya kuboresha mitaala yetu wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *Internal Audit, Academic Audit* na vile vile tuna chombo chetu kinaitwa *The Higher Education Accreditation Council* na vile vile tutakuwa na utaratibu wa *National Awards System* ambayo itaangalia *quality assurance and audit control* katika Vyuo vyetu ambayo itahakikisha kwamba wanataaluma wetu na wahitimu wetu wanapata mafunzo ambayo yanatufaa na kwa ajira zetu yanafaa. Kwa hiyo, suala la wageni kuajiriwa badala ya watu wetu litakwisha hivi karibuni ambayo tumeboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vigezo vya sifa za Walimu wa Vyuo Vikuu, nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kujielekeza pale ambapo wametusaidia. Mlitaja nchi mbalimbali pamoja na Japan. Japan nimekaa kule jamani, nimekaa miaka mitatu kama Balozi. Nilipokuwa kule walikuwa katika hali tofauti. Mwaka 2004 wamepitisha *White Paper* nyingine. Kule Japan wanazidi kuboresha na sisi hatubaki pale pale, wakati wote tunaboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa *The Third Part Assessment* ya Vyuo Vikuu. Wao wenyewe wana *internal assessment* zao. Kuna *Third Part Assessment* ambazo ni pamoja na Wabunge mnapozungumza hapa ndio mnafanya *quality assessment* ya Vyuo Vikuu vyetu navyo vinasikia na kwa adabu vinafanya mabadiliko ambayo yanafaa na ambayo tunawezeshwa kuyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya wanafunzi walemavu, tunakushukuru sana Mheshimiwa Margareth Mkanga kwa mara nyingi kutukumbusha hayo, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri, ameshajibu suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mmeuliza juu ya mkakati ambao nchi yetu inao ya kuweza kupokea mkakati mbinu ambao tayari umeanzishwa kwenye Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari yaani MMEM na MMES. Hili wimbi likifika huko juu, je, tuko tayari kulipokea? Nasema *affirmatively* kwamba ndio tuko tayari kulipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kutumia wataalam wake wenyewe sio kutoka nchi za nje wenyewe tumeweza kutengeneza mpango kamambe wa miaka 15 kuanzia mwaka 2003 haadi 2018 ambao una vipindi vya miaka mitano, mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwaka 2003/2004 utagharimu karibu dola milioni 410 za Kimarekani kwa utekelezaji wake na ni kuongeza miundombinu, kuboresha hali ya ufundishaji, kupokea wanafunzi wengi katika vyuo vyetu na kuanzisha vyuo vingi ili kupokea wanafunzi ambao watamaliza *Form Six* ambao tunakadiria watakuwa kati ya 125,000 mpaka kufikia 250,000 kwa mwaka. Hawa wote tutakuwa tayari kuwapokea kuanzia mwaka 2009 na mpaka itakapofika mwaka 2014 tutakuwa tayari kupokea zaidi ya 50,000 katika Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Sokoine na Vyuo Vikuu vya Kitaifa, halikadhalika vyuo vikuu binafsi vinaongezeka ambavyo navyo vitachangia mchango mkubwa katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hoja ni nyingi sana kujaribu kuzijibu zote hapa kwa kweli itatuchukua muda mrefu na vile vile nitawachosha Waheshimiwa Wabunge. Kazi yenu na nia yenu ilikuwa ni kulieleza Taifa hili, kueleza Wizara yangu na Serikali ielewe shida za Elimu ya Juu. Tumesikia na mmesema mara nyingi maneno hayo na mkaona pale ambapo uwezo tunao tunatekeleza, mniamini kwamba tutatekeleza haya ambayo mmetupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kitu kimoja, Vyuo Vikuu vya Binafsi hata vile vya Serikali popote vinapoanzishwa ni Vyuo vya nchi nzima sio vya sehemu. Kwa hiyo, kwa kuzingatia usawa katika nchi hii pamoja na kwamba Vyuo vinakuwa katika sehemu mbalimbali Serikali itajitahidi kwenye Vyuo vyake vya Umma kuvisambaza sehemu mbalimbali katika nchi hii. Mfano mzuri ni Chuo Kikuu Huria ambacho sasa kimesambaa katika Mikoa karibu yote. Hicho ni Chuo Kikuu sio kitu kingine, msidhani ni kituo tu, ni kituo cha Chuo Kikuu. Kwa hiyo, katika nchi yetu hii kila Mkoa una Chuo Kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Benson Mpesya, amenisikia na yeye ni yule ambaye amefaidika na Chuo Kikuu Huria kutoka Mbeya na akasoma mpaka kapata Shahada yake. Kwa hiyo, Chuo Kikuu kinakuwa popote pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa Mikoa yote na ni pamoja na Mikoa hii ambayo iko Kusini mwa Reli ya *TAZARA* tushirikiane pamoja. Juzi nilikuwa Mtwara nikaomba majengo ambayo yanakaa bure ya *CATA (Cashewnut),* majengo makubwa,

watupatie Vyuo Vikuu vyetu. Nimekuta *Open University* inakaa kwenye nyumba ya ovyo kwa sababu hawawezi kupata nyumba nzuri na huku majengo yanakaa bure. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Benson Mpesya kuwa tushirikiane pamoja katika kuleta hadhi kwenye Elimu ya Juu na ifanane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vikuu Binafsi katika kuwaruhusu na kuwapatia Ithibati vile vile tutaangalia mtandao unatandaa namna gani lakini uwezo wetu wa kuwalazimisha waende mahali pengine ni mdogo sana, ni fedha zao ambazo wanatumia. Tunaweza kuwalazimisha wachukue wanafunzi sio wa dini zao wala sio wa itikadi yao, wachukue wanafunzi wote katika nchi hii ambao wana sifa zinazohitajika. Kwa hali hiyo tutakuwa hatuna shida kubwa sana. Tumepokea maombi mengi na maombi hayo yanakwenda kwenye sehemu inayohusika ambayo ni Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na dukuduku, karibu nitamalizia kwa sababu mengine mmesema yote yamekubalika lakini kuna mawili ya kueleza. *(Kicheko)*

La kwanza ni kuhusu Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi, hili siwezi kulisemea sana kwa sababu tumeliongelea sana hapa. Nataka nisahihishe mambo fulani ambayo yamepotoshwa. Kwanza, Serikali haikufunga Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vyuo Vikuu vina uwezo wa kufunga au kufungwa kufuatana na sheria zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka ieleweke kwamba katika nchi hii Vyuo Vikuu vina *autonomy* ya kujiendesha vyenyewe, kwa kuchagua masomo yao *academic autonomy* na vile vile *administrative autonomy* katika sehemu kwa mujibu wa sheria iliyowaweka. Sasa wakiona kama ni hatari kuwa na watu ambao wamegoma kwenye *campus* zao wana uhuru wa kuwaondoa watu hao. Kama wewe ukiona nyumbani kwako kuna fujo unaweza kumwondoa mtu yeyote anayeleta vurugu asivunje mali yako. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huhitaji Serikali ije kufunga nyumba yako ili uwaondoe watu wanaoleta vurugu huko kwako. Chuo Kikuu hakikuhitaji Serikali, kilihitaji tu nguvu za dola kuwasaidia kuwaondoa wale kwa sababu ilidhani wangekaa pale wangevuruga na kuleta fujo zaidi. Leo Waheshimiwa Wabunge mngelaani kwamba Wizara hii ingeshtakiwa kwa *gross negligence* ambayo imeleta hasara kisheria kwamba sisi tumepewa mamlaka ya kusimamia pale hawa wamengojea mpaka wamevunja hali ya chuo mlikuwa wapi, mngekuwa mnazungumza hayo, Waziri mbona hukuchukua hatua? Hapa sikuchukua hatua kwa sababu nilijua Chuo kitachukua hatua kujilinda chenyewe na ndivyo kilivyofanya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, sio kweli kabisa kwamba wadau hawakushirikishwa labda tumefanya makosa hapa na pale na tumefanya utafiti kuhusu kwa nini migomo inatokea kwenye vyuo. Si muafaka na wala hatuna muda kueleza tunaposimama hapa kuhusu taarifa hiyo. Tutaileta Bungeni hapa mkihitaji msome wenyewe Waheshimiwa Wabunge mtaona nini hasa chimbuko la matatizo haya.

Mojawapo ya sababu naweza kusema ni ufinyu wa bajeti ambapo unaona wanafunzi wanabanana kwenye Maktaba ya kusomea, wanabanana kwenye *lecture theaters* halafu wanapata shinikizo la mitihani na utaona kwamba wakati wa migomo ni karibu na mitihani inatokea tu hivi? Ni lazima kuwe na *a kind of correlation* (uhusiano). Lakini bado hatujathibitisha *correlation* ni kiasi gani lakini utafiti umeonyesha wazi kwamba kuna chungu nzima ya matatizo ambayo yanaleteleza hawa wanafunzi wakagoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo mengine tutayazingatia tuyaondoe. Mojawapo ni uongozi hafifu kwa wanafunzi ambao hauna mawasiliano ya karibu na wanafunzi wenzao. Hapa lazima elimu ya uongozi wa wanafunzi tuizingatie katika Vyuo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu sisi katika Serikali tuna udhaifu wa kutoenda kuzungumza na wanafunzi. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kukuomba wewe binafsi ukipata nafasi tukukaribishe kwenda Vyuo Vikuu ukazungumze na wanafunzi wetu na ninyi Wabunge twende kule tukazungumze na wanafunzi wetu. Faida moja ni kwamba wanafunzi wanaweza kupata sasa *role model.* Sasa kama hatuendi pale wataipata wapi? Ni sisi twende tukazungumze. *(Makofi)*

Mimi nilipokuwa mwanafunzi niliwaona Wakoloni na Machifu wakija kwenye shule zetu za Sekondari. Namkumbuka Chifu Maruma, Chifu Kidaha Makwaia na Chifu Majebee, walikuja katika shule zetu kutuhamasisha. Sasa haya ndio tutapanga na tutawapangia ndugu zangu ili tuweze kuwasaidia wanafunzi wetu. Mimi na ninyi ni kama wazazi wa watoto wa *University,* sio watesaji wa vijana wetu. Tunataka watoto wetu wa *University* wapate elimu nzuri na wakae kwa hali nzuri kwa mujibu wa uwezo wetu. Hakuna mtu anataka watoto wake wateseke hata kidogo, wote tunataka watoto wetu wasome vizuri na waweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alikuwa ameulizia kuhusu Chuo Kikuu cha Zanzibar *(State University of Zanzibar).* Hili hatuwezi kuliacha likazagaa zagaa tu hivi hivi. Nataka kusema kwamba Chuo Kikuu cha Serikali cha Zanzibar ambacho kimeanzishwa, kimeanza kwa uhalali kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya utandawazi na *liberalization of education* kama Halmashauri zinaweza kuamua zikaanzisha Chuo Kikuu, kama Mkoa unaweza kuamua kuanzisha Chuo Kikuu, kama Walutheri wanaweza kuamua kuanzisha Chuo Kikuu kwa nini Serikali ya Tanzania Zanzibar isianzishe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapi katika Katiba ambapo imeandikwa kwamba hawawezi kuanzisha hiki kitu? Wanasema Elimu ya Juu ni mambo ya Kimuungano, ndio na bado inaendelea kuwa mambo ya Muungano kwa sababu hakiwezi kuwa Chuo Kikuu mpaka Ithibati *(The Higher Education Accreditation Council)* iwapitishe. Kwa hiyo, bado suala la Muungano liko pale pale, huwezi kuwa Chuo Kikuu mpaka tukupitishe na sheria iliyopitishwa na Bunge lako la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kwa heshima na taadhima nisiwachoshe, naomba tu mnipatie fedha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba fedha ambazo tumeziomba najua kabisa ni shilingi bilioni 89 hazitoshi kabisa kuendesha, lakini walau nipatieni mbegu hizi nikapande zitaota na nina matumaini kwamba zitazaa mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 68 - Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... 1,182,927,700/=

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 1001, *Programme10,* napenda kupata ufafanuzi wa Waziri. Katika mchango wa maandishi niliomplekea asubuhi nilieleza kwamba kuna tatizo ambalo Watanzania wengi ambao wanapenda kuchangia Mfuko wa Elimu wanalipata. Nilitegemea kauli ya Waziri kuhusu namna ya kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa tuliyonayo, utaona kwamba mchango wa Serikali unapungua mwaka 2001/2002 ulikuwa 5% leo umefika 3%. Kwa hiyo, mchango wetu kama Serikali kwenye Mfuko wa Elimu unazidi kupungua na tatizo linazidi kuwa kubwa na ndio maana tunashindwa kupata fedha.

Sasa Watanzania wengi, wafanyabiashara na wananchi wa kawaida wangependa kuchangia Mfuko huu kama watapata msamaha wa kodi kwa kile kiwango ambacho watakichangia kwenye Mifuko ya aina hii. Nataka kupata ufafanuzi wa Waziri anafikiria lini kuleta Bungeni sheria ambayo itaruhusu wananchi wanaochangia wapate msamaha kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na muuliza swali kwamba sheria inaruhusu wanaochangia elimu, afya na maeneo ya maendeleo ya jamii kwa namna yoyote wapate misamaha ya Kodi ya Mapato endapo watakuwa wamefanya hivyo kwa utaratibu fulani uliowekwa ndani ya sheria hiyo.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na vile vile Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nadhani majibu ya Waziri ni sahihi na nakumbuka katika *budget speech* yake kama sio mwaka 2002/2003 aliwahi kulisema lakini katika utekelezaji limekuwa gumu. Je, Waziri sasa yuko tayari kuitoa kwa

maandishi na kueleza utaratibu unaohitajika kufuatwa ili wananchi waweze kuchangia Mifuko hii iwe kwa Mfuko huo mkubwa au kwa Mifuko katika Halmashauri za Wilaya mbalimbali? Kinachotakiwa ni mwongozo ulio wazi, ni taratibu zinazoeleweka na watu wajue wanapeleka kwa nani. Sheria inawezekana ipo lakini haijulikani hiyo sheria iko wapi na watu wanaotaka kuchangia hawaijui. Je, Waziri yuko tayari kutoa hayo maelekezo ili fedha hizi ambazo vinginevyo zinapotea ziweze kupatikana kwa manufaa ya nchi yetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba radhi kama watu wengi hawafahamu sheria hiyo. Nitatoa taarifa kuonyesha ni sheria ipi na vifungu vipi vinavyotakiwa na utaratibu unaotumika sio tu kwa faida ya Mfuko huu, lakini kwa faida ya watu wengi wanaochangia elimu za aina nyingine. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati ya Huduma za Jamii tulitaka kujua kuhusu Mfuko wa Elimu kwamba Serikali inaweka sheria au utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba mchango wake haupungui kutoka mwaka hadi mwaka badala ya kuongezeka kutoka mwaka hadi mwaka? Sasa hatukupata majibu ni asilimia kiasi gani ama ya Bajeti ama ya Pato la Taifa Serikali inachangia? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wakati nikichangia nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu ule mpango kamambe ambao yeye anasema utatumia dola milioni 410 na akasema ni kwa miaka 15 kuanzia 2003 hadi 2018. Hizi dola milioni 410 nadhani ni kidogo kwa wale wanaosikiliza kwa kadri ya hali hii inavyotaka, sijui anaendelea na mpango wake ule ambao aliutayarisha bila ya kuangalia kama tulivyomwambia asubuhi ni kitu gani kimefanyika katika MMEM na MMES na matokeo yake Mheshimiwa Waziri hilo analiangalia halafu anali-*incorporate* au ameliacha?

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati nikijibu hoja hapa ni kwamba nisingeweza kujibu hoja zote lakini majibu ya hoja zote ninayo hapa kwa maandishi. Kama nilivyosema tumezingatia mchango wa Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, ulikuwa mchango mzuri, tumezingatia kabisa aliyosema.

Kwanza nimeshapata jibu kutoka kwa Spika, nadhani aliuliza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kuhusu Sheria ilikuwa namna gani? Mwanzoni ule Muswada haukuonyesha asilimia ni ngapi baadaye marekebisho yakatokea hapa kufuatana na kumbukumbu za Meza ni kwamba isiwe *not exceeding 2%.* Tumeona kuna ubovu katika hili, tutaleta marekebisho mengine kwamba isipungue 2%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ambao nimeutaja sasa hivi ni *dynamic* yaani unajisahihisha wenyewe jinsi unavyokwenda sio *static.* Tulipouanzisha ulizingatia mpango wa MMES maana yake hii ni miundombinu ambayo itaongezwa kwa ajili ya kupokea hawa wanafunzi. Kama tutaona kwamba takwimu hizi hazikidhi basi tutaenda na takwimu hizo ili kuweza ku-*update* na kufikia yale ambayo yanahitajiwa.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Labda nirudie lile lingine ambalo tuliomba kwamba kuna Sera ya Sayansi na Teknolojia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1996 na tukaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuleta sheria hapa ili sera ile sasa iweze kutekelezwa kisheria. Je, katika hilo Mheshimiwa Waziri analiambia nini Bunge na mimi mwenyewe?

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera huwa na mambo mengi na haiwezi kuwa na sheria moja, *legislation* itakuwa katika *pieces of legislation* mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji. Kwa hiyo, wakati muafaka utakapofika tutaleta Bungeni Miswada ya kutekeleza sera hiyo. Mfano ni hii Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia hiyo imetokana na sera na kutakuwa na Mfuko wa Utafiti inatokana na sera. Kama inahitajika sheria basi tutaileta hapa Bungeni lakini kutakuwa na sheria nyingi za utekelezaji haiwezi kuwa na sheria ya sera yaani sera yote inawekewa sheria moja kutakuwa na sheria nyingi za utekelezaji wa sera.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Nimefarijika kidogo kwa maelezo aliyokuwa anatoa Mheshimiwa Waziri, lakini sikuipata vizuri. Nina maswali matatu nahitaji maelezo kidogo.

Kwanza, ni hii inahusu Sheria ya Mamlaka ya Elimu. Wakati tunaipitisha sheria hiyo hapa, nilitoa mapendekezo kwamba ingefaa na Watanzania wengi wangefurahi sana kama tungechangia Mfuko wa Elimu hata kupitia kwenye vinywaji vya soda, bia na vinywaji tofauti. Wakati ule nilihakikishiwa kwamba hiyo haina haja kwa sababu Mfuko huu utapata ruzuku ya Serikali isiyopungua 2% ya Bajeti ya Serikali ukiondoa deni la Taifa.

Ningependa nipate maelezo kwa nini sheria yenyewe sasa imebadilika bila kubadilishwa na Bunge ikasema *not more than 2%* wakati sisi tulipitisha *not less than 2%* na *amendments* zilizokuwa hapa zilifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda nikipongeze sana Chuo Kikuu Huria kinaendesha masomo vizuri na kuyasimamia vizuri na watu wengi hata Wabunge hapa wamehitimu kupitia katika Chuo hicho. Lakini dunia hii ya utandawazi pia ina vyuo vingi na katika maeneo mengine hasa Marekani unaweza kwenda mwezi mmoja ukalete cheti na *Degree. (Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nieleweke vizuri hapa kwamba kuna Shahada nyingine za namna hiyo unaweza kupata kwa mfano unaweza kupata *Doctor Honoris Causa* ambayo ni Shahada ya Udaktari unayopewa kwa sababu ya heshima yako na heshima ya kazi ya utafiti uliyofanya au huduma ulizotoa zikasaidia jamii. Sasa nje ya *Doctor Honoris Causa* hakuna Shahada nyingine za barua, Shahada unaifanyia kazi halafu unapata, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye magazeti wameandika kuna mtu anatafuta *Degree* kwa sababu anataka kuwa Rais. Kuna bwana mmoja anasema amejiandikisha

huko Marekani *Pacific something.* Sasa hizi tutazi-*audit* namna gani, *how do we control these kind of influx* ya watu ambao wanatafuta *Degree* za barua wanaleta wanasema sisi tuna *Degree* tunataka kuwa Rais?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Wizara hii itueleze kwa wakati huu ina njia gani za kuweza kudhibiti *influx* hiyo au itaweka utaratibu gani maana *Higher Degree Accreditation Council Board is doing fantastic job for internal University* lakini kwa nje hatujui tutafanya nini, hicho cha pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, katika nyakati mbalimbali tumeelezwa na Serikali kwamba kuna uhaba wa Madaktari na kupitia Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu sasa Serikali itaweza kuwadhamini vijana ambao wanasomeshwa na wazazi wao au jamaa zao, Serikali itachukua mzigo huo ili kuweza kupunguza uhaba wa Madaktari hapa nchini. Sasa wazazi wengi hawajui utaratibu gani unafuatwa ili waweze kupata *sponsorship* hiyo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Kama nilivyoeleza na alivyoeleza Mheshimiwa Spika, asubuhi ni nini hasa kilipitishwa na Bunge hili nadhani mjadala umefungwa Katibu wa Bunge aliposema kwamba tulipitisha *not exceeding 2%* kumbukumbu ameenda kuzitafuta kwenye *Hansard* akaona tumepitisha hivyo. Sasa utaratibu wetu ni kwamba Kiti kikishaamua basi kiliamua kuwa tulipitisha hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nashukuru umekipongeza Chuo Kikuu Huria *(Open University). Open learning and distance learning* zitakuwa nyingi tu. Kuna mjadala mkubwa katika ulimwengu na tumehudhuria makongamano na *conference* nyingi kuhusu *value of opening learning* na *ICT* na ubora wake na matatizo yake. Hata *University of Dar es Salaam* tumeanzisha ile *Video Conference* hamuonani lakini mnaweza kukaa kwenye *conference.* Haya ndio mambo ya teknolojia ya kisasa yana uzuri wake na ugumu wake.

Sasa *Degree* hizi ambazo zinapatikana kwenye *internet* kutoka Vyuo Vikuu vingine, ukija na cheti chako sisi sasa tuna chombo chetu ambacho kinaitwa *Higher Education Accreditation Council* ambapo *Degree* yako ukija nayo unaipeleka pale tunaitathmini kufuatana na vigezo vyetu vya hapa nchini.

Kama usipoipeleka kule utakaa na cheti chako, umekitathmini wewe mwenyewe basi una *Degree* yako na siyo hivyo tu tunatathmini na chuo chenyewe ulichotoka na kwenye taarifa yangu tumeonyesha, tumetathmini vyuo vingapi na vyeti vingapi, tunafanya hivyo. *(Makofi)*

Sasa *Degree* za *Honoris Causa* ni juu Chuo Kikuu chenyewe, ndiyo maana ya *autonomy* ya Chuo Kikuu, lina sifa kwamba linajitegemea. Kama linataka kuongeza sifa yake linataka leo Ng'wandu limpatie *Honoris Causa* na Ng'wandu hana sifa hizo ni juu ya Chuo chenyewe kujiteremsha kiasi hicho au wakiona kwamba Ng'wandu ana sifa kubwa sana tukimpatia *Honoris Causa* kwetu na Chuo chetu kitapata faida.

Ndio maana yake yaani mtu mzito huyu akipata *Degree* kutoka kwetu na sisi Chuo tunapata faida. Maana yake Vyuo Vikuu Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, anafahamu kwamba vinajivunia kwa vitu viwili, *quality* ya wanafunzi wake na walimu wake kwamba sisi walimu wanafundisha *quality* ya kazi yake na wanafunzi waliopita hapa wana hadhi kiasi gani ndiyo wanawapatia hiyo *Degree* ya *Honoris Causa.*

Sasa hili nadhani nimejibu namna ya kuwa-*control,* lakini ili *control* izingatie utandawazi, sisi katika ulimwengu na katika Afrika tumekubaliana katika Azimio la Arusha, siyo lile la CCM, la Kiafrika *on accreditation of credentials, academic credentials* ambalo tumekubaliana na tutahitaji watu wa-*accede to that agreement* kwenye mkataba huo wa kuweza kuvitambua vyeti hivi na sifa hizi za ki-*academia* kwa hiyo, tupo mbioni Afrika. Katika dunia nzima pia *UNESCO* inafanya kazi kubwa ili kuweza kuzingatia na kulinganisha vigezo vya kuweza kutambua na kulinganisha vigezo vya kuweza kutambua na kudhibiti hati na vyeti.

La tatu, linahusu wanafunzi madaktari katika vyuo binafsi, kuna Kamati ambayo iliundwa ya wataalam ya Makatibu Wakuu ambayo iliweka vigezo vya nani ambaye atalipiwa. Tumesema kwamba katika Vyuo Vikuu binafsi, vijana wenye sifa kama zile za kuingia *MUCHS,* sifa zile siyo za kichinichini, hizo hizo ndiyo maana ya *accreditation,* kama Muhimbili na Ithibati maana yake mnalinganishwa wanafunzi, je, mna sifa zile zile ndiyo unapata sasa ule udhamini. Ndiyo natangaza hivi wazazi wasikie hiyo.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, nipo kwenye kifungu kile kile cha 1001. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilimwandikia Waziri kwamba kuna wanafunzi wanaotoka jamii ya wafugaji kwa mfano Wamasai na Wabarbaigi ambao wazazi wao hawataki wasome. Wengi waliofika *Form Six* ni kwamba wamesomeshwa na *NGOs* au Mashirika ya Dini, kwa mfano, mliowaona juzi waliokuja Dar es Salaam kutoka *Maasai Girls,* wengi wao mpaka wafike pale, wazazi wao hawakutaka wasome na mpaka sasa hawahitaji kuwasaidia kuwatafutia vyuo. Kwa hiyo, hawawezi kuendelea na Vyuo Vikuu.

Hayo nilimwandikia Mheshimiwa Waziri kwamba mtawafanyaje hawa wanafunzi ili wasaidiwe wasome bure kama walivyosoma kuanzia *Form One* mpaka *Form Six* ambapo mpaka sasa wazazi wao hawataki wasome? Ndio nikamwandikia kwamba hawa wanafunzi wasomeshwe bure mpaka wamalize.

Nasikitika kusema kwamba kuna ambao wamekwishamaliza *Form Six* na wamekwishaozwa. Hadi sasa *Maasai Girls* wamekwishamaliza mtihani wa *Form Six* nadhani mwaka wa tatu na kama kuna waliokwenda Chuo Kikuu nadhani ni wawili tu, wengine wote hawakwenda vyuo, wamerudi nyumbani na wameozwa. Ndio nikasema isingekuwa vizuri Serikali iwasaidie kuwasomesha bure kuliko kuzungumzia kila wakati suala la ukeketaji.

Sasa ili wabadilike jamii isaidiwe kwa kusomeshwa bure hawa wanafunzi. Niliandika hilo lakini Waziri hakulijibu. Sasa naomba maelezo.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba sikumjibu, nimejibu, muda haukuwepo wa kusoma kila jibu. Kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba nimejibu kila hoja kwa maandishi, haiwezekani kujibu kila hoja na hii ni hoja muhimu, ni vizuri amenikumbusha na jibu lake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mageuzi katika jamii hayawezi kutokana na sehemu moja tu, haitasaidia kuwasomesha bure tu hawa. Tutazingatia vigezo vingi katika kugeuza jumuiya, kupenda kwenda shule na kujua manufaa ya shule. Ni mabadiliko yote ya ujumla katika jumuiya hiyo yanahitajika kama ya kiuchumi. Nafurahi sasa uchumi unaanza kubadilika katika *Masai land,* jamii hiyo imebadilika na watu wengi wanapenda kwenda kusoma. Mfano ni yeye Mheshimiwa Lekule Laizer, kama mzazi ana watoto pale na anataka wasome. Hili jambo ni zuri sana. Wapo Wamasai wengi tu ambao wanataka kusomesha, si watoto wa kiume tu na watoto wa kike vile vile. Katibu Mkuu wangu ni Mmasai na amesoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa hili ili kuwasaidia, pamoja na mipango mingine ambayo lazima iende sambamba, wale ambao wameshinda vizuri wana sifa za kwenda Chuo Kikuu, maana hatuwezi kukubali chini ya sifa zinazohusika na ninyi Waheshimiwa Wabunge hamwezi kukubali, lazima wawe na sifa. Kwa hiyo, tunaanza kwanza kwenye sekondari kuhakikisha kwamba vijana wa Kimasai wa kike na wa kiume wanapata sifa za kuingia Chuo Kikuu, sifa za juu kabisa. Katika utaratibu wetu tunatoa kama asilimia kumi scholarship, tumeeleza hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa ya pili, kama wewe una sifa ya kawaida unaweza kukopa kwenye Bodi ya Mkopo. Watu hawa ambao hawana uwezo wazazi wao ndio watu wa kwanza kufikiriwa kukopa. Kwa hiyo, hawa ndugu zetu wafugaji wanaweza kufaidika na programu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza ya *scholarship* kwa asilimia kumi kwa watu ambao wameshinda vizuri sana na wale ambao waliobakia ambao wana sifa za kuingia Chuo Kikuu watakopa kwa mpango huu ambao tumeupitisha ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo, watu wote watasoma hakuna atakayebakia kwa sababu yoyote ile.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Waziri anasema ameandaa majibu, kwa hiyo, pengine ni kuyafikisha tu.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Nilitaka tu nipate ufafanuzi, tunafahamu kabisa kwamba mkopo umewekwa lakini kwa mtu ambaye mzazi wake hataki asome hatataka kukopa kwa sababu hataki huyo mtoto aendelee. Sasa ndiyo nilitaka Serikali ilegeze masharti kwa hawa wanafunzi, watoe upendeleo kwa hawa wanafunzi ambao wazazi wao bado hawataki wasome.

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkopo wala hakuna haja ya kulegeza masharti. Sharti mojawapo ni kwamba unakopa kwa dhamana yako mwenyewe. Kwa hiyo, hakuna haja ya kumwuliza baba au mama, wewe mwenyewe tu unataka kwenda kusoma, unakwenda tu unasoma na hakuna shida yoyote. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe yale niliyokuwa nakusudia ameyasema. Hata hivyo bado lile la *percentage,* ndilo ambalo bado kwangu ni tatizo, *not less than two percent and not more than two percent.* Ikikaa vizuri lile ndilo ambalo kusema kweli nilikuwa na matatizo nalo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... ... 108,049,900/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... ...512,578,800/=
Kifungu 2001 - *UNESCO Commission* ... ... ... ... ... ... ... ... ...280,186,900/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Higher Education* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 60,292,837,500/=

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona na nina maswali mawili katika kifungu hiki na ningependa Waziri anisaidie kupata ufafanuzi. La kwanza ni hili alilolieleza kuhusu vyeti bandia. Waziri ameeleza kwamba huwa wanahakiki na wana utaratibu wa kuhakiki lakini taarifa tuliyonayo na ambayo nilikwishampatia Mwenyekiti wa *Mzumbe University* nafikiri na wa *Sokoine University,* kwenye mtandao inaonekana kuna Maprofesa watano wenye *Ph.D* waliopata kutoka *Western Pacific University online.*

Sasa tatizo la msingi ni kwamba *Western Pacific University online* siyo *accredited* kwa *University* yoyote na kwa hiyo, hadhi yake haipo na haitambuliwi katika *University* yoyote ambayo inatambulika. Je, Waziri atakuwa tayari kufuatilia na kuona kwamba Wahadhiri wetu katika *University* zetu wanakuwa na sifa zinazotakiwa na kwamba zile sifa ambazo zimepatikana kwa njia hizo zina hatari ya kuangusha elimu katika vyuo vyetu vile vile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika kifungu hicho 3001, vile vile ni kuhusu ufafanuzi ambao Mheshimiwa Waziri ameutoa. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Waziri amejibu swali ambalo halikuulizwa. Mimi sikuuliza kwamba je, madhehebu ya dini yanaweza kuanzisha *University* au nani mwingine.

Mimi niliuliza swali *specific* ambalo Waziri analijua, lipo kwa maandishi na limetoka kwa barua kutoka kwa Katibu wa Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu, Waziri

analo na ufafanuzi ulitakiwa kwa sababu tatizo hilo lilikuwa na sura ya mgogoro wa Kikatiba. Suala si Zanzibar kuanzisha Chuo Kikuu, suala ni utaratibu wa kuanzisha, je, kama ulivyo katika Katiba na katika sheria zilizoko za kuendesha elimu ya juu utaratibu umefuatwa na Katibu wa Baraza la Ithibati ndiye anayeomba msaada. Sasa tunataka kujua kama utaratibu ule umekwisharekebishwa au hapana na hilo bado ni tatizo kwa sababu hata Naibu Waziri wakati wa kujibu kuhusu fedha *University* ya Zanzibar anaeleza kwamba wanaweza kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu ya juu ni la Muungano, *State University* ya Zanzibar ni sawa na *University* ya Dar es Salaam au *Sokoine University* na sisi wa Bara pia tuna haki ya kuingia kule kama imefuata utaratibu kwa sababu ni suala la Muungano. Lakini kwa sababu utaratibu haukufuatwa, kuna utaratibu tofauti tu ambao uko kwenye giza.

Mheshimiwa Waziri anakumbuka, nadhani ilikuwa kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, tulisema tusiamshe mgogoro wa Kikatiba, tuumalize chini kwa chini. Sasa mwaka wa tatu, hakuna hatua inayochukuliwa na Waziri anajibu kidogo kwa njia ambayo si wazi.

Mimi nataka kujua, je, utaratibu ambao ulilalamikiwa na Katibu wa Baraza kwa barua kwa chombo cha Bunge utaratibu ule umefikia wapi na je, kama imerekebishwa *State University* ipo kwenye utaratibu ambao mtu yeyote kutoka mahali popote Tanzania anaweza akaingia kwa masharti yale yale ya kawaida kama ilivyo kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *Sokoine University* na Vyuo vingine vya Taifa hili? Nashukuru. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina habari kwamba *HEAC* imelalamika Bungeni kuhusu suala hili bila kupitia Waziri. Nina habari tu kwamba Baraza la Wawakilishi lilipitisha kuanzisha *State University* huko Zanzibar na nikafuatilia mwenyewe suala hili linaweza kurekebishwa namna gani na tumekuwa na mawasiliano ya ngazi za juu mpaka kwenye ngazi za juu kabisa upande wa Serikali ya Zanzibar. Tukafikia muafaka kwamba, kwa kuwa Chuo Kikuu hiki kitakuwa kiko chini ya mamlaka ya Muungano, kitatii *conditions* zote za *HEAC* ambazo ni pamoja na udahili wa wanafunzi bila ubaguzi. Kwa hiyo, hili lieleweke hivyo kwamba *State University of Zanzibar* ni Chuo Kikuu cha Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kinaweza kuomba msaada kutoka *TEA* na kikapewa na utaratibu wote wanaufuata. Ili kurekebisha hizi dosari zilizotokea za namna ya kukiunda, *charter* yake na kingeweza kuundiwa hapa, lakini wakaunda upande ule, basi tunaleta Muswada wa Sheria ya Elimu ambao utatoa mwongozo wa jinsi ya kuanzisha Vyuo Vikuu vya Umma na Vyuo Vikuu Binafsi bila kupitia Bungeni mradi tu wamefuata tu sheria mama. Tungependa kuleta Muswada huo mapema iwezekanavyo, mkituweka kwenye ratiba tunataka mwezi Oktoba tuwe tumeleta Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyeti bandia, suala hili namshukuru Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kwa kulileta, nilikuwa sina habari nani ana cheti bandia

katika Vyuo Vikuu vyetu. Ni vizuri kama wanajulikana hao tunawapeleka tena kwenye *HEAC* wakaweze kutathminiwa vyeti vyao na jambo hili linaweza likamalizika kwa kuwaambia wakasome zaidi wapate au wapate *accreditation* inayofaa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya mwisho ya maelezo ya Waziri yananiridhisha kidogo, lakini kwa ajili ya rekodi naomba niweke wazi kwamba Mheshimiwa Waziri atakubali kwamba tulikwishakaa kwanza kwenye Kamati ikarudishwa ile barua kwamba Serikali iifanyie kazi. Halafu baada ya pale tukakaa na Naibu Waziri kwa kuwa siku ile Waziri hakuwepo na alikuwepo vile vile Katibu wa Baraza na wakanihakikishia kwamba suala hilo wanalishughulikia. Sasa leo Waziri anapotamka ndani ya Bunge kwamba hana taarifa anataka kukana kwamba Naibu Waziri wake aliyofanya sio sehemu ya kazi ya Waziri?

**MWENYEKITI:** Pengine kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Waziri nilitaka kusema, hii barua ambayo unaizungumzia *for the sake of Hansard* kama ulivyosema, ni barua iliandikwa na nani kwenda kwa nani ili wote hapa tuelewe ni nini?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Barua hii iliandikwa na Katibu wa Baraza akieleza jinsi *State University of Zanzibar* ilivyoanzishwa na akaandika...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Baraza lipi?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Baraza la Ithibati, Baraza ni moja tu tunalolizungumza hapa, ni Baraza la Ithibati. Wale wasiojua Baraza la Ithibati ni *Higher Education Accreditation Council.* Kwa hiyo, barua hiyo iliandikwa kwa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati tukakubaliana kwa muafaka pale kwamba ili tusifumue mgogoro wa Kikatiba, tuirudishe Serikalini. Lakini ni miaka mitatu na baada ya pale mimi nikawa nafuatilia suala hilo.

Waziri akamtuma Naibu Waziri pamoja na maofisa wa Wizara yake tukakaa tukajadili, wakaniambia kwamba watalifikisha mwisho. Sasa ndiyo nashangaa leo ndani ya Bunge Waziri anasema hana taarifa. Nilitaka kuweka rekodi kwamba rekodi sahihi Waziri angetueleza kwamba tumekwishalishughulikia kwa utaratibu ambao mimi mwishoni nimekuja kuukubali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri hiyo barua inayotajwa uliipokea?

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo barua inayotajwa sijaiona wala sijaisoma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge anasema ilionekana na Waziri anasema hajaipata. Kwa hiyo...

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaitafuta ile barua, nita-*submit* lakini Naibu Waziri ni shahidi kwamba tulifanya kikao kwenye jengo la Bunge pamoja na Katibu wa Baraza. Sasa kama hakuna mawasiliano ndani ya Wizara, hilo ni tatizo kubwa kabisa ambalo lazima tulifanyie kazi.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tatizo hapa linalotokea ni kukosea utaratibu. Kwa sababu huyo Katibu hakutakiwa kupeleka barua ya namna hiyo katika Kamati ya Bunge. Alitakiwa apeleke barua yake katika vyombo vya Serikali vinavyohusika viifanyie kazi, ndiyo baadaye ije kwenye Kamati ya Bunge.

Kwa hiyo, taratibu hizo zikikosewa, ndiyo zinaleta matatizo ya namna hii. Kwa hiyo, tunaomba watu wote wajue kwamba kuna taratibu, kuna Serikali, Bunge na Mahakama, ndivyo tunavyokwenda, tukichanganya hivi vitu, tutagongana hapa bila sababu. Kwa hiyo, nina hakika barua hiyo itawasilishwa kwenye *channel* za Serikali zinazohusika, itafanyiwa kazi kana kwamba wala hili la Kamati halijahusika. Ahsante. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3002 - *Technical Education* ... ... ... ... ... ... ... ... 6,168,151,400/=
Kifungu 3003 - *Science and Technology* ... ... ... ... ... ... ... 1,739,935,600/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 68 - Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... 256,000,000/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... ...192,436,300/=
Kifungu 3001 - *Higher Education* ... ... ... ... ... ... ... ... ...12,882,014,500/=
Kifungu 3002 - *Technical Education* ... ... ... ... ... ... ... ... ...450,000,000/=
Kifungu 3003 - *Science and Technology* ... ... ... ... ... ... ... 250,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU JUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa mwaka wa fedha 2004/2005, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadiiro ya Matumizi ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Baada ya kufika hapo tumemaliza shughuli za leo, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.55 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne tarehe 20 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*